

**UCHANGANUZI WA VIJENZI UNGANISHI VYA  
MSHIKAMANO KATIKA MATINI ZA KIKISII**

**NA**

**OPANDE NILSON ISAAC**

**TASNIFU ILIYOTOLEWA ILI KUTIMIZA BAADHI YA  
MAHITAJI YA D.PHIL KISWAHILI KATIKA CHUO KIKUU  
CHA MOI, ELDORET.**

**2015**

## **IKIRARI**

Kazi hii ni yangu mwenyewe na haijawahi kuwasilishwa katika chuo kikuu chochote ili kutimiza baadhi ya mahitaji ya shahada yoyote. Sehemu yoyote ya tasmifu hii hairuhusiwi kutoleshwa bila ya ridhaa yangu na/au ya chuo kikuu cha Moi.

---

**OPANDE NILSON ISAAC**

SASS/DPHIL/KIS/05/2010

---

**TAREHE**

Tasmifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi wa chuo kikuu.

---

**PROF. OGECHI NATHAN  
IDARA YA KISWAHILI NA  
LUGHA NYINGINE ZA KIAFRICA,  
CHUO KIKUU CHA MOI,  
ELDORET.**

---

**TAREHE**

---

**DR. ODUORI ROBERT  
IDARA YA KISWAHILI NA  
LUGHA NYINGINE ZA KIAFRICA,  
CHUO KIKUU CHA MOI,  
ELDORET.**

---

**TAREHE**

## **TABARUKU**

Tasnifu hii nawatabarukia wapenzi wa lugha ya Kiswahili: walimu na wanafunzi wote wanaoshughulikia na watakaoshughulikia tafiti mbalimbali za Kiswahili. Mwenyezi Mungu awaimarishe katika kumbi za utafiti na usomi wa Kiswahili; awafanye muwe watetezi wa Kiswahili. Mkienzi na kukikuza siku zote. Kiswahili kiwe ndiyo bendera yenu na wimbo wenu wa uzalendo.

## **ABSTRACT**

Cohesion and coherence are very essential in enabling communication. Cohesion and coherence are effected by use of different devices; among these devices are conjunctive forms. This study analyzes the Morphology, Syntax and Semantics of the conjunctive forms, structure, interrelatedness and semantic functions. The research uses Systemic Functional Grammar (SFG) to study and analyze how conjunctive forms in Gusii spoken texts enhance cohesion and coherence. The study is guided by the principle of SFG that language is formed of closed systems that enhance meaning. It is also embodied in the principle of SFG that the biggest importance of language is its meaning in societal context. The research is also built on the SFG's principle that lays emphasis on text to analyse how different conjunctive forms are used in Gusii spoken texts so as to effect cohesion and coherence and which other functions they play when used in Gusii spoken texts. The researcher tape-recorded monologic narratives and naturally occurring conversations on different issues of life by different Gusii speakers. He embarked on intentional sampling of four native speakers of the Gusii language to help him in grammaticality judgment; in determining the acceptability of the identified conjunctive forms by the Gusii natives. He later engaged his linguistic competence in analysing the functions of the identified forms in particular texts. The study found out that the conjunctive forms in Gusii spoken texts have distinctive forms and structures. It also concluded that these conjunctive forms are interrelated and that apart from enhancing cohesion and coherence they also have other pragmatic and semantic functions. The study recommends that there be done studies in other Bantu languages to establish which other functions apart from cohesion and coherence are effected by conjunctive forms. Also there is need to do studies to realize whether in those languages, there is interrelatedness of the different conjunctive forms. There is also need to carry out research on different conjunctive forms basing on different theoretical frameworks to realize whether the functions witnessed in this study are also evident.

## IKISIRI

Mawasiliano hayawezi kukamilika bila ya kuwepo kwa mshikamano na muwala katika matini. Yamkini mshikamano na muwala huweza kufanikishwa kwa matumizi ya vijenzi mbalimbali. Miongoni mwa vijenzi hivyo ni vijenzi unganishi vya mshikamano. Utafiti huu unachunguza na kuchanganua jinsi vijenzi unganishi vya mshikamano (VUM) hufanikisha mshikamano na muwala katika matini semwa za Kikisii. Unachambua Mofolojia, Sintaksia na vilevile Semantiki ya VUM kwa lengo la kubainisha wazi maumbo ya VUM hivyo pamoja na alomofu zake, miundo ambamo maumbo hayo yanajitokeza, kuingiliana kwa VUM hivyo pamoja na amali zinazotekelezwa na VUM hivyo. Nadharia ya sarufi Msonge Amilifu (SMA) ndiyo iliyotumika katika utafiti huu. Misingi ya SMA iliyotumika katika utafiti huu ni kuwa lugha ni mfumo ulio na mifumo fungo na ambayo ina majukumu ya kutekeleza katika kuibua maana za aina mbalimbali na hivyo kufanikisha amali mbalimbali. Utafiti huu pia ulijifunga katika msingi wa SMA kuwa umuhimu mkubwa wa lugha ni maana katika muktadha wa jamii. Mtafiti alijikita katika kunasa hadithi na vilevile mazungumzo kuhusu mada mbalimbali baina ya wazungumzaji wazawa wa Kikisii ili kupata matini mbalimbali. Baada ya kunasa sauti, alinakili data zilizokusanya na kisha kuteua VUM kama vilivyobainika katika matini hizo. Mtafiti alifanya uteuzi kimakusudi wa wasailiwa wanne ambao walimsaidia katika kuzithibitisha data. Aidha, alitumia ujuzi wake wa kiisimu katika kupambanua maumbo na miundo ya VUM hivyo. Utafiti huu ulibaini kuwa VUM katika matini semwa za Kikisii huwa na maumbo na miundo maalumu. Aidha, ulibaini kuwa VUM hivi huingiliana na kukamilishana na kuwa kando na kutekeleza mshikamano VUM hivi hufanikisha amali nyingine kipragmatiki na pia kisemantiki. Utafiti ilibainisha kuwa pana haja ya kufanya tafiti mbalimbali katika lugha nyingine za kibantu ili kubaini iwapo VUM katika lugha hizo huwa na amali nyingine muhimu kando na kufanikisha mshikamano na upatanifu na vilevile iwapo VUM katika lugha hizo huingiliana na kukamilishana. Isitoshe, palibainika haja ya kufanywa tafiti nyingine kuhusu VUM kwa kurejelea nadharia nyingine ili kubaini iwapo hali zilizotokeza katika utafiti huu zinaweza pia kubainika katika tafiti hizo nyingine zilizopendekezwa.

## YALIYOMO

|  |           |
|--|-----------|
| IKIRARI .....  | ii        |
| TABARUKU.....  | iii       |
| ABSTRACT.....  | iv        |
| IKISIRI .....  | v         |
| <b>YALIYOMO .....</b>                                      | <b>vi</b> |
| ORODHA YA VIFUPISHO NA VIELELEZO.....                      | ix        |
| VIJELEZI VYA ISTILAHİ .....                                | xii       |
| SHUKURANI .....  | xiii      |
| <b>SURA YA KWANZA .....</b>                                | <b>1</b>  |
| MISINGI YA UTAFITI.....                                    | 1         |
| 1.1 USULI WA SUALA LA UTAFITI.....                         | 1         |
| 1.2 SUALA LA UTAFITI .....                                 | 6         |
| 1.3 MADHUMUNI YA UTAFITI .....                             | 7         |
| 1.4 NADHARIA TETE .....                                    | 7         |
| 1.5 UPEO .....   | 8         |
| 1.6 UMUHIMU WA UTAFITI.....                                | 9         |
| 1.7 NADHARIA YA UTAFITI .....                              | 10        |
| 1.8 MBINU ZA UTAFITI .....                                 | 18        |
| 1.8.1 ENEO LA UTAFITI NA WATAFITIWA.....                   | 18        |
| 1.8.2 LUGHA ILIYOTAFITIWA .....                            | 18        |
| 1.8.3 SAMPULI.....   | 20        |
| 1.8.4 VIFAA .....  | 21        |
| 1.8.5 MBINU ZA UKUSANYAJI WA DATA .....                    | 22        |
| 1.8.6 UCHANGANUZI WA DATA .....                            | 25        |
| 1.8.7 MUHTASARI WA DATA.....                               | 27        |
| <b>SURA YA PILI .....</b>                                  | <b>31</b> |
| DHANA YA MSHIKAMANO NA YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA .....     | 31        |
| 2.0 Utangulizi .....                                       | 31        |
| 2.1 Dhana ya mshikamano .....                              | 31        |
| 2.1.1 Urejeshaji.....                                      | 32        |
| 2.1.2 Uwakilishaji.....                                    | 34        |
| 2.1.3 Udondoshaji .....                                    | 35        |
| 2.2 Vipatanishi vya kileksimu .....                        | 42        |
| 2.3 Hitimisho .....  | 59        |
| <b>SURA YA TATU .....</b>                                  | <b>60</b> |
| MAUMBO NA MIUNDO YA VIJENZI UNGANISHI VYA MSHIKAMANO ..... | 60        |
| 3.0 Utangulizi .....                                       | 60        |
| 3.1 MAUMBO, MIUNDO NA AINA ZA VUM (VIUNGANISHI).....       | 60        |
| 3.1.1 Vya mofu moja .....                                  | 60        |
| Ko.....  | 61        |
| Na.....  | 62        |
| 3.1.2 Vya neno moja .....                                  | 63        |
| Gose .....   | 63        |
| Na.....  | 65        |
| Aba .....  | 67        |

|   |     |
|---|-----|
| Ani .....   | 69  |
| Korende .....   | 70  |
| Omanyete .....  | 72  |
| Kobua .....   | 73  |
| Ekiagera .....  | 74  |
| 3.1.2.2.4 VUM vinavyotokana na MZZ ya –b- (kuwa) .....    | 76  |
| Okoba .....   | 76  |
| Neba .....  | 77  |
| 3.1.2.2.5 VUM vinavyotokana na MZZ ya –ik- (fika) .....   | 78  |
| Goika .....   | 78  |
| 3.1.2.2.6 VUM vinavyotokana na MZZ ya –nyor- (pata) ..... | 79  |
| Oranyore .....  | 79  |
| 3.1.2.2.7 VUM vinavyotokana na MZZ ya –tig- (acha) .....  | 80  |
| Otatiga .....   | 80  |
| Obobe .....   | 81  |
| Omanyе .....  | 83  |
| Omanya .....  | 84  |
| Tomanyе .....   | 85  |
| Mono .....  | 86  |
| Naende .....  | 87  |
| Ekero .....   | 89  |
| Bono .....  | 90  |
| Erio .....  | 91  |
| Erinde .....  | 91  |
| Egere .....   | 92  |
| Igo .....   | 93  |
| 3.1.3    VUM vilivyo na muundo wa Kirai .....             | 94  |
| Ase engencho .....  | 94  |
| Ribaga ria .....  | 95  |
| Ase obwenge .....   | 96  |
| Ase igo .....   | 97  |
| Magega yayu .....   | 98  |
| Ase ekeene .....  | 99  |
| Ase enchera ende .....                                    | 100 |
| Ase bono .....  | 100 |
| Ase ogokorera ekeene .....                                | 101 |
| Ase bono iga .....  | 102 |
| Ase chingaki echo .....                                   | 103 |
| Kobua mono .....  | 104 |
| Komenta nayu .....  | 105 |
| Naki gekogera .....                                       | 106 |
| Kobwati ayu .....   | 107 |
| Goikera bono .....  | 108 |
| Goikera abu .....   | 109 |
| Otatiga bono .....  | 110 |
| Kobwatekani naywo .....                                   | 111 |

|   |     |
|---|-----|
| Nabo oranyore .....   | 112 |
| Omoerio oye .....   | 113 |
| Mambi yaye .....  | 114 |
| Ekeru ekio gionsi .....   | 115 |
| Chinsa echio echio .....  | 115 |
| Igo bono .....  | 116 |
| Bono bono .....   | 117 |
| Bono ekero .....  | 118 |
| Rirorio onye .....  | 119 |
| Buna bono .....   | 120 |
| Erinde erio .....   | 121 |
| 3.1.3.4 VUM vilivyo na muundo wa virai vinavyotokana na viunganishi ..... | 121 |
| Nonya nigo .....  | 121 |
| Ase enchera ende oku n'ogoteba nga .....                                  | 123 |
| Eki ngoteba nkeri nga .....   | 124 |
| Eki ngotebera bo nkeri nga .....  | 126 |
| Buna narenge goteba .....   | 127 |
| Igo n'ogoteba nga .....   | 128 |
| Nonya kere boigo .....  | 129 |
| Nonya tari boigo .....  | 130 |
| 3.2 MAUMBO, MIUNDO NA AINA ZA VUM (LEKSIMU PATANIFU) .....                | 131 |
| 3.2.1 Udondoshaji .....   | 131 |
| 3.2.2 Uradidi .....   | 138 |
| 3.2.3 Visawe unganishi .....  | 143 |
| 3.2.4 Jina la jumla .....   | 145 |
| 3.3. Hitimisho .....  | 147 |
| <b>SURA YA NNE</b> .....  | 148 |
| <b>MWINGILIANO WA VIJENZI UNGANISHI VYA MSHIKAMANO</b> .....              | 148 |
| 4.0 Utangulizi .....  | 148 |
| 4.1 Mwingiliano wa LP na U .....  | 148 |
| 4.2 Mwingiliano wa U na U .....   | 163 |
| 4.3 Hitimisho .....   | 165 |
| <b>SURA YA TANO</b> .....   | 166 |
| <b>AMALI ZINAZOTEKELEZWA NA VIJENZI UNGANISH VYA MSHIKAMANO</b> .....     | 166 |
| 5.0 Utangulizi .....  | 166 |
| 5.3 Upanuzi .....   | 177 |
| 5.5 Zidishi/endelezi .....  | 189 |
| 5.6 Hitimisho .....   | 208 |
| <b>SURA YA SITA</b> .....   | 210 |
| <b>HITIMISHO, MCHANGO WA UTAFITI NA MAPENDEKEZO</b> .....                 | 210 |
| 6.0 Utangulizi .....  | 210 |
| 6.1 Hitimisho .....   | 210 |
| 6.3 Mapendekezo .....   | 214 |
| <b>MAREJE</b> .....   | 215 |
| <b>VIAMBATISHO</b> .....  | 218 |

## ORODHA YA VIFUPISHO NA VIELELEZO

|       |   |   |
|-------|---|---|
| E     | ➔ | KIELEZI                                     |
| H     | ➔ | KIHUSISHI                                   |
| ID    | ➔ | IDADI                                       |
| IDU   | ➔ | IDADI YA UMOJA                              |
| IDW   | ➔ | IDADI YA WINGI                              |
| IT    | ➔ | IRABU TAMATI                                |
| ITKAN | ➔ | IRABU TAMATI KANUSHI                        |
| K     | ➔ | KAULI                                       |
| KAN   | ➔ | KANUSHI                                     |
| KAT   | ➔ | KIAMBISHI AWALI TANGULIZI                   |
| Kat   | ➔ | KIAMBISHI AWALI CHA KITENZI (verbal prefix) |
| KE    | ➔ | KIRAI ELEZI                                 |
| KH    | ➔ | KIRAI HUSISHI                               |
| KIM   | ➔ | KIIMARISHI                                  |
| Kj    | ➔ | KIREJESHI                                   |
| KN    | ➔ | KIRAI NOMINO                                |
| KNNA  | ➔ | KIAMBISHI NOMINO AWALI                      |
| KUM   | ➔ | KIJENZI UNGANISHI CHA MSHIKAMANO            |
| KT    | ➔ | KIRAI KITENZI                               |
| KTJ   | ➔ | KIAMBISHI CHA KITENZI JINA                  |
| KTK   | ➔ | KIAMBISHI TAMATI KIKANUSHI                  |
| KV    | ➔ | KIRAI VUMISHI                               |

|       |   |                       |
|-------|---|-----------------------|
| LP    | ➔ | LEKSIMU PATANISHI     |
| MAT   | ➔ | MATILABA              |
| MZZ   | ➔ | MZIZI                 |
| N     | ➔ | NOMINO                |
| NFS   | ➔ | NAFSI                 |
| NFS1U | ➔ | NAFSI YA KWANZA UMOJA |
| NFS1W | ➔ | NAFSI YA KWANZA WINGI |
| NFS2U | ➔ | NAFSI YA PILI UMOJA   |
| NFS2W | ➔ | NAFSI YA PILI WINGI   |
| NFS3U | ➔ | NAFSI YA TATU UMOJA   |
| NFS3W | ➔ | NAFSI YA TATU WINGI   |
| NGL   | ➔ | NGELI                 |
| NJ    | ➔ | NJEKO                 |
| OP    | ➔ | WAKATI ULIOPPO        |
| PING  | ➔ | PINGANIFU             |
| PT    | ➔ | WAKATI ULIOPITA       |
| S     | ➔ | SENTENSI              |
| SK    | ➔ | KISHAZI KIKUU         |
| SM    | ➔ | S1MULIZI              |
| SMA   | ➔ | SARUFI MSONGE AMILIFU |
| T     | ➔ | KITENZI               |
| t     | ➔ | KITENZI KISHIRIKISHI  |
| Ts    | ➔ | KITENZI KISAIIDIZI    |

|     |   |                                  |
|-----|---|----------------------------------|
| U   | ➔ | KIUNGANISHI                      |
| UJ  | ➔ | WAKATI UJAO                      |
| UT  | ➔ | USEMI TENDI                      |
| V   | ➔ | KIVUMISHI                        |
| VUM | ➔ | VIJENZI UNGANISHI VYA MSHIKAMANO |
| W   | ➔ | KIWAKILISHI                      |
| *   | ➔ | MUUNDO/UMBO LISILO LA KISARUFI   |

## VIJELEZI VYA ISTILAHİ

**Kipashio kiini** – Sehemu ya matini inayochukuliwa kuwa muhimu zaidi kwa kuwa inakaliwa na kipengee kinachotafitiwa.

**Kiunganishi** – Kijenzi cha kiisimu ambacho hufanya kazi ya kuweka pamoja neno na neno, kundi/kirai na kingine au kishazi na kingine

**Leksimu patanishi** – Kipashio ambacho kinafanya kazi ya kuweka pamoja vishazi katika matini.

**Matini** – Kifungu cha diskosi chenye urefu wowote na ambacho ni semwa.

**Mshikamano** – Hali ya vipashio na viambajengo mbalimbali vya lugha kuingiliana na kukamilishana kwa kusudi la kukamilisha maana.

**Msonge** – Hali ya lugha kuwa mfumo wa mtandao au uhusiano wa seti mbalimbali za chaguzi ambao unaleta maana.

**Sarufi Msonge Amilifu** – Nadharia inayochukulia lugha kuwa mfumo wenye utando ambao una jukumu la kuibua maana kutokana na matumizi ya vijenzi mbalimbali vya mshikamano.

**Vijenzi unganishi vya mshikamano** – Vijenzi vya kiisimu (viunganishi/virai elezi/virai husishi au leksimu patanishi) ambavyo hufanya kazi ya kufanikisha mshikamano katika matini.

**Uamilifu** – Uwezo wa kutekeleza jukumu fulani

**Muwala** - Kule kuwiana kwa maana anayokusudia mse maji na ile anayofasiri msikilizaji

## SHUKURANI

Natoa shukurani za dhati kwa Mwenyezi Mungu kwa kunijalia neema, rehema na fadhili na kwa kuniwezesha kumaliza safari hii ya masomo ya uzamifu. Nawashukuru wasimamizi wangu Prof. Ogechi, N.O. na Dkt. Oduori, R.W. kwa kujitolea kwao bila ya kuchoka kunielekeza na kuniongoza katika utafiti huu. Pia Namshukuru marehemu Prof. Shitemi, N.L na Prof. Mwamzandi, I.Y. kwa kunitaalamisha.

Nawashukuru wanafunzi wenzangu Ann Kawa, Joy Mocho, Alexander Rotich, Mudhune na Kitito kwa ushirikiano tuliokuwa nao masomoni. Nyote nawaombea Maulana awape neema na fadhili.

Namshukuru mpenzi wangu Jane Nyaboke kwa kunihimiza katika masomo haya. Wanangu Jesse Opande, Laura Neema na Shanice Zawadi pia nawashukuru kwa mapenzi yenu kwangu na kunitia moyo ili niyakamilishe masomo yangu.

## SURA YA KWANZA

### MISINGI YA UTAFITI

#### 1.0 Utangulizi

Sura hii inaweka wazi usuli wa suala la utafiti huu, inaliweka wazi suala la utafiti na kuyaweka wazi madhumuni ya utafiti. Inabainisha pia upeo na umuhimu wa utafiti wa utafiti huu na kuichanganua nadharia iliyotumika katika utafiti huu kwa kuweka misingi yake wazi na kuonyesha ni kwa jinsi gani misingi hiyo ilivyozingatiwa katika utafiti huu. Isitoshe, sura hii inaweka wazi mbinu zilizotumiwa katika kukusanya data zilizotumika katika utafiti huu na jinsi data hizo zilivyochangانوليوا. Katika sehemu ya mwisho ya sura hii, kumesawiriwa muhtasari wa data zilizokusanywa.

#### 1.1 USULI WA SUALA LA UTAFITI

Mawasiliano ni mchakato unaonuiwa kupitisha ujumbe kutoka kwa mse maji hadi kwa msikilizaji. Mchakato huu unahusisha kuyapanga vizuri yaliyomo akilini mwa mse maji na kuyasimba kwa njia maalumu ambazo zitamwezesha msikilizaji kuyapokea yaliyowasilishwa na kuyasimbua ili kupata maana iliyokusudiwa. Yamkini, lililo muhimu katika mchakato huu wa mawasiliano ni suala la mshikamano na muwala. Mshikamano ni dhana inayorejelea hususan jinsi sentensi, katika maongezi au maandishi, hushikamana pamoja katika kuunda matini inayoleta maana (Finch, 2000:210). Mshikamano unahusisha matumizi ya njia na vigezo maalumu vinavyokubalika ili kupokeza ujumbe kutoka kwa mse maji hadi kwa msikilizaji.

Mshikamano hurejelea uhusiano uliopo katika matini na hutokea pale ambapo ufasiri wa elementi fulani katika usemi hutegemea ule wa elementi nyingine (Halliday na Hassan, 1976:4). Katika elementi hizi mbili zinazobeba mshikamano wa uhusiano, moja kwa kawaida hufuata nyingine. Kwa mujibu wa Barongo (1996) kutegemeana ndilo jambo kuu katika mshikamano kwani kipashio kimoja katika matini lazima kitegemee kingine ili kuleta mshikamano na umoja unaoleta maana kamili na kuwezesha maelewano. Kilicho cha msingi mno katika mshikamano ni ile hali ya kutegemeana; kwamba elementi moja haiwezi kufafanuliwa bila ya kurejelea nyingine katika matini iwe ama moja imetangulia au imefuata nyingine. Salkie (1995) anadai kuwa urejeleaji, ubadilishaji na udondoshaji na uunganishaji ni vipengele muhimu sana katika kuwezesha mshikamano katika matini. Anadai kuwa vipengele hivi ndivyo huwezesha kule kushikamana kwa sehemu tofauti za matini na kuifanya kuwa na mfungamano na hivyo kuifanya matini kuwa na mtiririko na maana.

Ni kweli kama anavyodai Salkie (1995) kuwa mshikamano una umuhimu mkubwa katika kuifanya matini ieleteweke na ama msomaji au msikilizaji. Muwala kwa upande wake unahusisha kule kuwiana kwa maana kati ya kile anachokusudia mse maji na kile anachofasiri msikilizaji. Ili mchakato mzima wa mawasiliano uweze kukamilika na muwala uafikiwe, ni lazima kuwepo na mshikamano katika jumbe zinazotolewa.

Mshikamano huweza kutokana na matumizi ya vijenzi mbalimbali. Halliday na Hasan (1976) wanatambulisha vijenzi hivi vya mshikamano kuwa ni: urejeshaji, uwakilishaji, udondoshaji, uunganishi na vipatanishi vya kileksia. Halliday (1985) anafafanua vijenzi hivi kwa undani; anabainisha aina mbalimbali za viunganishi na kudai kuwa viunganishi hivi vinajitokeza katika nafasi maalumu katika tungo na kuwa vina amali maalumu. Miongoni mwa maumbo na miundo ya vijenzi vya mshikamano iliyopambanuliwa na Halliday na Hasan (1976) na Halliday (1985) inajitokeza katika mifano ifuatayo:

## MF 1<sup>1</sup>

- a<sup>1</sup>) He was very uncomfortable. **Nevertheless** he fell asleep  
(Hakuwa anahisi vizuri. **Ingawa hivyo** alipatwa na usingizi)
- a<sup>2</sup>) **Although** he was very uncomfortable, he fell asleep  
(**Ingawa** hakuwa anahisi vizuri, alipatwa na usingizi)
- b) They fought a battle. **Afterwards**, it snowed.  
(Walipigana vita. **Baadaye**, kulinyesha dhoruba ya theluji)

Katika **MF1<sup>1</sup>** kunajitokeza vipashio ‘*nevertheless*’ na ‘*although*’ vipashio hivi vinabainika kuwa na jukumu la kuunganisha sehemu mbili za matini husika ambazo ni ‘*he was very uncomfortable*’ (hakuwa anahisi vizuri) na ‘*he fell asleep*’ (alipatwa na usingizi) katika **MF1a<sup>1</sup>** na **MF1a<sup>2</sup>**. Kipashio ‘*afterwards*’ kilichotumika katika **MF1b** nacho kinadhikirika kuwa na jukumu la kuunganisha sehemu mbili husika: ‘*They fought a battle*’ (walipigana vita) na ‘*It snowed*’ (kulinyesha dhoruba ya theluji). Vipashio hivi vinaweza kuchukuliwa kuwa ni viunganishi (U).

Halliday na Matthiessen (2004) nao wanadai kuwa mshikamano katika matini pia huweza kufanikishwa kutokana na matumizi ya leksimu patanishi:

### **MF1<sup>2</sup>.**

a) Algy met a bear. The **bear** was bulgy.

(Algy alikutana na dubu. **Dubu** huyo alikuwa mkubwa)

b) He fell asleep. What **woke** him was a loud crash

(Alihisi usingizi. **Kilichomwamsha** ni kishindo kikubwa)

Vijenzi viliyvoandikwa kwa wino mzito katika **MF1<sup>2</sup>** ni leksimu ambazo zinapatanisha sehemu moja ya matini na nyingine. Kwa kuwa leksimu hizi zinapatanisha sehemu mbili za matini zinazoweza kujisimamia, zinaweza kuchukuliwa kuwa ni leksimu patanishi (LP). LP hizi ni tofauti na maumbo na miundo inayojitokeza katika **MF1<sup>1</sup>** ambayo inatambulishwa kuwa ni viunganishi (U). Ingawa kunadhihirika tofauti hii, udadisi unaonyosha kuwa U na LP vyote vinatekeleza jukumu muhimu la kuleta mshikamano katika matini vilimotumika. Sababu hii inapelekea utafiti huu kuchukulia kuwa U pamoja na LP ni vijenzi unganishi vya mshikamano (VUM).

Katika **MF1<sup>1</sup> b**, kipashio ‘**afterwards**’ kimetumika. Ingawa kipashio hiki kimetumika ili kuunganisha vishazi katika sentensi kilimotumika, inabainika kuwa kina amali nyingine tofauti na hii; kwamba kinaonyesha msururu wa matukio. Kinabainisha kuwa vita vilitangulia ile dhoruba ya theluji. Katika **MF1<sup>2</sup>a** neno ‘**bear**’ limetumika kuleta mshikamano baina ya vishazi viwili husika: ‘Algy met a bear’ na ‘The bear was bulgy.’ Mshikamano katika kifungu hiki cha matini umefanikishwa na kurudiwa kwa neno ‘bear’ hasa kama inavyojitokeza katika kishazi cha pili.

Katika **MF1<sup>2b</sup>** ‘He fell asleep. What woke him was a loud crash’ neno ‘woke’ limetumika ili kufanikisha mshikamano baina ya vishazi ‘he fell asleep’ na ‘what **woke** him was a loud crash’. Neno hili ‘**woke**’ ni antonimu ya neno ‘sleep’ ambalo limetumika katika kishazi tangulizi. Katika **MF1<sup>2b</sup>**, mshikamano umefanikishwa na matumizi ya antonimu.

Mifano iliyotolewa hapo juu pia inaweza kujitokeza katika Kikisii:

## **MF 2<sup>1</sup>.**

a) Moraa tasometi nomokia, /*ase igo, takoreti buya ase amatemu aye*.

Moraa ti-a-som-et-i na omokia, /*ase igo, ti-a-kor-et-i buya ase a-ma-temu a-ye*

Moraa KAN-NFS3U-MZZ-NJ-IT H N/ (U) KAN- NFS3U-MZZ- NJ- IT E H KAT-IDW-MZZ NFS3W- MZZ

(Moraa hakusoma kwa bidii, ***kwa sababu hiyo***, hakufanya vyema katika mitihani yake)

b) Omogeni nacha. /*Mogeni oyu tarenteti kende*

o-mo-geni ni-a-ch-a. /*Mo-geni oyu ti-a-rent-et-i kende*

KAT-IDU-geni KIM-NFS3U-MZZ-IT. IDU-geni (LP) oyu KAN-NFS3U-MZZ-MAT-IT kende

(Mgeni alikuja. Mgeni huyo hakuleta chochote)

Vipashio U katika **MF2<sup>1a</sup>** na LP katika **MF2<sup>1b</sup>** vinadhihirika kuwa na jukumu muhimu la kuwezesha mshikamano katika tungo vilimotumika. Kando na mshikamano, vipashio hivi vinadhihirika kutekeleza amali nyingine ambazo zinahitaji kuchanganuliwa.

Msingi wa usuli huu uliufanya utafiti huu kuchukulia kuwa U pamoja na LP vyote ni VUM kwa kuwa vinatekeleza jukumu la kuunganisha sehemu moja ya matini na nyingine. Isitoshe, usuli huu ndio uliozua hoja iliyoufanya utafiti huu kulichunguza suala hili kwa undani ili kuchunguza VUM katika matini semwa za Kikisii hasa U na LP kwa

lengo la kubainisha maumbo, alomofu na miundo ya VUM hivi na vilevile kubaini amali zake: je, U na LP huingiliana na kutekeleza amali sawa au kila mojawapo huwa na amali tofauti.

Utafiti huu pia ulichunguza iwapo U na LP huweza kutokea pamoja katika tungo za matini na ni kwa jinsi gani VUM huchangia katika kuelekeza fahiwa ya msikilizaji na ufasiri wa maana; hali inayochangia pakubwa katika kufanikisha mshikamano na muwala katika matini.

## **1.2 SUALA LA UTAFITI**

Utafiti huu ulilenga kuchunguza jinsi ambavyo vijenzi unganishi vya mshikamano hasa viunganishi na leksimu patanishi huwezesha mshikamano katika matini semwa za Kikisii na kupambanua amali nyingine kando na mshikamano ambazo hufanikishwa na VUM hivyo katika matini semwa za Kikisii. Utafiti huu ulibainisha aina mbalimbali za VUM: viunganishi (U) na Leksimu patanishi (LP) hivyo na kuchanganua jinsi vinajitokeza katika nafasi maalumu katika tungo ili kufanikisha amali maalumu. Aidha, ulichunguza maumbo na miundo ya VUM katika matini semwa za Kikisii na vilevile kuchunguza iwapo VUM hivyo vinaingiliana na kukamilishana. Isitoshe, utafiti huu ulichunguza iwapo VUM vinatekeleza amali nyingine tofauti na ile ya kuwezesha mshikamano.

### **1.3 MADHUMUNI YA UTAFITI**

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza jinsi ambavyo vijenzi unganishi nya mshikamano hasa viunganishi na leksimu patanishi huwezesha mshikamano katika matini semwa za Kikisii na kupambanua amali nyingine kando na mshikamano ambazo hufanikishwa na VUM hivyo katika matini semwa za Kikisii. Ili kufikia lengo hili, utafiti huu uliongozwa na madhumuni yafuatayo:

- a) Kuchanganua maumbo na miundo ya VUM (U na LP) katika matini semwa za Kikisii.
- b) Kufafanua jinsi VUM katika matini za Kikisii huingiliana na kukamilishana.
- c) Kupambanua jinsi VUM hufanikisha mshikamano katika matini za Kikisii.
- d) Kuchunguza amali nyingine kando na mshikamano zinazotekeliza na VUM katika matini za Kikisii

### **1.4 NADHARIA TETE**

Utafiti huu uliongozwa na nadharia tete zifuatazo:

- a) VUM huwa na maumbo na miundo maalumu.
- b) Aina mbalimbali za VUM katika matini semwa za Kikisii huingiliana na kukamilishana.
- c) VUM hufanikisha mshikamano katika matini semwa za Kikisii.
- d) Kando na mshikamano, VUM hutekeleza amali mbalimbali katika matini semwa za Kikisii.

## 1.5 UPEO

Utafiti huu ulijikita katika kuchunguza na kuchanganua jinsi VUM hufanikisha mshikamano katika matini semwa za Kikisii. Ulichunguza maumbo na miundo mbalimbali ya VUM katika matini semwa za Kikisii na kubaini ni amali gani nyingine kando na mshikamno ambazo VUM hivi vinaweza kufanikisha. Ili kubaini VUM mbalimbali, mtafiti alizingatia matini semwa za Kikisii. Utafiti alichunguza matini semwa kwa kuwa inaaminika kuwa ni katika usemaji ambapo utendaji halisi wa lugha hutokea katika mazingira halisi; usemaji ni asilia zaidi ya maandishi.

Utafiti ulichanganua matini semwa za Kikisii kwa nia ya kupambanua maumbo na alomofu za VUM pamoja na miundo yake. Ulibaini jinsi VUM huingiliana na kukamilishana katika matini semwa za Kikisii na jinsi VUM hivyo hutekeleza amali mbalimbali. Ulijikita katika maoni ya Halliday (1976 & 1985) kuwa maana katika lugha hutokana na jinsi ambavyo vijenzi mbalimbali vyta mshikamano vinatumika katika matini.

Kipashio kilichozingatiwa katika utafiti huu ni tungo zilizoteuliwa kutoka kwa matini semwa za kikisii. Tungo zilizoteuliwa ni zile zilizokuwa na:

- Sentensi ambatano ambazo zina vishazi viwili vyenye dhima sawa na ambavyo vimeunganishwa kwa viunganishi ambatishi.
- Sentensi ambatano zinazodhihirisha mtendaji katika kishazi cha pili akiwa ni tofauti na wa kishazi cha kwanza.
- Sentensi ambazo zina miundo unganifu ya vitenzi.
- Vishazi ambavyo vimeunganishiwa vitegemezi ambavyo havina kitenzi.

Utafiti huu ulijikita katika kuchunguza Kikisii cha lahaja ya *Rogoro*. Hii inatokana na sababu kwamba mtafiti ni mzawa wa Kikisii anayezungumza lahaja hii. Hii inaafikiana na maoni ya Vaux na Cooper (1999:93,98) kuwa ni vyema mtafiti atafitie lugha ambayo anafahamu muundo wake wa kisarufi.

Soko la Kegati ndilo lililochaguliwa kuwa eneo lake la utafiti. Soko hili linapatikana Kisii; kati ya miji midogo ya Bobaracho na Keumbu. Sababu ya kuchagua eneo hili ni kuwa wazungumzaji wengi katika eneo hili wanazungumza lahaja ya *Rogoro*. Wengi wa wazungumzaji katika eneo hili wamezaliwa na kulelewa Kisii hadi kufikia utu uzima na wana umilisi wa lugha hiyo. Aidha, wazungumzaji hawa hutumia lahaja ya *Rogoro* wanaposhiriki mazungumzo kuhusu masuala mbalimbali na wakiwa katika miktadha mbalimbali.

## **1.6 UMUHIMU WA UTAFITI**

Kwa kadri mtafiti anavyofahamu, kuna uhaba wa kazi za kiisimu zinazoshughulikia VUM katika lugha ya Kikisii. Inatarajiwa kwamba utafiti huu utachangia katika kujaza pengo hilo. Aidha, utafiti huu utatoa changamoto kwa wataalamu wengi wa isimu kuchunguza uamilifu wa VUM katika lugha mbalimbali za kibantu.

Kutokana na uchanganuzi wa matini mbalimbali za Kikisii uliofanywa katika uchunguzi huu, nadharia ya SMA imeimarishwa na kuboreshwa zaidi. Ikishikiliwa kuwa Halliday alitumia SMA katika kuchunguza data za Kiingereza (mojawapo ya lugha za kijeruman), Utafiti huu umechangia katika kuhakiki ufaafu wa nadharia hii katika kuchanganua data za Kikisii ambayo ni mojawapo wa lugha za kibantu. Aidha,

data za Kikisii zilizokusanywa katika utafiti huu pia zitaweza kutumika katika tafiti nyingine za baadaye kuhusu maswala ya lugha. Inaaminiwa vilevile kwamba utafiti huu umetoa mchango katika nyanja za Mofolojia, Sintaksia, Semantiki na vilevile Uchanganuzi Matini kwa kuwa umechananua matini mbalimbali za lugha kwa kuhusisha Mofololojia, Sintaksia, Semantiki na Uchanganuzi Matini. Aidha, utafiti huu umejaribu kuonyesha mwingiliano kati ya Mofolojia, Sintaksia na Semantiki katika kufanikisha mawasiliano; lugha haihusishi tu kanuni bali pia mifumo maalumu na chaguzi maalumu zinazofanywa ili kukamilisha mawasiliano.

## **1.7 NADHARIA YA UTAFITI**

Nadharia iliyotumika katika utafiti huu ni ile ya Sarufi Msonge Amilifu. SMA iliasisiwa na Halliday katika mwaka wa 1961. Nadharia hii imeendelezwa na kuboreshwa katika Halliday na Hasan (1976), Hatch (1992), Thompson (2004) na Olateju (2006) miongoni mwa wengine. SMA imejengwa katika mawazo ya kikundi cha wanaisimu wa Prague. Hawa ni kama vile Saussure, Louis Hjelmslev, Malinowski na Firth. Aidha, nadharia hii imechangiwa na misingi ya mawazo ya wanaisimu anthropopolojia wa Marekani kama vile Boas, Sapir na Whorf. Kati ya wote hawa, inaelekea kuwa Halliday ndiye aliyeiendeleza zaidi nadharia hii. Inadaiwa kuwa Halliday alichota pakubwa katika mawazo ya Firth ambako inaaminika ndiko alikozua dhana ya lugha kuchukuliwa kuwa ni mfumo. Halliday anaamini kuwa lugha ilivyo sasa ni tokeo la mabadiliko mbalimbali ambayo imepitia. Aidha, anaamini kuwa lugha ni kama mfumo wenye utando au uhusiano wa seti mbalimbali za chaguzi ambao unaleta maana.

Ingawa nadharia hii inaelezea muundo wa kisintaksia wa lugha, inaweka msisitizo mkubwa katika amali ya lugha (ni nini ambacho lugha inafanya na inakifanya namna gani). SMA inaweka msisitizo mkubwa katika muktadha wa kijamii. Inachunguza ni vipi lugha inafanya kazi na ni vipi lugha hiyo inathibitiwa katika muktadha wa kijamii.

Nadharia ya SMA inachukulia kuwa lugha ni utando wa mifumo au seti za chaguzi zinazoingiliana na ambazo huweza kuibua maana; SMA inachukulia kuwa lugha huwa na majukumu mbalimbali ya kutekeleza. Inajikita katika kuchunguza chaguzi zinazofanywa katika matumizi ya lugha. SMA huchukuliwa kuwa inayochunguza uwezekano uliopo wa raslimali fulani za lugha kutumika badala ya nyingine. Hivyo SMA haielezi lugha kwa kuzingatia kanuni bali huieleza lugha kama mfumo ambao huwezeshe na hali na kupanuliwa na hali hizo zinazoiwezesha na kuwa kila wakati huzalishwa na kuundwa upya katika au kwa matumizi.

Kwa mujibu wa Halliday, miundo mbalimbali ya lugha husawiri tajriba mbalimbali alizo nazo binadamu na huweza kuonyesha jinsi binadamu anavyoingiliana na wenzake katika jamii. Mawazo haya ya Halliday pia yanashikiliwa na Whorf. Whorf anadai kuwa binadamu wanapotumia lugha huwa hawamaanishi dhana sawa/maana sawa. Hii inatokana na hali kuwa kila binadamu ameathiriwa na mazingira na utamaduni wake kwa namna tofauti na alivyoathiriwa binadamu mwingine.

SMA inajishughulisha na kubaini namna matini semwa na matini andikwa hujenga maana na namna raslimali za lugha zimepangiliwa katika mfumo wazi na

zimefungamanishwa kiamali kwa maana. Ni nadharia ya namna lugha inavyotumika kwa kujenga uhusiano kati ya chaguzi na maumbo kati ya pande mbili, upande wa chini ukiwa ni ule wa sarufi na fonolojia na upande wa juu ukiwa ni ule wa muktadha wa hali na muktadha wa utamaduni. Azimio kubwa la SMA ni kuwakilisha mfumo wa kisarufi kama raslimali ya kuunda maana.

Kwa mujibu wa Halliday, msingi mkuu wa nadharia ya SMA ni kuwa tendo lolote la mawasiliano linahusisha uchaguzi. Lugha ni mfumo na kuwa chaguzi zinazopatikana katika aina yoyote ya lugha huundwa kwa kutumia vifaa vyta uwasilishaji vinavyopatikana katika mtandao wa mfumo husika.

### **1.7.1 Misingi ya Sarufi Msonge Amilifu**

Dhana kuu zinazoiwekea msingi SMA ni mfumo, uamilifu na hadhi. Dhana nyingine ni sarufileksia. Halliday anasisitiza kuwa sarufi ni mfumo na wala sio kanuni. Anadai kuwa hii inatokana na hali kuwa kila muundo wa kisarufi unahusisha uchaguzi kutoka kwa seti nyingine za miundo zilizopo na ambazo lau zingeteuliwa na kuwekwa katika matumizi, zingezua maana tofauti. Hivi inachukuliwa kuwa lugha ina uwezo wa kuibua maana mbalimbali.

Halliday anadai kuwa mifumo ya kisarufi ni fungo ilhali mifumo ya kileksimu ni wazi. Anadai hivi kwa kuwa tunaweza kuingiza maneno mapya katika lugha kila uchao lakini hatuwezi kuunda miundo mipyta ya lugha; tunaweza tu kufanya uteuzi kwa kutumia miundo ambayo tayari ipo.

SMA inashikilia kuwa mifumo ya kisarufi huwa na jukumu katika kuunda maana za aina mbalimbali. Huu ndio msingi wa madai ya Halliday kuwa lugha imepangiliwa kwa kuzingatia uamilifu wake. Anadai kuwa jukumu kubwa la lugha ni kutoa maana na kuwa kwa sababu hii lugha zote zina aina tatu za vijenzi vya kisemantiki: Kila lugha ina kijenzi cha kimawazo, kijenzi cha kimahusiano na kijenzi cha kimatini. Kila mfumo wa kisarufi ulioasisiwa na Halliday unahusiana na amali hizi kuu. Halliday anashikilia kuwa lugha ni amilifu; lugha huwa na vijenzi ambavyo ni amilifu na kuwa vijenzi hivyo amilifu ndivyo huamua hali ya mfumo wa lugha na kwa sababu hiyo vinahitaji pia kuhusishwa katika ufanuzi wa mfumo wa lugha.

Dhana ya kileksia huzingatia mahusiano ya kifahiwa pamoja na uradidi wa kileksia. Dhana ya kisarufi kwa upande wake, huzingatia uradidi wa maana ambao unadhihirika kuitia kwa urejeshaji, uwakilishaji na udondoshaji pamoja na jukumu la kuhusisha vielezi. SMA hushughulikia nyanja hizi zote za maana kwa njia sawa katika mfumo wa sarufi wenyewe.

Dhana mbalimbali zilizotambulishwa hapo juu zimebainika kuwa zilizofungamanishwa na misingi ifuatayo ambayo inadhihirika kuwa ndiyo inayojenga nadharia ya SMA:

#### A. Mtazamo wa kifaridi

Msingi huu unashikilia kuwa maana hutegemea chaguzi mbalimbali zinazofanywa. Watumizi wa lugha hufanya uchaguzi wa miundo ya lugha watakayotumia ili kutoa maana wanayokusudia.

### B. Mtazamo wa mpangilio kihadhi

Mtazamo huu hujihusisha na kupangiliwa kwa lugha kutoka kwa viwango vyatini hadi viwango vyati juu. Kuliundwa nafasi au sehemu ambapo maana zingepangiliwa kwa dhana zake zenyewe ambazo ni dhahania na zinaingiliana. Hii iliipelekea lugha kuwa mfumo wa uundaji maana.

### C. Mtazamo wa kienzo amali

Lugha huashiria au kuonyesha ukamilishaji kimaana; kwa maneno mengine, imetokana na hitaji la mwanadamu la kuunda maana kuhusu ulimwengu unaomzunguka na vilevile yale anayoyahisi ndani yake. Vilevile lugha inachukuliwa kuwa ni njia ya kufanikisha mahusiano baina ya watu katika jamii. Halliday anazua vienzo vitatu vyatini kiamali: kienzo cha kimawazo, kienzo cha kimahusiano na kienzo cha kimatini.

#### i) Kienzo cha kimawazo

Kinahusishwa na namna tunavyoolewa tajriba za binadamu. Ni njia inayotuwezesha kusimba mambo tunayokabiliana nayo kwa namna inayowezesha maana. Halliday anakigawa kijenzi hiki katika vitengo viwili: kimantiki na kitajriba. Amali ya kimantiki inahusisha namna vijenzi vyatini kisarufi vinaungana ili kuunda vipashio vikubwa na ambavyo ni changamano. Amali za kitajriba huhusisha namna vipashio vyatini kisarufi vinavyojenga tajriba kupitia kwa vishazi mbalimbali. Kijenzi amali ya kimawazo husawiri muktadha wa nyanja; yaani mchakato wa kijamii inamotumika lugha husika. Uchunguzi wa lugha katika kiwango hiki huhusisha kufanya uchunguzi wa chaguzi zinazofanywa za mifumo ya kisarufi, hii ni pamoja na aina za michakato, aina za

wahusika, aina za hali, ikiunganishwa na uchanganuzi wa namna vishazi vinaunganishwa.

ii) Kienzo amali cha kimahusiano

Kienzo hiki hujihusisha na kuchunguza mahusiano mbalimbali kama vile msemaji/mwandishi, uhusiano baina ya wahusika, mahusiano ya wahusika kihadhi. Hii pia inahusisha kuchunguza mielekeo ya msemaji. Mielekeo hii inaweza kudhihirika kwa kuchunguza iwapo lugha inayotumika ni asi au chanya.

iii) Kienzo amali cha kimatini

Kienzo hiki kinajihuisha zaidi na mpangilio wa ndani wa matini na uwezo wa matini katika kufanikisha mawasiliano. Hii inahusisha kuingiliana kwa matini, kuzuka kwa mada na umbali wa kimawasiliano. Mahusiano katika matini huchunguzwa kwa kuchanganua visitisha mawasiliano kama vile: vituo, uradidi na kadhalika. Uzukaji wa mada huchunguzwa kwa kuchunguza uzito wa kileksia, uchangamano wa kisarufi, namna vishazi vinaingiliana pamoja na matumizi ya virai nomino. Masuala ya kileksia yanajihuisha na mahusiano ya kifahiwa na uradidi wa leksimu ilhali masuala ya kisarufi huchunguza namna uradidi unavyojitokeza kutokana na urejeshaji, uwakilishi na udondoshaji pamoja na jukumu la vielezi ambatishi.

Uchunguzi wa umbali wa kimawasiliano unahusisha kuchunguza mshikamano katika matini. Jinsi matini hiyo inavyoingiliana pamoja na lugha dhahania ambayo imetumika katika matini hiyo. Mshikamano huchunguzwa katika muktadha wa kileksia, kisarufi pamoja na kitoni.

#### D. Mtazamo wa kisintagmatiki

Lugha inachukuliwa kuwa ni muundo unaotolewa kwa wakati fulani au unaochukua nafasi fulani. Muundo huu unahusisha vipashio katika ngazi mbalimbali kama vinavyodhihirika katika mfumo wa lugha. Kwa mfano katika sarufileksia kipashio cha juu zaidi ni kishazi ilhali cha chini zaidi ni mofimu. Kati ya vipashio hivi (cha juu zaidi na cha chini zaidi), kuna kirai na neno.

#### E. Mtazamo wa utukiaji

Mtazamo huu huangazia uhusiano baina ya tukio na mfumo unaowekea msingi tukio hilo. SMA huchukulia kwamba kuna uhusiano wa karibu zaidi baina ya tukio na mfumo wa tukio hilo: hivi, SMA huchukulia kuwa jinsi mfumo fulani unavyowekwa katika matumizi huweza kusababisha athari katika mfumo huo.

Utafiti huu ulijikita katika misingi ya SMA kuwa lugha ni mfumo na wala sio kanuni. Aidha, ulishikilia kuwa mifumo ya lugha ni fungo na kuwa ina majukumu ya kutekeleza katika kuibua maana za aina mbalimbali na hivyo kufanikisha amali mbalimbali. Utafiti huu vilevile ulijifunga katika misingi wa SMA kuwa umuhimu mkubwa wa lugha ni maana katika muktadha wa jamii na kuwa kwa sababu hiyo, kila lugha ina aina tatu za

vijenzi vya maana: nyenzo zinazojenga tajriba, nyenzo za kukuza mahusiano baina ya mtu na wengine, na nyenzo ya dhima za kimatini.

Kienzo kikuu kilichozingatiwa katika utafiti huu ni kile cha kimatini ambacho kinajihuhi na mpangilio wa ujumbe kwa njia yenyeye mshikamano. Utafiti huu ulijikita katika msingi uliojengeka katika kienzo hiki ili kubaini ni kwa jinsi gani vijenzi unganishi vinatumika katika matini za Kikisii ili kuleta mshikamano na ni amali gani vinatekeleza vinapotumika katika matini hizo. Kienzo amali cha kimatini kilitumika kama nguzo ya kuchunguza muundo wa ndani wa matini kwa lengo la kubaini ni viperi ambavyo vipashio mbalimbali vimeingiliana katika matini ili kufanikisha mawasiliano.

Aidha, SMA ilitumika katika kubaini iwapo maana ambayo hufasiriwa na msikilizaji ndiyo huwa imekusudiwa na msemaji au siyo. Isitoshe SMA ilitumika katika kubainisha iwapo VUM vinapotumika vinaafikisha mshikamano na muwala au la. Matini zilichunguzwa kwa kuegemea sio tu umbo na muundo bali pia maana. Hii ni kwa sababu dhana ya mshikamano hujikita sio tu katika maumbo na miundo bali pia katika maana iliyopo katika matini.

## **1.8 MBINU ZA UTAFITI**

### **1.8.1 ENEO LA UTAFITI NA WATAFITIWA**

Utafiti huu unahu su Kikisii: lugha ambayo wazungumzaji wake huitwa AbaGusii. AbaGusii ni mojawapo ya zaidi ya makabila arobaini na mawili yaliyoko nchini Kenya. AbaGusii wamo katika familia ya waBantu ambao hususan hupatikana sehemu za kusini mwa ikweta katika bara la Afrika (Ogechi 1992:71).

Nchini Kenya, makazi ya asilia ya AbaGusii ni Nyanza magharibi. AbaGusii wamepakana na kuzungukwa na waKipsigis, waMaasai na waLuo (Ogechi 1992:71). Kwa mujibu wa takwimu za 1948, AbaGusii walikuwa takriban elfu mia mbili hamsini (Whiteley 1965:1). Takwimu za 1989 zinaonyesha kuwa AbaGusii ni 1,137,054 nazo za 1999 zinaonyesha kuwa wako takriban 1,450,830. Takwimu za 2010 zinaonyesha kuwa AbaGusii ni 2,205,669. Tangu wakati huo, idadi hiyo imeongezeka na inaelekea kuwa sasa AbaGusii ni takriban watu zaidi ya milioni mbili na laki tatu.

### **1.8.2 LUGHA ILIYOTAFITIWA**

Lugha iliyofanyiwa utafiti huu ni Kikisii. Katika uainisho wa lugha uliofanywa na Guthrie (1948), Kikisii kimeainishwa E42. Lugha nyingine zinazokaribiana na Kikisii ni Logoli (E41) na Kuria (E43) ambayo ndiyo lugha inayokaribiana sana na Kikisii kimuundo. Guthrie aliainisha lugha za kiBantu kwa kuzingatia maeneo kulikozungumzwa lugha hizo. Alitumia herufi A hadi S ili kuwakilisha maeneo hayo ya kijiografia. Herufi E ilitumika katika kubainisha lugha za kibantu zilizopatikana sehemu

za Uganda kusini, kusini magharibi mwa Kenya na kaskazini magharibi mwa Tanzania. Kikisii kinapatikana sehemu ya kusini Magharibi mwa Kenya na kiliainishwa E42. Kuna tofauti ndogo sana za kilahaja katika Kikisii. Kwa mujibu wa Ogechi (2006:63) katika Akama na Maxon (2006) kuna lahaja mbili za Kikisii. Ogechi anadai kuwa lahaja hizi ni za kimaeneo: lahaja ya **maate** (ya kusini) na lahaja ya **rogoro** (kaskazini). Lahaja ya **maate** inazungumzwa na koo za AbaGusii ambazo zimepakanana na waLuo na waMasai. Koo hizi ni kama vile za *Abamachoge* na *Abagirango maate*. Hawa wanapatikana katika jimbo la Kisii. Lahaja ya **rogoro** ambayo pia hujulikana kama lahaja ya **masaba** inazungumzwa katika maeneo mengine yote ya Gusii katika majimbo ya Kisii na Nyamira.

Ogechi (2006:63) anadai kuwa tofauti kati ya lahaja hizi za Kikisii ni za kimsamiati na kifonetiki kwa mfano:

Tofauti za kimsamiati:

| Lahaja ya rogoro | lahaja ya maate | maana katika kiswahili |
|------------------|-----------------|------------------------|
| oroteru          | orogare         | uteo                   |
| etwoni           | riororo         | jogoo.                 |

Tofauti za kifonetiki:

| lahaja ya Rogoro | lahaja ya maate | maana katika kiswahili |
|------------------|-----------------|------------------------|
| tata             | dada            | baba                   |
| tama             | dama            | toroka.                |

Utafiti huu ulijikita katika kuchunguza Kikisii cha lahaja ya **Rogoro**. Hii inatokana na sababu kwamba mtafiti ni mzawa wa Kikisii anayezungumza lahaja hii; hii inaafikiana na maoni ya Vaux na Cooper (1999:93,98) kuwa ni vyema mtafiti atafitie lugha ambayo anafahamu muundo wake wa kisarufi. Aidha, asilimia kubwa ya wasailiwa wake ambaeo ni wakazi wa eneo la Kegati ni wazungumzaji asilia wa lahaja hii ya **Rogoro**.

### **1.8.3 SAMPULI**

Ili kuhakikisha kuwa data za kihalisia na kiasilia zimepatikana, mtafiti aliteua sampuli kimakusudi. Aliteua miktadha ya mahusiano ya kawaida mionganini mwa wanajamii. Vilevile mtafiti aliteua muktadha wa shulenii. Mtafiti alikusanya data zake kutoka kwa watu wa umri kati ya miaka kumi na miwili na hamsini. Hii ni kwa sababu watu kati ya umri huu wanaelekea kuwa na viwango vifaavyo vyaa umilisi wa lugha.

Mtafiti aliteua sampuli kutoka kwa watu anaoingiliana nao hasa nyakati za jioni anapokuwa ametoka kazini. Yeye hupiga gumzo na watu hawa kuhusu maswala mbalimbali ya mahusiano ya kijamii na ya kisiasa. Kwa sababu hiyo ilikuwa rahisi yeye kuwashirikisha watu hawa katika majadiliano na kupata data. Aghalabu, mtafiti hushiriki gumzo na vikundi vyaa vijana wa kati ya umri wa miaka ishirini na miaka thelathini na tano na vilevile wazee wa umri kati ya miaka arobaini na hamsini. Mtafiti alikusanya data kutoka kwa vijana na vilevile kutoka kwa wazee hao katika nyakati tofauti tofauti.

Katika muktadha wa shulenii, mtafiti alichagua sampuli ya wanafunzi walio na umri wa kati ya miaka kumi na miwili na kumi na mitano. Alipata wanafunzi hawa katika shule ya msingi ya Kegati hasa kutoka katika darasa la sita na darasa la saba. Wanafunzi wa madarasa ya tano kuelekea chini hawana umakinifu mkubwa na wana mzaha mwingi ilhali wale wa darasa la nane wanafungika zaidi kimasomo hasa kwa kuwa wanajitayarisha kufanya mitihani ya kitaifa.

Mtafiti alikusanya jumla ya hadithi kumi zilizohadithiwa na wanafunzi wa shule ya msingi ya Kegati. Aidha, kutoka kwa sampuli aliyoingiliana nayo katika muktadha wa mazungumzo ya kawaida, mtafiti alinasa jumla ya mazungumzo binafsi ishirini na manne. Hadithi zilizoteuliwa kwa uchanganuzi zilikuwa ni tano ilhali mazungumzo binafsi kumi na mawili yaliteuliwa kama sampuli ya kufanya uchanganuzi. Hadithi na mazungumzo binafsi yaliyoteuliwa katika utafiti huu ni yale yaliyobainika kuwa na mtiririko.

#### **1.8.4 VIFAA**

Mtafiti alitumia kinasa sauti ili kuweza kunasa sauti za sampuli aliyoteua. Alinasa sauti za AbaGusii walipokuwa wakishiriki mazungumzo kuhusu mada tofauti tofauti. Pia alinasa sauti za wanafunzi walipokuwa wakihadithia visa mbalimbali. Huku akirejelea kanda zilizokuwa zimenasa sauti, mtafiti alitumia kalamu na daftari ili kunakili tungo kutoka kwa matini semwa ambazo zilidhihirika kuwa na VUM .

### 1.8.5 MBINU ZA UKUSANYAJI WA DATA

Ili kupata matini mahususi zinazofaa kwa uchanganuzi, mtafiti alitumia mbinu ya kunasa sauti za wazungumzaji AbaGusii walipokuwa katika mazungumzo kuhusu mada mbalimbali. Wasailiwa alioteua mtafiti ni watu ambao ana maingiliano ya karibu nao pamoja na wanafunzi wa shule ya msingi. Mtafiti aliunganika na wasailiwa hawa mbalimbali katika mazungumzo mbalimbali. Alipojiingiza katika mazungumzo na wasailiwa, mtafiti alichangia mada kwa kiasi kidogo huku akiwapa wasailiwa muda mwangi wa kuzungumza. Huku akitumia kinasa sauti alichokuwa amekificha mfukoni, mtafiti alirekodi mazungumzo hayo kwa siri na baadaye akawafahamisha wasailiwa hao kuhusu kurekodi kwake. Baadaye aliwaomba wasailiwa kumpa ruhusa ya kutumia data alizopata. Hatimaye alinakili mazungumzo yaliyobainika kuwa mazungumzo binafsi. Haya yalijitokeza pale ambapo mhusika mmoja angezungumza kwa muda mrefu kuhusu suala fulani kabla ya kuwapa wenzake nafasi ya kuchangia mada husika

Vilevile data zilikusanywa kutoka kwa watoto kati ya miaka kumi na miwili na kumi na mitano. Hawa walipatikana katika shule ya msingi hasa katika darasa la sita na saba; Alikusanya data kutoka shule ya msingi ya Kegati. Mtafiti aliomba idhini ya kunasa sauti za wanafunzi kutoka kwa wasimamizi hasa mwalimu mkuu na walimu wengine waliohusika. Mtafiti aliwaeleza wasimamizi hao kuhusu malengo yake ya utafiti na nia yake ya kunasa sauti za wasailiwa. Baada ya kupewa idhini, mtafiti aliwaomba wanafunzi wakiwa darasani kusimulia hadithi tofauti tofauti. Walipokuwa wamejikita katika shughuli hizi za usimulizi, mtafiti alirekodi kwa siri masimulizi yao. Baadaye mtafiti

aliwafichulia wanafunzi hao kuwa alikuwa amenasa sauti zao; aliwaomba idhini ya kutumia data hizo.

Njia hii ya ukusanyaji data inakwenda sambamba na madai ya Vaux na Cooper (1999:110) wanaodai kuwa kuwaomba wasailiya kusimulia visa na matukio mbalimbali huku mtafiti akinasa sauti zao na kuzichanganua baadaye ni njia mwafaka na rahisi ya kukusanya data kutoka kwa wasailiya bila ya kuwachosha wala kuwakinaisha.

Kwa kuzingatia maoni ya Vaux na Cooper (1999:110) kuwa ni vyema kuthibitisha data zilizokusanywa kwa msaada wa wasailiya wenyewe, mtafiti aliteua wathibitishajiji data wanne ambao ni wazunguzaji wazawa wa Kikisii. Wathibitishajiji data hawa walihitajika kuwa na umri kati ya miaka ishirini na ishirini na sita. Wathibitishajiji data hawa ni wanafunzi waliteuliwa kutoka chuo kikuu cha Kisii ambako mtafiti ni mhadhiri. Chuo hiki kina asilimia kubwa ya wanafunzi wazawa wa lugha ya Kikisii. Mtafiti aliteua wanafunzi ambao wanasomea maswala ya lugha ya kiswahili katika kitivo cha elimu. Aliamini kuwa ingekuwa rahisi kwa wanafunzi hawa kuyaelewa maswala mbalimbali ya lugha na hivyo kuzithibitisha data kwa urahisi. Wanafunzi walioteuliwa ni wale waliokuwa katika miaka ya pili, tatu na nne. Ilichukuliwa kuwa wanafunzi wa mwaka wa kwanza walikuwa hawajapata weledi wa kutosha hasa kuhusu maswala ya isimu. Mmoja aliteuliwa kutoka mwaka wa pili, mmoja kutoka mwaka wa tatu na wawili kutoka mwaka wa nne. Wote hawa walitakiwa kuwa na uwezo wa kusoma na kuandika lugha za Kikisii, Kiswahili na Kiingereza bila ya matatizo yoyote. Umri wa wathibitishajiji data (kati ya miaka ishirini na miaka ishirini na miwili) uliteuliwa kimakusudi kwa kuwa mtafiti

aliamini kuwa katika umri huu wasailiwa wana uwezo wa kufuata maagizo bila ya kukanganyikiwa au kupuuza.

Mtafiti aliwaeleza wathibitishaji data hawa kuwa alikuwa akitafuta tungo za Kikisii ambazo zinaonekana kuwa moja lakini zinazotoa jumbe mbili au zaidi. Tungo hizi huwa na VUM ambavyo kando na kuunganisha, pia huwa na amali nyingine anuwai. Aliwapa mifano ya tungo hizo katika Kikisii na baada ya kubaini kuwa wameelewa kile alichokuwa anatafuta katika tungo hizo, mtafiti aliwapa wathibitishaji nakala za matini alizokuwa amekusanya na kuwaomba wazisome na kuziwekea alama tungo za Kikisii ambazo ni halisi. Aidha, aliwashirikisha katika kubaini iwapo kweli tungo hizo zinatoa jumbe zaidi ya mmoja. Kila mthibitishaji data alitakiwa kuthibitisha data alizopewa bila ya kuathiriwa na mthibitishaji mwenzake; hawakutakiwa kushirikiana au kushauriana kuhusu data hizi kwa vyovyote.

Tungo zilizothibitishwa na wathibitishaji wote wanne kuwa tungo halisi za Kikisii na ambazo zina jumbe zaidi ya mmoja ndizo zilizotumiwa na mtafiti katika uchanganuzi wake. Mtafiti alitumia ujuzi wake wa kiisimu kubaini ni maana gani inayojitokeza kutokana na matumizi ya VUM vilivyobainika katika sentensi zilizokuwa zimefanyiwa uthibitishaji. Kutokana na uchambuzi na uchanganuzi uliofanyiwa tungo zilizokuwa zimethibitishwa, mtafiti aliweza kutambua amali mbalimbali zilizotokeza kutokana na matumizi ya VUM mbalimbali vilivytumika katika sentensi hizo zilizo na jumbe zaidi ya mmoja.

### 1.8.6 UCHANGANUZI WA DATA

Mtafiti alitumia ujuzi wake wa Sintaksia na uchanganuzi matini katika kuainisha tungo mbalimbali zilizo na VUM zilizojitokeza katika matini semwa za Kikisii. Aidha, alitumia ujuzi wake wa Mofolojia, Sintaksia na Semantiki pamoja na nadharia ya SMA, katika kutambua na kubainisha vijenzi vya kiisimu vilivyo na dhima ya ‘uunganishaji’ kama vilivyojidhihirisha katika matini mbalimbali. Vijenzi vilivyopewa uzito aghalabu ni vile vilivyojitokeza kuwa na dhima ya kufanikisha mshikamano katika matini. Mtafiti alitumia ujuzi wake wa Mofolojia katika kuchanganua maumbo na alomofu za VUM vilivyojitokeza katika matini semwa za Kikisii. Ujuzi wa mtafiti kuhusu SMA ulimwezesha mtafiti kubainisha amali mbalimbali zilizopatikana kutokana na matumizi ya VUM katika tungo mbalimbali zilizojitokeza katika matini semwa za Kikisii.

Mtafiti aliteua tungo kutoka kwa matini alizokuwa amenasa kutoka kwa wasailiwa. Aliteua tungo zilizodhihirisha kuwa na vijenzi vya mshikamano. Mtafiti aliongozwa na dhana ya kipashio kiini (F – unit). Dhana hii imezuliwa kutoka kwa Lieber (1981:93:96). Lieber alichukulia kuwa kipashio kiini kinahusisha vishazi pamoja na baadhi ya vijalizo ambavyo vinatekeleza dhima sawa na vishazi. Kwa mujibu wa Lieber, Kipashio kiini kinaweza kuchukuliwa kuwa:

- a) Sentensi ambatano ambazo zina vishazi viwili vyenye dhima sawa na ambavyo vimeunganishwa kwa viunganishi ambatishi:

Nigo akana/ *na gosoka isiko*  
 Nigo a-kan-a/ *na go-sok-a isiko*  
 KIM NFS3U-MZZ-IT/ KUM Kat-MZZ-IT E  
 (Alikanusha/ *na kutoka nje*)

- b) Sentensi ambatano zinazodhihirisha mtendaji katika kishazi cha pili akiwa ni tofauti na wa kishazi cha kwanza:

Omwarimu nigo abwatete ekaramu, / *na omongina ekeranya*  
 O-mw-arimu nigo a-bwat-et-e e-karamu, / *na o-mo-ngina e-ke-ranya*  
 KAT-NGL-MZZ KIM NGL-MZZ-MAT-IT NGL-MZZ/ KUM KAT-IDU-MZZ KAT-IDU-MZZ  
 (Mwalimu alichukua kalamu/ *na mama kiboko*)

- c) Sentensi ambazo zina miundo unganifu ya vitenzi:

Nigo ambwatete okoboko, / *na gontamboki orache*  
 Nigo a-m-bwat-et-e o-ko-boko, / *na go-n-tambok-i o-roche*  
 KIM NFS3U-SH-MZZ-MAT-IT NGL-IDU-MZZ/ KUM Kat-SH-MZZ-ITKAN IDU-MZZ  
 (Alinishika mkono/ *na kunivusha mto*)

- d) Vishazi ambavyo vimeunganishiwa vitegemezi ambavyo havina kitenzi:

Kera omonto natambogete, / *otatiga Moraa*  
 Kera o-mo-nto ni-a-tambok-et-e, / *otatiga Moraa*  
 V NGL:IDU-MZZ KIM-NFS3U-MZZ-MAT-IT/KUM N  
 (Kila mtu alivuka/ *isipokuwa moraa*)

Kipashio kiini kilibainika kumiliki KUM na alama ya msharazi (/) ilitumika ili kutambulisha vipashio kiini na kubainisha ni wapi VUM vilipotumika. VUM vilivyojiteza katika vipashio kiini mbalimbali ndivyo vilivyochanganiuliwa na mtafiti kwa lengo la kubaini umbo, muundo pamoja na amali zake.

Data zilizopatikana katika utafiti huu zilipimwa kwa utokeaji, ulinganishaji, kukadiria au wastani na asilimia. Kila kijenzi kiliwekwa kwenye jedwali ili kuonyesha ni mara ngapi kimetumika katika tungo zilizoteuliwa. Hali hii iliwezesha kutambua ni VUM vipi ambavyo vinatumika mara nyingi na vipi ambavyo vinatumika mara chache. Katika utafiti huu tulipima kitakwimu VUM vinavyojiteza katika matini semwa za Kikisii. Aidha kutokana na data tulizopata kutokana na utafiti huu tuliweza kupambanua maumbo

na miundo mbalimbali ya VUM pamoja na kuchanganua amali mbalimbali zinazotekelawa na VUM hivyo. Muhtasari wa data tulizokusanya katika utafiti huu unaonyeshwa katika 1.8.7 hapa chini.

### **1.8.7 MUHTASARI WA DATA**

Katika sehemu hii mtafiti ametoa muhtasari wa data alizokusanya kutoka kwa wasailiwa wake. Ametoa jedwali linaloonyesha VUM alivyopata kulingana na utokeaji wake kiasilimia. Tungo zilizobainishwa katika majedwali haya zinatokana na matini zilizoteuliwa kama sampuli katika utafiti huu ambazo zilikuwa ni hadithi tano pamoja na mazungumzo binafsi kumi na mawili. Katika jedwali la kwanza kunabainishwa idadi ya viunganishi vilivyojitokeza katika tungo hizo ilhali katika jedwali la pili kumebainishwa idadi ya vipatanishi vya kileksimu vilivyopatikana katika tungo zilizochanganuliwa.

#### **1.8.7.1 JEDWALI LINALOONYESHA VIUNGANISHI**

| Aina ya U                                 | Idadi ya aina ya U | Idadi ya tungo zenye U | Asilimia ya kurudiwa kwa U |
|---|--------------------|------------------------|----------------------------|
| Vipanuzi (mrejeosawa, kwa kutumia mifano) | 22                 | 194                    | 11.34                      |
| Urekebishaji                              | 9                  | 194                    | 4.64                       |
| Yenye kuvuta mawazo                       | 6                  | 194                    | 3.09                       |
| Yenye kutoa fikirani                      | 1                  | 194                    | 0.52                       |
| Yenye kuonyesha umahususi                 | 4                  | 194                    | 2.06                       |
| Yenye kuendeleza                          | 8                  | 194                    | 4.12                       |
| Yenye kufupisha                           | 2                  | 194                    | 1.03                       |
| Yenye kuthibitisha                        | 3                  | 194                    | 1.55                       |

|                                   |     |     |       |
|-----------------------------------|-----|-----|-------|
| Vya kupanua; kuongeza chanya/ asi | 15  | 194 | 7.73  |
| Yenye kuteka mawazo               | 12  | 194 | 6.19  |
| Uzidishaji                        | 7   | 194 | 3.61  |
| Vya sababu                        | 19  | 194 | 9.79  |
| Vya mfuatano wa kimantiki         | 10  | 194 | 5.15  |
| Vinavyoashiria mahali             | 5   | 194 | 2.58  |
| Vya kuonyesha matokeo             | 1   | 194 | 0.52  |
| Vya muda                          | 34  | 194 | 17.53 |
| Kuonyesha wasiwasi                | 16  | 194 | 8.25  |
| Visivyo vipinganifu               | 11  | 194 | 5.67  |
| Vipinzani                         | 2   | 194 | 1.03  |
| Vipinganifu                       | 4   | 194 | 2.06  |
| Vya mfuatano kimantiki            | 3   | 194 | 1.55  |
| JUMLA                             | 194 |     |       |

### 1.8.7.2 JEDWALI LINALOONYESHA VIPATANISHI VYA KILEKSIMU

| Aina ya LP                              | Idadi ya aina ya LP | Idadi ya tungo zenye LP | Asilimia ya kurudiwa kwa LP |
|---|---------------------|-------------------------|-----------------------------|
| Uwakislishaji: nomino, vitenzi, kishazi | 13                  | 72                      | 18.06                       |
| Udondoshaji: nomino, vitenzi, kishazi   | 31                  | 72                      | 43.06                       |
| Urudiaji                                | 16                  | 72                      | 22.22                       |
| Visawe unganishi                        | 9                   | 72                      | 12.50                       |
| Jina la jumla                           | 3                   | 72                      | 4.17                        |
| JUMLA                                   | 72                  |                         |                             |

Kutokana na data zilizoratibiwa katika majedwali haya ilidhihirika kuwa viunganishi katika matini semwa za Kikisii vilikuwa ni vingi ikilinganishwa na vipatanishi vya kileksimu. Aidha, majedwali haya yanaashiria kuwa viunganishi vyenye dhima ya kuashiria muda ndivyo vinavyotokea kwa wingi katika matini semwa za Kikisii ilhali vile vya kutoa fikirani na kuonyesha matokeo vikitokeza kwa uchache mno. Jedwali la pili linadhihirisha kuwa vipatanishi vya kileksimu ambavyo ni vya udondoshaji vinajitokeza kwa asilimia kubwa katika matini semwa za Kikisii ilhali vipatashi vya kileksimu vinavyoonyesha jina la jumla vikitokeza kwa asilimia ndogo zaidi.

### 1.8.8 Hitimisho

Sura hii imeweka wazi usuli wa suala la utafiti huu, inaliweka wazi suala la utafiti, madhumuni ya utafiti na upeo wa utafiti. Aidha, imebainisha umuhimu wa kufanya utafiti huu. Vilevile imeweka wazi misingi ya nadharia ya SMA na kuonyesha ni vipi nadharia hii ilivyotumika katika utafiti huu. Isitoshe sura hii imeweka wazi mbinu za utafiti zilizotumika katika utafiti huu. Inabainisha eneo la utafiti na watafitiwa, lugha iliyotafitiwa na namna sampuli ilivyoteuliwa. Aidha, imebainisha vifaa vilivyotumika katika kukusanya data, pamoja na mbinu zilizotumika katika ukusanyaji data. Isitoshe, sehemu hii inaonyesha jinsi data zilizokusanywa zilivyochanganuliwa. Katika sehemu ya mwisho ya sura hii, kumesawiriwa muhtasari wa data zilizokusanywa; data hizi ziliratibiwa kiasilimia kulingana na utokeaji wake. Ilibainika kuwa VUM viunganishi vilitokeza kwa wingi katika matini semwa za Kikisii ikilinganishwa na VUM leksimu patanishi. Aidha sehemu hii ilibainisha kuwa VUM viunganishi vya kuonyesha muda vilitokeza kwa asilimia kubwa kuliko VUM vile vingine unganishi. Aidha, VUM leksimu patanishi vya udondoshaji navyo vilitokeza kwa asilimia kubawa ikilinganisha na vile vingine.

## SURA YA PILI

### **DHANA YA MSHIKAMANO NA YALIYOANDIKWA KUHUSU MADA**

#### **2.0 Utangulizi**

Sura hii inapambanua dhana ya mshikamano kwa jumla. Vilevile inahakiki kazi mbalimbali kuhusu mshikamano na muwala hasa zile zilizoegemea katika kuchunguza vijenzi unganishi vilivyo na dhima ya mshikamano. Kazi anuwai kuhusu mshikamano zimehakikiwa katika sura hii ili kudhihirisha jinsi zilivyochangia utafiti huu na pia kubaini ni kwa namna gani utafiti huu umechangia katika kuyaziba baadhi ya mapengo yaliyoachwa katika kazi hizo.

#### **2.1 Dhana ya mshikamano**

Halliday na Hassan (1976) wanadai kwamba dhana ya mshikamano ni ya kisemantiki na hurejelea uhusiano wa maana ndani ya matini fulani na kwamba mshikamano hutokea pale ambapo ufanuzi wa elementi moja katika matini hutegemea ile nyingine. Dhana hii hujishughulisha na kipengele cha matini kinachobeba maana katika lugha. Matini huweza kuwa neno moja au sentensi moja au msururu wa sentensi, na sentensi hizi ziwe zimeunganishwa kimaana kwa utaalamu ili kuwasilisha wazo lilokamili. Utafiti huu unachukulia matini kuwa tungo zilizo na mtiririko na ambazo hupitisha habari iliyo na maana. Kwa mujibu wa Halliday na Hassan (1976:6) kuna mshikamano ndani ya sentensi ambapo vipengele mbalimbali vinavyoiunda sentensi vinashirikiana kwa ukubalifu ili kuunda sentensi inayokubalika kisarufi. Kuna mshikamano baina ya sentensi na sentensi, ambapo kiungo cha mshikamano huundwa na faridi mbili kila moja ikiwa

katika sentensi tofauti. Faridi hizi huunganisha sentensi kisemantiki. Aidha, kuna mshikamano baina ya kirai na kirai, kishazi na kishazi. Halliday na Hassan (1976) wanashikilia kuwa mshikamano katika mkururo wa sentensi hujitokeza wazi kwa sababu ndio asili pekee ya muwala.

Hatch (1992) anajadili mshikamano katika matini; anadai kuwa mshikamano katika matini unaweza kuafikiwa kwa njia mbalimbali. Kwa mfano, kwa kutumia violezo kutoka kwa makala na maumbo ya kiusemi, kwa uteuzi wa vishazi maalumu na kwa vibainishi nya kisintaksia. Anadai kuwa vijenzi nya mshikamano pia vinaweza kutumika katika kuunganisha vipande mbalimbali nya matini kwa njia maalumu. Anatambua vijenzi hivi nya mshikamano kuwa ni urejeshaji, uwakilishaji, udondoshaji, viunganishi na vipatanishi nya kileksia.

### **2.1.1 Urejeshaji**

Hatch (1992) anaeleza kuwa aghalabu viwakilishi hutumika katika kuashiria nomino husika. Katika Kiingereza kwa mfano, kiwakilishi ‘she’ kinaweza kutumika badala ya nomino ‘Mary’. Kiwakilishi hiki ni kijenzi cha mshikamano kinachoashiria nomino. Kwa mfano:

Mary is a good student. *She* likes working hard.

(Mary ni mwanafunzi mzuri. Anapenda kufanya bidii).

Katika Kiswahili hakujadhihirika kipashio kilicho sawa na ‘she’ hii ni kwa sababu Kiswahili ni lugha ambata na hivyo neno ‘she’ limewakilishwa na kiambishi ‘a-‘ kinachodhihirisha NFS3U. Urejeshaji katika Kiswahili hudhihirika kupitia kwa matumizi ya viwakilishi nafsi, vimilikishi, vivumishi vimilikishi, viashiria (vikitumika kama viwakilishi au vivumishi) na vielezi na vivumishi vya ulinganifu (Munyua, 1994).

Hatch (1992) anafafanua kuwa katika Kiingereza viwakilishi nafsi, viashiria na vilinganishi hutumika kuleta mshikamano. Viashiria katika Kiingereza huweza kurejesha nyuma na vilevile mbele (Hatch, 1992; Halliday na Hassan, 1976; Brown na Yule, 1983) mathalani:

1. “If the buyer wants to know what is covered by the guarantee, **he** has to read the fine print and consult a lawyer.”  
(Ikiwa mnunuzi anataka kujua kinachoghamiwa na dhamana, anatakiwa asome yaliyoandikwa au atafute ushauri wa mwanasheria)
2. “John asked **him** to sing and so Bill sang.”  
(John alimtaka aimbe na hivyo Bill aliimba)

Katika mfano wa kwanza, uashiariaji unaturudisha nyuma kutokana na matumizi ya ‘he’ (mnunuzi) ilhali katika mfano wa pili urejeshaji unatupeleka mbele kutokana na matumizi ya ‘him’ (Bill).

Barongo (1996) anapambanua kuwa urejeshaji ni uhusiano wa kisemantiki baina ya sehemu mbalimbali zinazoiunda matini ambapo maumbo fulani ya lugha hutumiwa kurejelea faridi fulani za kiisimu ambazo ama hutokea mwanzoni mwa matini au baadaye. Anadai kuwa maumbo haya hayawezi kutafsiriwa bila ya kurejelewa katika faridi hizi. Halliday na Hassan (1976:37) wanadai kuwa ulinganishi ni urejeshaji usiokuwa wa moja kwa moja kwa njia ya utambuzi au ufanano. Toolman (1998) naye anaeleza kuwa ulinganishi unapotumika kama mbinu ya mshikamano huleta maana tu iwapo pana mfananisho wa vitu viwili hivi kwamba kitu kimoja kinalinganishwa na kingine. Ulinganisho huu huweza kufanywa kwa kutumia dhana kama vile; *sawa, kama, tofauti na kuliko* na kadhalika. Salkie (1995) anapambanua kuwa ikiwa vitu viwili au zaidi vinalinganishwa katika matini, itachangia pakubwa mshikamano. Hii inadhihirisha kuwa ulinganishi ni njia mojawapo ya kuleta mshikamano katika matini.

### **2.1.2 Uwakilishaji**

Kuhusu uwakilishaji, Hatch (1992) anadai kuwa kinacholengwa hapa sio kigezo maalumu bali ni kundi la vigezo. Kwa mfano:

“Did you find the blankets? Only the blue **ones**”

(“Ulipata blanketi? Zile samawati pekee”)

Neno ‘**ones**’ linaashiria blanketi. Uwakilishaji pia unaweza kuundwa kwa nomino, vikundi tenzi, na vishazi kwa mfano:

#### **Nomino**

‘Do you want the blankets? Yes I’ll take **one**’  
 (Unataka blanketi? Ndio nitachukua *moja*)

### Vitenzi

‘Did you sing? Yes, **I did**’  
 (‘Uliimba? Ndio, *nifanya*’)

### Kishazi

‘The blankets needed to be cleaned. **Yes they did**’  
 (‘Blanketi zilihitaji kuoshwa. *Ndio zilihitaji*’)

#### **2.1.3 Udondoshaji**

Hapa kijenzi cha mshikamano hakitajwi waziwazi. Kwa mfano:

“Would you like to hear another verse? **I do**”  
 (Ungependa kusikia fungu lingine? *Ningependa*)

Neno ‘verse’ halijatajwa katika sehemu ya pili ya utungo huu; limedondoshwa kwa njia inayowezesha mshikamano.

Halliday na Hassan (1976:142) wanadai kwamba udondoshaji ni ile hali ya ‘kuacha kitu nje’ kitu hicho huweza kuwa kipashio cha kisarufi katika sentensi. Udondoshaji huu hufanywa ili kuondoa urudufishaji katika matini na vilevile kuwezesha mshikamano katika matini husika. Wanaendelea kueleza kuwa kinachoachwa nje si kuwa hakieleweki, bali kinaeleweka. Kinaeleweka kwa sababu huwa kinadhaniwa kutoka kwa sentensi iliyotangulia katika matini. Kipashio kinachoachwa huacha pengo maalumu la kimuundo ambalo hujazwa kwa kurejelea kipashio hicho kidhana tu. Maoni haya pia yanashikiliwa na Hatch (1992:225). Halliday (1985) naye anashikilia kuwa sehemu ya kishazi au sehemu ya kitenzi au kikundi nomino kinawenza kudhaniwa katika sehemu ya mbele katika matini kwa njia ya kukidondo na hivyo kusababisha udondoshaji. Anadai kuwa hii ni njia moja ya kufanikisha mshikamano katika matini.

Kwa mujibu wa Beaugrande na Dressler (1981) udondoshaji ni kurudia umbo fulani na viungo lakini kuacha nje baadhi ya vielelezo vyake. Hii ina maana kuwa neno linaweza kurudiwa katika sentensi inayofuatia nyingine lakini visifa au vifuasi nya neno hilo visitajwe kwa mara ya pili bali virejelewe kidhana tu. Udondoshaji hutokea katika sentensi inayofuata nyingine huku ikiacha kipashio au vipashio fulani vilivyotangulia kutajwa katika sentensi iliyotangulia. Madai haya pia yanashikiliwa na Crystal (1997) na vilevile Matthews (1981). Verma na Krishnaswamy (1994:245) hata hivyo wanatahadharisha kuwa mtu hawezi kufanya udondoshaji kiholela. Wanadai kuwa baadhi ya elementi haziwezi kudondoshwa; mwandishi au msemaji hawezi tu kudondosha anavyotaka kwa sababu kwa kufanya hivyo anaweza kupotosha maana au hata mshikamano wa matini.

Crystal (1997:119) anafafanua kuwa udondoshaji ni wakati kijishemu fulani cha muundo kinaachwa nje na kinaweza kupatikana tena kutoka kwa usemi uliotangulia. Maoni haya pia yanashikiliwa na Matthews (1981:38) ambaye anadai kuwa udondoshaji ni pale ambapo maneno au elementi fulani zimeachwa nje katika matini na huweza kurejelewa. Kulingana na Matthews, udondoshaji huenda sambamba na muktadha na kwamba mtu huweza kurejelea sentensi tangulizi ili kupata kile kilichodondolewa. Brown na Yule (1983) wanaeleza kwamba udondoshaji huweza kutokea pale ambapo kipashio fulani kilichotajwa awali katika sentensi tangulizi kinaachwa nje katika sentensi inayofuata. Hii ina maana kwamba kipashio hicho hakitajwi tena na ili kupata maana inabidi kipashio hicho kirejelewe kidhana tu kuziba pengo hilo.

Verma na Krishnaswamy (1994:245) wanaeleza kuwa udondoshaji unapaswa kufanywa kwa makini kwa sababu kuna vipashio vinavyoweza kudondoshwa na kuna vile visivyoweza kudondoshwa. Wanafafanua kuwa udondoshaji ukifanyika kiholela maana ya matini huweza kupotoka na mshikamano ukapotea.

Thompson (2004:184) akijadili udondoshaji anaeleza kuwa ni wakati kuna pengo lililoachwa na kujazwa na elementi zinazorejelewa kutoka kwa habari tangulizi. Anaendelea kudai kuwa udondoshaji hujitokeza zaidi katika usemi halisi kuliko katika maandishi, palipo na majibu “ndiyo” au “la”. Majibu haya hudhania maneno kutoka kwa taarifa tangulizi.

Hatch (1992) anatambulisha aina zifuatazo za udondoshaji:

#### Udondoshaji wa nomino

‘They’re small; take two (cookies)’

{Ni ndogo; chukua mbili (biskuti)}

#### Udondoshaji wa vitenzi

‘Were you typing? No I wasn’t (typing)’

{Ulikuwa ukipiga chapa? Hapana sikuwa (nikipiga chapa)}

#### Udondoshaji wa kishazi

‘I don’t know how to work this computer. I’ll have to learn how (to work the computer)

{Sijui jinsi ya kutumia tarakilishi hii. Itabidi nijifunze (jinsi ya kutumia tarakilishi)}

### Udondoshaji wa viunganishi

‘I was not invited. **Otherwise**, I would have been there.

(Sikualikwa. *Vinginevyo*, ningekuwepo)

Katika mfano: ‘*I was not invited. Otherwise, I would have been there*’ (Sikualikwa. *Vinginevyo*, ningekuwepo), Vishazi hivi viwili (sikualikwa na ningekuwepo) vimeunganishwa/ vimewekwa pamoja kwa kutumia KUM - vinginevyo (otherwise); KUM hiki kinatusaidia katika kufasiri uhusiano baina ya vishazi hivi; mhusika hakuenda na sababu ya kutoenda kwake ni kuwa hakualikwa. Neno ‘*otherwise*’ katika mfano huu linawezesha mshikamano katika tungo hii kwa kuziba pengo ambalo limeachwa kutokana na kudondoshwa kwa ‘*had I been invited*’ (ningekwa nimealikwa)

Hatch (1992:225) anadai kuwa kuna aina mbalimbali za viunganishi:

### Vya kuongeza:

‘She worked on the computer the whole day without stopping. *And as she worked, she thought about the problem.*’

(Alifanya kazi kwenye tarakilishi mchana mzima bila ya kupumzika. *Na alivyofanya kazi alilifikiria tatizo hilo*)

### Vya kuteka mawazo:

‘She was hardly conscious of her attempts to solve the problem. *Yet, by evening the solution magically appeared.*’

(Hakuwa na nadhari ya juhudhi zake za kutatua tatizo hilo. *Ingawa, ilipofika jioni suluhisho lilitokeza kimujiza*)

Vya sababu:

‘Her work was finished, so she turned off the computer.’

(Kazi yake iliisha, *kwa hivyo alizima tarakilishi.*)

Vya muda:

‘Then as the five o’clock bell rang, she hurried out of the office building.’

(*Halafu kengele ya saa kumi na moja ilipokiriza, alitoka nje ya jengo la ofisi upesi*)

Kwa mujibu wa Hatch, tunaweza kutumia leksimu mbalimbali kama vijenzi vya mshikamano kwa kutegemea diskosi tunayojenga. Hii hujitokeza wazi kutegemea na chaguzi zetu za vijenzi unganishi.

Toolman (1998:28-29) anafafanua kuwa matumizi ya kiunganishi hufanya uunganishi kuwa wazi zaidi. Anaeleza kuwa mshikamano unganishi hurejelea matumizi ya baadhi ya maneno na virai. kwa kawaida maneno haya huwa mwanzoni mwa sentensi, kwa madhumuni ya kufafanua uhusiano wa kisemantiki kati ya habari ifuatayo ile tangulizi. Uunganishi huu unaweza kuwa fiche kati ya elementi iliyotangulia na inayofuata. Anaendelea kueleza kuwa matumizi ya kiunganishi hufanya uunganishi kuwa wazi zaidi na kuwa viunganishi vya mshikamano vina uamilifu kisemantiki.

Thompson (2004:19) anaeleza kuwa uunganishi hurejelea uchanganyaji wa elementi zozote za kimundo mbili katika kipashio changamano cha kisemantiki katika mshikamano. Elementi hizi huweza kuwa na miundo mbalimbali na si lazima iwe miundo yao inafanana. Kwa mfano kishazi tegemezi kuunganishwa na kishazi kikuu au

sentensi sahili, kirai kitensi kuunganishwa na sentensi sahili, nomino kuunganishwa na kirai husishi. Uunganishi huu unapotokea huleta mshikamano katika matini husika.

Kwa mujibu wa Quirk na Greenbaum (2000:253) uunganishi hutokea ama kwa kutumia viunganishi au kwa kutotumia viunganishi lakini viunganishi hivyo vikarejelewa kwa muktadha wa dhana. Wanapambanua kuwa uunganishi hujumuisha uunganishi wa vipashio vyta kisintaksia na pia maana. Wanatoa mifano ya viunganishi kama *and, or, but, so, furthermore, finally, as a result of, however, besides, still, of course* na kadhalika. Aidha, wanaeleza aina mbalimbali za uunganishi kama vile elezi, nyongeza, sababishi, kubalifu na kadhalika.

O'grady na wenzake (1996) wanaeleza kwamba viunganishi hutumika kuunganisha elementi au kategoria za kisintaksia mbili au zaidi. Wanapambanua kuwa viunganishi vyta nomino vinaweza kudondoshwa isipokuwa kile kinachotokea mara tu kabla ya nomino ya mwisho. Kutokana na maelezo haya, inabainika kuwa iwapo kuna viunganishi vinavyounganisha nomino kadhaa zinazofuatana, viunganishi vinavyotokea awali vinaweza kudondoshwa lakini kile cha mwisho kikasalia. Hata viunganishi hivi vinapodondoshwa, mshikamano bado huwepo katika matini. Hali hii haitoeki tu katika nomino pekee bali huweza pia kutokea katika vitenzi. Viunganishi vinaweza kudondoshwa isipokuwa kile cha kabla ya kitensi cha mwisho.

Van Dijk (1976) alishughulikia uunganishi katika semi za Kiingereza. Alionyesha matumizi ya viunganishi mfano '*but yet*' '*but nevertheless*' '*because although*' na vikwazo

na athari zake katika usemi. Van Dijk alieleza kuwa katika Kiingereza, kuna matumizi yasiyokubalika. Kwa mfano: '*but although*'

Winter (1971) naye kwa upande wake anabainisha aina zifuatazo za vijenzi unganishi katika Kiingereza:

- a) Vya mfuatano wa kimantiki: 'thus', 'therefore', 'then', 'thence', 'consequently', 'so'
- b) Vipinzani: 'however', 'infact', 'conversely'.
- c) Vya kuonyesha wasiwasi: 'probably', 'possibly', 'indubitably'
- d) Visivyo pinganifu: 'moreover', 'likewise', 'similarly'
- e) Vipanuzi: 'for example', 'in particular'.

Halliday na Hassan (1976) wanaeleza kuwa uunganishi huhusisha elementi za kiisimu zinazotokea katika mfululizo na hazina uhusiano wa kumuundo. Uhusiano katika elementi hizi huletwa na viunganishi. Uunganishi huu huwa ni uhusiano wa kisemantiki wenye uamilifu wa mshikamano. Viunganishi hutokea katika sentensi moja ikiwa kiunganishi kinaunganisha dhana inayotokea katika kishazi tangulizi na kile kinachoifuata. Mfuatilizo wa wakati katika sentensi moja au mbili huwa kipengele cha mshikamano kwa sababu ya uhusiano wa kisemantiki unaouanganisha dhana mbili. Mfuatilizo huu huweza kuonyeshwa kwa kielezi. Hivyo kielezi kinakuwa kiunganishi.

Quirk na Greenbaum (2000) wanapambanua kuwa kuna viunganishi vyta kategoria za kileksia na kisemantiki. Viunganishi vyta kategoria za kileksia ni vile ambavyo huunganisha sentensi katika daraja moja na kuunganisha sentensi katika daraja tofauti. Uunganishi huu hujikita katika muundo wa sentensi. Viunganishi vinapounganisha sentensi kumuundo, huzaa sentensi ambatano. Mfano wa viunganishi vyta kileksia ni

*lakini, kwa sababu, au , wala, ingawaje* n.k. viunganishi hivi pia hutumika kuunganisha dhana na vinapotumika huwa na uamilifu wa kisemantiki unaoleta mshikamano katika matini.

Uunganishi wa kisemantiki huenda zaidi ya viunganishi vya kategorigoria ya kisintaksia. Viunganishi vya kisemantiki, huunganisha dhana mbili au zaidi katika matini ambazo lazima ziwe na uhusiano kimuktadha. Aidha, dhana moja hudhania dhana tangulizi. Uunganishi unapotokea katika hali hii, ndipo huleta mshikamano katika matini. Mfano wa viunganishi hivi ni *hata hivyo, baada ya, kabla ya, baadaye, kisha, kwa minajili ya, kutokana na, hivyo, pia, hatimaye, zaidi ya, kando ya*, n.k.

## 2.2 Vipatanishi vya kileksimu

Hivi vinaweza kuwa ama vifupi au virefu; vinaweza kutokea katika sehemu ndogo ya diskosi au katika sehemu kubwa. Wakati mwingine, neno au kisawe cha neno hilo kinaweza kutumika na kurudiwa katika sehemu mbalimbali za matini. Wakati mwingine, maneno yanayohusiana na neno hilo yanaweza kutumika. Urudiaji wa namna hii unawezesha mshikamano katika matini:

### Urudiaji

‘Sue is in the *race* on Saturday. Everyone believes that she or Tamara will win the *race*’

(Sue atashiriki *mashindano ya mbio* jumamosi. Kila mtu anaamini kuwa yeye au Tamara atashinda *mashindano* hayo ya mbio)

### Visawe

‘Sue hopes to set a PR. Her *personal best* is still 1.2 seconds’

(Sue anatarajia kuweka rekodi yake. *Yake nzuri zaidi* bado ni sekunde 1.2)

### Visawe unganishi

‘She’ll win a *trophy*. The prize won’t mean as much to her as a new PR’

(Atashinda *kikombe*. Tuzo hilo halitakuwa na maana sana kwake kama vile rekodi yake mpya)

### Jina la jumla

‘The *runner* needs to be well prepared to be competitive in this race.’

(*mkimbiaji* anatakiwa kuwa amejitayarisha vyema ili ashindane vizuri katika mbio hizi)

Vipatanishi vya kileksia pia hufungamanishwa kwa utangamano hivi kwamba tunapofikiria kuhusu ua kwa mfano, tunafikiria pia kuhusu shina, majani, petali na kadhalika na labda hata chombo ambamo ua hilo limewekwa.

## **2.2 Yaliyoandikwa kuhusu mada**

Wataalamu mbalimbali wameshughulikia suala la mshikamano. Wengi wao (Halliday 1985; Halliday na Matthiessen 2004; Omondi 1993; Salkie 1995; Thompson 2004; Olateju 2006) walishughulikia mshikamano katika Kiingereza na kuna wale walioshughulikia mshikamano katika Kiswahili mathalan Barang (1996). Kama

inavyobainika hapa wengi wa watafiti hawa wameshughuliki mshikamano kwa kurejelea matini andikwa.

Halliday (1985:288) anaeleza kuwa kuna njia nne ambazo kwazo mshikamano unaweza kuundwa katika kiingereza: urejeshaji, udondoshaji, uunganishi, na mpangilio wa leksimu. Kuhusu viunganishi, anaeleza kuwa kishazi au kishazi changamano au matini yenyе urefu fulani inaweza kuhusiana na kile kinachoifuata kwa seti maalumu ya mahusiano ya kisemantiki. Mahusiano haya kimsingi ni ya aina moja kama yale yanayopatikana kati ya vishazi katika sentensi ambatano. Halliday anaendelea kuhoji kuwa mahusiano unganishi huweza kuhusisha elementi hata katika viwango vyaya au visawe vyake katika lugha semwa. Viunganishi katika hali hii ni njia ya kuweka mahusiano ya kimantiki ambayo hupatikana katika sentensi ambatano.

Halliday (1985:303) anahoji kuwa viunganishi vinaweza kuwa na majukumu mbalimbali:

1) Ufafanuzi. Kuna aina mbili za mahusiano fafanuzi

(a) Mrejeosawa

Katika aina hii ya ufanuzi, elementi fulani inawasilishwa au kutajwa upya ama (i) kwa ufanuzi/maelezo → mahusiano ya ‘yaani’ au kwa mahusiano ya ‘kwa mfano’

Mifano ya viunganishi hivi ni:

- (i) Mrejeosawa. Mathalani: kwa maneno mengine, hivi ni kusema, ninamaanisha (kusema), kuweka kwa maneno mengine
- (ii) Kwa kutumia mifano. Mathalan: kwa mfano, mathalan na kadhalika.

(b) Ufafanuzi

Hapa elementi inayofafanuliwa haitajwi tu kwa mara ya pili bali hurejeshwa mahali pake, ikatolewa muhtasari na kufupishwa zaidi:

- i) Urekebishaji: au pengine, angalau, kwa hakika.
- ii) Yenye kuvuta mawazo: ‘by the way’, ‘incidentally’
- iii) Yenye kutoa fikirani: kwa vyovyote vile, hata hivyo, tukiachana na hayo
- iv) Yenye kuonyesha umahususi: hasa, zaidi
- v) Yenye kurudisha nyuma: kama nilivyokuwa nikisema, kurudi nyuma, kurejelea hoja hiyo.
- vi) Yenye kufupisha: kwa ufupi, kwa muhtasari, katika kuhitimisha, kifupi na kadhalika
- vii) Yenye kuthibitisha: kwa hakika, kwa kweli

2) Kupanua

Upanuzi unahuishisha kuongeza au kutoa vibadala. Nyongeza inaweza kuwa chanya (na) au asi (wala) au inayoteka mawazo (lakini). Lakini kwa sababu mahusiano yanayoteka mawazo huchukua nafasi muhimu katika diskosi ni vyema ichukuliwe kama mada kivyake. Matumizi ya vibadala huhusisha aina za ubadilishaji, uondoaji, na ubadala.

Kuna mifano mbalimbali inayodhihirisha upanuzi:

a) Kuongeza

i) Chanya: na, pia, zaidi, kuongezea

ii) Asi: wala

b) Yenye kuteka mawazo: lakini, kwa upande mwengine, hata hivyo.

c) Matumizi ya vibadala:

- i) Inayochukua nafasi ya nyingine: kinyume cha hayo, badala ya
- ii) Yenye kuondoa: licha ya hayo,
- ii) Yenye vibadala: ‘*alternatively*’.

3) Uzidishaji.

Aina mbalimbali za uzidishaji zinazounda mshikamano ni (a) Urejeshaji wa mahali (b) namna (c) kisababishi hali (d) suala.

**a)** Urejeshaji wa mahali unaweza kutumika kama kiunganishi katika matini k.m. hapa na pale, vielezi vya mahali kama vile ‘nyuma na’, ‘karibu na’, pamoja na tungo zilizo na nomino za mahali kwa mfano; ‘mahali sawa’, ‘popote pale’ na kadhalika. Hapa mahusiano ya mahali yanatumika katika kuunda vijenzi vya mshikamano. Viunganishi hivi huweza kuwa vya kiistriara. Kwa mfano; ‘mwanzo’, ‘kwa upande mwininge’. ‘*Upande*’ hapa unachukuliwa kuwa ni sehemu ya mjadala.

Viunganishi vya muda hudhihirisha aina nyingine nyingi za mahusiano:

- i) Sahili
  - a) Kufuatia: ‘halafu’, ‘kisha’, ‘baadaye’, ‘mwanzo .... kisha’,
  - b) Mfululizo: ‘mara tu’, ‘wakati uo huo’
  - c) Tangulizi: ‘kabla ya hapo’, ‘awali’
  - d) Hitimishi: ‘mwishowe’, ‘hatimaye’.

ii) Changamano

- a) Mara tu baada ya: ‘mara moja’ ‘kisha baada ya hapo’
- b) Katizi: ‘punde’, ‘baada ya kitambo kidogo’
- c) Radidi: ‘mara nyingine’, ‘wakati mwingine’
- d) Maalumu: ‘siku ya pili’, ‘saa moja baadaye’, ‘asubuhi hiyo’
- e) Ya muda: ‘wakati huo’, ‘wakati huo wote’
- f) Kukamilisha: ‘hadi hapo’, ‘kufikia hapo’.
- g) Wakati halisi: ‘wakati huu’

Viunganishi vinavyoitwa ‘changamano’ ni vile ambavyo huwa na muundo sahili lakini pia vina sifa nyingine za kisemantiki zinazodhihirika kwa wakati mmoja.

Viunganishi hivi vya muda vina fasiri ya ‘ndani’ na ya ‘nje’. Hili linadhihirika hivi kwamba wakati ambao vinaashiria ni muda huo ambapo diskosi yenewe inafunguka na wala sio mfuatano wa muda unaohusu michakato inayoashiriwa. Kuhusu vigezo amilifu vya Semantiki, kilicho muhimu ni mahusiano baina ya msemaji na msikilizaji na wala sio wakati wa majaribio. Sambamba na kategoria sahili zilizo hapo juu tunaweza kutambua:

iii) Sahili za ndani

- a) Kufuatia: kisha, pili, mwanzo ... kisha.
- b) Mfululizo: wakati huu, , hapa, sasa
- c) Tangulizi: hadi sasa
- d) Kuhitimisha: mwisho, mwisho wa yote, hatimaye.

Viunganishi hivi vya muda huelekeza katika sitiara za muda na kuleta aina kama vile ‘kwa wakati huu’, ‘kwa wakati huo’

- e) Linganishi: viunganishi vya namna hii hujenga mshikamano:
- b) Uzidishaji unaodhihirisha namna. Uzidishaji wa namna hufanikisha mshikamano kwa njia mbili kuu:
  - i) Kwa ulinganishi na
  - ii) Kwa urejeshaji wa namna.

Halliday na Matthiessen (2004:546-548) wanafafanua kuwa viunganishi vya ulinganishi hivi vinaweza kuwa chanya au asi: Viunganishi linganishi chanya ni kama vile ‘vilevile’, ilhali vilivyo asi ni kama vile ‘kwa njia nyingine’. Aidha, wanafafanua kuwa baadhi ya tungo zinazodhihirisha namna; hasa zilizo na ulinganishi pia huweza kudhihirisha uunganishi kwa mfano: ‘kwa namna sawa’.

- c) Hali sababishi: uunganishi hapa hutokana na kuonyesha sababu ya kutokea kwa jambo fulani. Midhihiriko ya sababu huweza kuwa ni ya jumla, mingine huhusisha zaidi athari au matokeo na mingine sababu au madhumuni.
- i) Jumla: kwa hivyo, kisha, hivyo, kutokana na hayo, kwa sababu ya hiyo, kwa sababu

ii) Mahususi:

- a)** Matokeo: kutokana na hayo
- b)** Sababu: kwa sababu hiyo
- c)** Madhumuni: kwa ajili ya hiyo, kwa kushikilia hili

Midhihiriko ya hali hugawika katika sehemu tatu:

- i) Chanya: kisha, katika hali hiyo
- ii) Asi: vinginevyo, ikiwa sivyo
- iii) Ridhifu: bado, ingawa, ingawa hivyo

**d)** Rejelezi: hapa mshikamano unatokana na urejeshaji kwa habari iliyotangulia. Kama ambavyo imeelezewa tayari, midhihiriko mingi ya habari (matter) ni sitiara za mahali zinazohusisha maneno kama vile sehemu, uwanja na kadhalika na haya huwa viunganishi wakati yameunganishwa na vigezo vya urejeshaji. Mifano ni:

- i) Chanya: hapa, pale, katika hali hiyo,
- ii) Asi: kwagineko.

Omondi (1993) alichunguza umilisi wa mshikamano unavyohitajika katika uandishi wa insha za Kiingereza. Alichunguza insha za Kiingereza za wanafunzi wa kidato cha nne wa shule za upili wilayani Migori, Kenya. Alichunguza matumizi ya urejeshaji, ubadilishaji, udondoshaji, uunganishaji, na kileksia katika insha hizo. Katika utafiti wake, alitumia maswali ya uteuzi, kujaza vijenzi vya mshikamano katika mapengo ambamo vijenzi viliachwa kwa makusudi katika insha zilizoandikwa na wanafunzi wenyewe.

Utafiti wa Omondi ulisaidia utafiti huu katika kufanya ufanuzi wa kijumla kuhusu mshikamano.

Salkie (1995) alieleza aina mbalimbali za mshikamano na vijenzi katika matini na usemi. Alibainisha mshikamano wa kileksia na mshikamano wa kisarufi na kuonyesha jinsi vijenzi vya aina hizi za mshikamano vinatumika katika matini za Kiingereza. Alionyesha urejeshaji, udondoshaji, ubadilishaji, uunganishi na mshikamano wa kileksia. Alitumia dondo Kutoka kwa matini za Kiingereza '**The Gurdian**', '**Economic Times**' na hotuba mbalimbali. Alieleza kuwa mshikamano wa kileksia huletwa na urudufishaji wa maneno, matumizi ya visawe, maneno jumuishi na maneno husishi. Aidha, alieleza mshikamano wa kisemantiki unavyojitokeza katika matini za Kiingereza ambao hautegemei vijenzi vya mshikamano. Utafiti wa Salkie ulishughulikia Kiingereza na ulijikita katika kuchunguza matini andishi. Utafiti huu unatofautiana na ule wa Salkie kwa kuwa unachunguza matini semwa za lugha ya kibantu (Kikisii). Utafiti wa Salkie hata hivyo ulitoa mchango katika kufafanua mshikamano kwa jumla.

Barongo (1996) alifanya utafiti kuhusu mshikamano kwa jumla kaika insha za wanafunzi wa kidato cha nne zilizoandikwa kwa Kiswahili wilayani Kisii, nchini Kenya. Alichunguza vijenzi vyote vya mshikamano kama vilivyotumika katika insha za wanafunzi hao. Alichunguza iwapo vijenzi hivyo vinawezesha mshikamano katika insha hizo. Barongo alipata kuwa wengi wa wanfunzi hawakutumia vijenzi hivyo kwa njia sahihi katika insha zao na hivyo kuzifanya insha zao kukosa mshikamano. Ingawa utafiti wa Barongo ulitoa mchango katika kufafanua namna vijenzi mbalimbali hufanikisha

mshikamano, utafiti huo ulijikita tu katika matini zilizoandikwa (insha). Utafiti huu unatofautiana na utafiti wa Barongo (1996) kwa kuwa huu unarejelea matini semwa na umejikita zaidi katika kupambanua vijenzi unganishi vyta mshikamano pekee hasa viunganishi na leksimu patanishi.

Thompson (2004) naye ameshughulikia namna ya kuendeleza ujumbe kwa kutumia mshikamano. Anaeleza kuwa msemaji hujaribu kwa kila namna kuhakikisha kuwa ameeleweka na msikilizaji. Msemaji hufanya hivyo kwa kuipanga matini kwa namna ambavyo maana itajitokeza wazi. Mtaalamu huyu anatumia mshikamano na vilevile muwala katika kushughulikia matini. Anadai kuwa mshikamano unarejelea vijenzi vyta kiisimu ambavyo msemaji hutumia kueleza yaliyomo mawazoni mwake na kukamilisha muwala wa kiuhusiano baina yake na msikilizaji wake.

Kulingana na Thompson, mshikamano ni suala la kimatini. Anafafanua kuwa muwala ni dhahania kwa kuwa huhusisha mwingiliano na uwiano baina ya kile kilicho katika ubongo wa msemaji na kile kilicho katika ubongo wa msikilizaji. Kwa upande mwingine, unachukuliwa kuwa kile kilichomo katika ubongo wa msemaji na katika ubongo wa msikilizaji. Anadai kuwa mshikamano na muwala vinaingiliana hivi kwamba vijenzi vyta mshikamano katika matini vinatumika kwa namna inayoleta muwala. Hata hivyo watumizi wengi wa lugha inaelekea wanaweza kupata muwala katika matini hata ikiwasio vijenzi vyote vyta mshikamano vimetumika katika matini hiyo. Thompson (2004:180) anafafanua kuwa mshikamano ni malighafi muhimu sana ya kiisimu katika uwasilishaji wa maana patanifu.

Kuhusu VUM, Thompson (2004:189) anaeleza kuwa uunganishi unarejelea kwa mapana kule kuweka pamoja elementi mbili za matini ili kuunda kipashio kimoja changamano cha kisemantiki ambacho kina muwala. Anadai kuwa viunganishi vinaweza kuchanganuliwa kwa kuzingatia viwango vitatu vikuu: katika vishazi (kama vihusishi), kati ya vishazi (viunganishi) na kati ya vishazi au sentensi changamano (viunganishi chagizi). Kati ya hivi, viunganishi chagizi ndivyo vinavyofanikisha mshikamano katika sentensi ambatano. Thompson anaorodhesha viunganishi hivi chagizi na kisha kujadili aina mbalimbali za mahusiano ya kiunganishi yanayoashiriwa kwavyo.

Kwa upande mwingine, Thompson anachukulia kuwa inaweza kushikiliwa kuwa katika matumizi ya lugha ya kawaida kila kishazi chochote kinaweza kuchukuliwa kuwa kina uhusiano wa kipatanifu na kishazi au vishazi vingine ambavyo vinakitangulia. Hivyo, kishazi tangulizi kinaweza kutoa muktadha wa kufanyia fasiri ya vishazi vinavyofuata. Kutokana na madai haya, tunaweza kuchanganua aina za jumla za mahusiano yaliyopo baina ya vishazi katika matini na mwishowe tuchunguze sifa zozote za kimshikamano katika matini ambazo zinaashiria mahusiano hayo katika kila hali. Mwelekeo huu utatuwezesha kutambua seti za ishara za mshikamano ambazo zinahusisha nyingine ambazo kimapokeo huhesabika kuwa ni viunganishi. K.m.

- a) “The prince alienated the aristocracy because he did not visit. *This was probably not a question of snubbing them or of snobbery but of a certain rectitude.*”  
 (Mwana wa mfalme alifarakisha utabaka kwa sababu hakuzuru. Hili **halikuwa suala la** kuwapuuza au upuuzaji **bali** njia ya uadilifu)

- b) “After 10 years of standardization, there should be a healthy UK market for used models. *Curiously*, there seems to be only one big second-hand PC leader in London”

(Baada ya miaka kumi ya usawazishaji, kunatakiwa kuwepo soko zuri la miundo (ya tarakilishi) iliyotumika. **La ajabu** ni kuwa inaelekea kuna muuzaji mmoja tu wa tarakilishi zilizotumika London.)

Katika mfano wa kwanza, kumetumika **KUM** ‘*question*’ (swali) ambacho kinafanya kazi kama kibadala cha ‘*because of*’ (kwa sababu). Katika mfano wa pili kumetumika **KUM** ‘*curiously*’ (la ajabu) ambacho kinafanya kazi badala ya ‘however’ (hata hivyo). Vipashio ‘*question*’ na ‘*curiously*’ vimetumika ili kuleta mshikamano katika tungo ambamo vimetumika. Kipashio ‘*because of*’ (kwa sababu) kama kilivyotumika katika mfano wa kwanza kinajitokeza kimapokeo kama kiunganishi. ‘*curiously*’ (la ajabu) ambacho kimejitokeza katika mfano wa pili ni kiunganishi chagizi. Kimapokeo, kiunganishi chagizi hakikuchukuliwa kuwa ni kiunganishi (kilichukuliwa kuwa hakina dhima sawa na kiunganishi). Hii inatokana na hali kwamba mawazo kuhusu viunganishi nyakati hizo yalichukuliwa kuwa finyu mno.

Mifano hii miwili inapelekea kuwepo kwa mitazamo miwili kuhusu viunganishi. Kwanza mtazamo finyu kuwa maneno fulani tu ndiyo yanayoweza kuwa viunganishi kwa mfano, ‘na’, ‘lakini’, ‘au’ na kadhalika. Mtazamo wa pili ni ule unaoangalia viunganishi kwa upana; unachukulia kuwa hata miundo chagizi pia ina uwezo wa kuwa viunganishi. Uchunguzi wa makini hata hivyo, unadhihirisha kuwa mitazamo hii miwili inaingiliana

kwa karibu hivi kwamba kutohana na matumizi ya vipashio hivi<sup>1</sup> uunganishi unapatikana na hivyo muwala unaafikiwa.

Hoey (2000) anazingatia mtazamo wa pili kuhusu viunganishi na anashikilia kuwa hatupaswi kuwa na fikira finyu tunaposhughulikia viunganishi. Halliday na Matthiessen (2004) wanashikilia mtazamo wa kwanza lakini wanashikilia kuwa viunganishi vinapaswa kutazamwa kwa upana wake kwa kuwa kila diskosi hudhihirisha matumizi tofauti ya viunganishi. Tasnifu hii iliegemea mtazamo wa pili ambao uliviangazia viunganishi kwa upana wake; ulichukulia kuwa kiunganishi ni kijenzi cha kiisumu ambacho hufanya kazi ya kuweka pamoja neno na neno, kundi/kirai na kingine au kishazi na kingine. Aidha, ulichukulia kuwa kiunganishi kinaweza kuwa ni neno moja, kirai au kishazi ambacho kinatekeleza amali ya kuweka pamoja elementi za kimatini kwa namna inayofanikisha muwala.

Thompson (2004) anadai kuwa viunganishi vinavyotumika katika tungo fulani hutegemea na ni dhamira gani iliyomo katika tungo hiyo pamoja na hali ya tungo yenyewe. Anafafanua kuwa kuna aina mbalimbali za viunganishi, mathalani: vya sababu na athari (kwa sababu, sababu, na kwa hivyo); hali (ikichukuliwa kuwa, ikiwa, katika hali hiyo); vya kuridhia (liche ya, ingawa, isitoshe); vya kulinganisha na kulinganua (kama, ilhali, hivyo hivyo); vya wakati (kwa wakati huo, baada) na kadhalika. Katika orodha hii, Halliday na Matthiessen wanaongezea viteka mawazo (*by the way*) na vifafanuzi (kama ninavyosema).

---

<sup>1</sup> Maneno yenye dhima ya uunganishaji pamoja na chagizo zenye dhima ya uunganishaji

Olateju (2006) alishughulikia mshikamano katika matini andikwa za watoto waliokuwa wakisoma Kiingereza kama lugha ya pili. Alichunguza ni kwa namna gani wanafunzi wanaosoma Kiingereza kama lugha ya pili walivyoweza kutumia vijenzi vya mshikamano katika kuandika matini mbalimbali. Wanafunzi walitakiwa kuandika insha mbili ambazo zilinuiwa kudhihirisha uwezo wao wa kutumia vijenzi vya mshikamano. Uchanganuzi wa data ulidhihirisha kuwa wanafunzi hawakuwa na uwezo mzuri wa kutumia vijenzi vya mshikamano licha ya kuwa walikuwa wamefundishwa Kiingereza kama lugha ya pili kwa muda wa miaka sita katika shule za upili. Wanafunzi hawa walikuwa wa shule ya upili ya wasichana ya Ooni iliyo katika jimbo la Osun nchini Nigeria. Kwake Olateju (2006) mshikamano ni mahusiano ya maana yaliyomo katika matini; ni sehemu ya mfumo wa lugha inayofanikisha maana katika matini.

Mecha (2013) alichunguza lugha ya Kikisii ili kuchanganua jinsi amali za kipragmatiki (mada na fokasi) zinavyoathiri vipengele viwili vya diskosi ambavyo ni: mpangilio wa umbo na yaliyomo katika mpangilio wa maneno pamoja na muwala wa kiurejeshaji. Utafiti wa Mecha ulibaini kuwa vikwazo vya muundo wa ujumbe katika kiwango cha sentensi haswa huweza kuathiri hali ya ujumbe unaotokana na mpangilio wa maneno unaokubalika au usiokubalika. Utafiti wa Mecha pia ulibaini kuwa vikwazo hivyo vinaweza kuathiri fasiri inayofanywa na msikilizaji kuhusu mada husika.

Makoti (2013) amefanya utafiti kuhusu mshikamano wa kisarufi katika Kiswahili. Katika utafiti huu amechunguza na kufafanua vijenzi mbalimbali vinavyoleta mshikamano wa kisarufi. Vjenzi hivyo ni urejeshaji, ubadilishaji, udondoshaji na uunganishi.

Alichanganua jinsi vijenzi hivi vinatumika katika kuleta mshikamano na ufungamano katika matini zilizochunguzwa. Matini zilizochunguzwa ni za nathari za Kiswahili: *Watoto wa Mama 'tilie* (Mbogo, E) na *Musaleo!* (Wamitila, K.W). Utafiti wa Makoti ulionyesha jinsi vijenzi vya mshikamano vilitumika katika kuunganisha sentensi na dhana ili kuleta mshikamano na ufungamano katika matini zilizoteuliwa. Aidha, utafiti huo ulichunguza ikiwa vijenzi hivi hukumbwa na vikwazo katika Kiswahili na kuharibu au kudhibiti sarufi katika matini. Kutokana na utafiti huo ilidhihirika kuwa kuna vikwazo kati ya urejeshaji, ubadilishaji na uunganishi. Vikwazo hivi hutokea kwa sababu ya mchakato na sheria za lugha yenye. Hivyo hubidi wakati mwingine, vikwazo hivi vipuuzwe ili kukwepa uharibifu wa mshikamano katika matini. Utafiti uligundua kuwa baadhi ya vijenzi vya mshikamano hutumika zaidi kuliko vingine. Utafiti wa Makoti ulitoa mchango mkubwa katika utafiti huu hasa kutokana na fasili mbalimbali pamoja na maelezo yaliyotolewa kuhusu mshikamano pamoja na vijenzi mbalimbali vya mshikamano. Hata hivyo utafiti huu unatofautiana na ule wa Makoti kwa kuwa umejikita katika kupambanua jinsi vijenzi unganishi vya mshikamano na hasa uunganishi na leksimu patanishi hutumika kufanikisha mshikamano katika matini semwa za Kikisii.

Hatch (1992) amezingatia mno suala la mshikamano na kupuuza muwala. Ni vyema ifahamike kuwa mshikamano pekee hauwezi kufanikisha mawasiliano. Ni lazima pia muwala uhusishwe. Hatch anakiri kuwa tunaweza kutumia leksimu mbalimbali kama vijenzi vya mshikamano kwa kutegemea diskosi tunayojenga na kuwa hii hujitokeza wazi kutegemea na chaguzi zetu za vijenzi unganishi. Kando na kukiri huku, Hatch hafafanui ni kwa namna gani diskosi mbalimbali tunazojenga zinaweza kuathiri matumizi ya

leksimu ili kufanikisha mshikamano. Winter (1971) naye anafafanua vijenzi unganishi katika Kiingereza. Hata hivyo, haonyeshi jinsi vijenzi hivi unganishi vinafanikisha mshikamano na muwala katika matini na iwapo kando na uunganishi kuna amali nyingine ambazo zinatekelezwa na vijenzi hivyo.

Olateju (2006) alishughulikia mshikamano katika matini andikwa za wanafunzi waliokuwa wakisoma Kiingereza kama lugha ya pili. Olateju hakuchanganua maumbo au miundo ya vijenzi vya mshikamano. Aidha, hakubainisha iwapo kando na mshikamano kuna amali nyingine zinazotekelawa na vijenzi hivyo. Upungufu huu vilevile unajitokeza katika Thompson (2004) ambaye vilevile hafafanui iwapo kando na kufanikisha mshikamno na muwala kuna amali nyingine ambazo vijenzi hivi vya mshikamano vinatekeleza. Ingawa Halliday (1985) na vilevile Halliday na Matthiessen (2004) wamelijadili suala hili la VUM kwa undani, walijikita tu katika lugha ya Kiingereza. Isitoshe hawakuyapambanua maumbo na miundo ya VUM walivyojadili.

Utafiti wa Mecha (2013) uliegemea zaidi suala la urejeshaji kama kipashio kinachoathiri muwala. Utafiti huu haukushughulikia vijenzi unganishi vya mshikamano na pia haukujadili namna mshikamano unavyoafikiwa katika matini za Kikisii.

Utafiti huu unaua kutoa mchango ambao inaelekea haukuzingatiwa katika kazi za wataalamu tuliowataja: Hatch (1992); Winter (1971); Barongo (1996); Olateju (2006); Thompson (2004); Halliday (1985); Mecha (2013) na Halliday na Matthiessen (2004) na wengine. Utafiti huu ulijikita katika kufanya uchunguzi kuhusu maumbo na miundo

mbalimbali ya VUM na vilevile amali mbalimbali ambazo VUM hivyo hutekeleza. Ikizingatiwa kuwa wataalamu tuliotaja hapo juu wamechunguza mshikamano katika matini andishi, uchunguzi huu utatoa mchango katika taaluma ya isimu kwa kuwa umeshughulikia matini semwa. Mchango huu unatarajiwa kuwa muhimu hasa kutokana na ukweli kuwa usemi ni asilia zaidi ikilinganishwa na maandishi. Aidha, utafiti huu ulijikita sio tu katika kuchunguza jinsi mshikamano unavyofanikishwa na VUM bali pia jinsi VUM hufanikisha muwala. Isitoshe, ulichanganua iwapo kuna amali nyingine ambazo hufanikishwa na VUM kando na mshikamano na muwala katika matini. Ikishikiliwa kuwa wataalamu wengi tuliotaja hapo juu walifanya chunguzi zao kwa kuegemea Kiingereza, utafiti huu unatoa mchango kwa kuchunguza VUM katika Kikisii ambayo ni lugha ya KiBantu.

### **2.3 Hitimisho**

Maandishi tuliojadili hapo juu kuhusu mshikamano yanachangia katika kufanya upambanuzi wa dhana ya mshikamano. Tafiti mbalimbali zilizohakikiwa katika sura hii zimechangia katika kuweka wazi dhana na vipengele muhimu vyta mshikamano. Aidha, maelezo pamoja na mifano ya vijenzi mbalimbali vyta mshikamano iliyotelewa katika sehemu hii, imetoa mchango mkubwa katika kutoa fasiri ya mshikamano na kupambanua aina mbalimbali za vijenzi hivyo vyta mshikamano. Isitoshe, mifano na fafanuzi hizi mbalimbali zimetoa mwanga katika kujadili na kutoa mifano ya Kikisii kama ilivyobainika katika utafiti huu.

## **SURA YA TATU**

### **MAUMBO NA MIUNDO YA VIJENZI UNGANISHI VYA MSHIKAMANO**

#### **3.0 Utangulizi**

Sura hii inaweka wazi maumbo na miundo ya VUM (U) kama vilivyodhahirika katika matini semwa mbalimbali za Kikisii. Uchanganuzi uliofanywa katika sura hii ulilenga katika kuonyesha ni vipi ambavyo VUM katika matini semwa za Kikisii vimeumbika. Sura hii pia inachanganua aina mbalimbali za VUM (LP) vinavyopatikana katika matini semwa za Kikisii. VUM (LP) vilivyochanganiwa katika sura hii vilibainika kutokana na udondoshaji na vilevile uradidi.

#### **3.1 MAUMBO, MIUNDO NA AINA ZA VUM (VIUNGANISHI)**

Ilibainika kuwa VUM (U) katika matini semwa za Kikisii huwa na maumbo pamoja na miundo mbalimbali. Kulibainika VUM (U) vilivyo vya mofu moja pekee, vilivyo na neno moja pekee, na vilivyo na maneno mawili. Aidha, kulibainika VUM (U) ambavyo vilikuwa na muundo wa virai na vile ambavyo vilikuwa na muundo wa vishazi tegemezi.

##### **3.1.1 Vya mofu moja**

Kutokana na uchanganuzi uliofanywa katika utafiti huu, ilidhahirika kuwa katika matini semwa za Kikisii kuna VUM (U) ambavyo huwa na mofu moja. Ilibainika kuwa VUM (U) vyenye mofu moja katika matini semwa za Kikisii huwa vya aina mbili. Hizi huwa ni ‘ko’ na ‘na’.

**Ko**  
**MF4<sup>1</sup>**

(Muktadha: Mazungumzo ya kijamii: *Mzungumzaji a anazungumza kuhusu kijana fulani ambaye alitoka nyumbani kwenda kufanya kazi mjini*)

| Kikisii  | Kiswahili   |
|--|---|
| Omwana oyu nigo arenge omoigweri mono. Meremo ende yonsi arenge koegu nigo arenge konyekora atabwati mioyo ebere. Buna bono engaki eyemo nigo airetu achi gokora emeremo bw'omogambi. Nomanyete nga nairete engaki entambe gokora emeremo eyu atanyoreti besa ende <b>ko</b> takweti moyo. Akaba kagokora emeremo eyu atari kweiranana nonya ngake. Noo aberete abu goika engaki gete ekero omogeni gete achete abwo bw'omogambi. Agacha komororera amabera akomoira esukuru.... | Mtoto huyo alikuwa msikivu sana. Kazi yoyote ambayo angepewa aliifanya bila ya kuwa na mioyo miwili. Kama sasa wakati mmoja alipelekwa kwenda kufanya kazi kwa chifu. Unajua kuwa alifanya kazi hiyo kwa muda mrefu akifanya kazi hiyo bila ya kupata pesa zozote <b>ila</b> hakufa moyo. Akawa anaifanya kazi hiyo bila manunguniko hata kidogo. Alikaa huko hadi wakati fulani ambapo mgeni fulani alikuja hapo kwa chifu. Akamwonea huruma akampeleka shule..... |

Nairete engaki entambe gokora emeremo eyu atanyoreti besa ende/ *ko takweti moyo* ni-a-ir-ete e-ngaki e-ntabe go-kor-a e-me-remo e-yu a-ti-a-nyor-eti besa e-nde/ *ko ti-a-kw-eti moyo*

KIM-NFS3U-NJ-MZZ-MAT NGL-MZZ Kat-MZZ-IT NGL-IDW-MZZ NGL-MZZ NFS3U-KAN-NJ-MZZ-MAT N NGL-MZZ **KUM** KAN-NFS3U-MZZ-MAT E

(Alichukua muda mrefu kufanya kazi hiyo bila ya pesa zozote ila hakufa moyo)

Katika **MF4<sup>1</sup>** kumetumika **KUM** ambacho kina mofu moja - '**ko**'. **KUM** hiki kimetumika ili kuunganisha tungo mbili ambazo ni: '*Nairete engaki entambe gokora emeremo eyu atanyoreti besa ende*' (alichukua muda mrefu kufanya kazi hiyo) na '*ere takweti moyo*' (yeye hakufa moyo) mofu '**ko**' katika mfano huu inawakilisha maana ya '**ila**'.

Ingawa KUM hiki ‘**ko**’ kinajitokeza kama KUM chenyé mofu moja katika **MF4<sup>1</sup>**, inajitokeza kuwa KUM hiki ni ufupisho wa KUM **korende** chenyé maana ya ila au lakini. Kwa kuwa VUM hivi viwili vinatekeleza maana sawa, vinaweza kuchukuliwa kuwa ni alomofu za mofimu moja yenyé maana ya ‘ila’ au ‘lakini’.

## **Na**

### **MF4<sup>2</sup>:**

**(Muktadha: Hadithi ambapo msimulizi anasimulia kisa kuhusu watoto fulani waliokuwa watundu)**

| Kikisii  | Kiswahili  |
|--|--|
| Egatoka nga tibakonyara gokora buna konyora batebigu n’abaibori babo. Tibachieti gokanyeka nore. Naki gekogera abange bare abareu <b>na</b> abarwaire. Naende tari boigo rioka, tibarikonyara nonya nokorengereri nga naki baranyare gwekonya ase obogima bwabo. | Ikawa kuwa hawangeweza kufanya kama walivyokuwa wameambiwa na wazazi wao. hawakupoa hata kidogo. Ndiyo sababu wengi ni wanyonge <b>na</b> wagonjwa. Tena si hivyo tu, hawawezi hata kufikiria ni vipi wanaweza kujisaidia katika maisha ya sasa. |

Naki gekogera abange bare abareu /**na** abarwaire

Naki ge-ko-ger-a a-bange ba-r-e a-ba-reu /**na** a- ba-rwaire

W NGL-Kat-MZZ-IT NGL-NGL IDW-MZZ-K NGL-IDW-MZZ **KUM** NGL-IDW-MZZ

(Ndicho kinafanya wengi kuwa wanyonge na wagonjwa)

Katika **MF4<sup>2</sup>** mofu ‘**na**’ imetumika kama **KUM** ambacho kinaunganisha tungo mbili:

‘*Naki gekogera abange bare abareu*’ (ndicho kinafanya wengi kuwa wanyonge) na ‘*Naki*

*gekogera abange bare abarwaire*’ (ndicho kinafanya wengi kuwa wagonjwa).

Kinachodhiihirika katika mifano hii miwili: **MF4<sup>1</sup>** na **MF4<sup>2</sup>** ni kuwa mofu ‘ko’ na ‘na’ zimefanya kazi kama vijenzi unganishi vyta mshikamano (**VUM**). Mofu hizi haziwekewi viambishi vyovyyote. Zinapotumika kama **VUM**, udondoshwaji hutokea katika tungo ya pili. Kwa mfano katika **MF4<sup>1</sup>**, KN(W) – ‘ere’ (yeye) imedondoshwa. Katika **MF4<sup>2</sup>**, kumedondoshwa sehemu nzima – ‘Naki gekogera abange bare...’ (ndicho kinafanya wengi kuwa...).

### **3.1.2 Vya neno moja**

Utafiti huu ulidhihirisha kuwa katika matini semwa za Kikisii kuna **VUM (U)** vilivyo na neno moja. Ilidhihirika kuwa **VUM** hivi huweza ama kuwa asilia au ambavyo vimezuliwa kutoka kwa vitenzi, kutokana na nomino au kutokana na vielezi.

#### **3.1.2.1 VUM asilia vya neno moja**

**VUM** asilia huchukuliwa kuwa vile ambavyo havijaundwa kutokana na maneno mengine na pia ambavyo havijaambatishiwa viambishi vingine. Katika matini semwa za Kikisii kulijitokeza ‘gose’, ‘na’, ‘aba’, ‘ani’ pamoja na ‘korende’ kama **VUM** asilia.

#### **Gose**

##### **MF5<sup>1</sup>:**

**(Muktadha: Mazungumzo ya kijamii. Wazee wawili c na d wanashiriki mazungumzo, mara anatokeza mtoto fulani na d anaamua kumtuma kwa mjomba wake)**

| Kikisii   | Kiswahili   |
|---|---|
| <p><b>C:</b> Ense ya bono yakongire. Tenga buna riri kare.</p> <p><b>D:</b> Aaah! Ee nabo igo tata. Noroche buna endagera yoka yachi igoro. Gose omonto igo ogosinyu mmeremo ki oranyore egere oikere oboigima bwa bono. (anatokeza mtoto fulani). Aye baba mbuya ore?</p> <p><b>Mtoto:</b> Ee! Mbuya mono sokoro</p> | <p><b>C:</b> Dunia ya sasa imekuwa ngumu. Sio kama zamani.</p> <p><b>D:</b> Aaah! Ee ni hivyo bwana. Unaona namna chakula pekee kimepanda. Si mtu unashindwa ni kazi utapata ili ufikie maisha ya sasa. (anatokeza mtoto fulani) we hujambo?</p> <p><b>Mtoto:</b> Ee! Sijambo babu</p> <p><b>D:</b> Nani yuko nyumbani?</p> |

|  |  |
|--|--|
| <p><b>D:</b> Ningo ore nka?</p> <p><b>Mtoto:</b> Ntata.</p> <p><b>D:</b> Igo mbuya. Gachi omotebi atome omwana<br/>ache kondora <b>gose</b> motebi ache ere<br/>bweka. Narosire namanga akonya<br/>gonkori. Tiga amanye nga nche n'omonto<br/>omonene. Tindi mwana nche.</p> | <p><b>Mtoto:</b> Ni baba</p> <p><b>D:</b> Hivyo ni vizuri. Nenda umwambie atumie mtoto<br/>aje kuniona <b>au</b> mwambie aje ye ye mwenyewe.<br/>Nimechoshwa na mambo ambayo ananifanyisha.<br/>Acha ajue kuwa mimi ni mtu mzima. Mimi si<br/>mtoto.</p> |
|--|--|

- a) Gachi omotebi atome omwana ache kondora / **gose motebi ache ere bweka**.  
**Gach-i o-mo-teb-i a-tom-e o-mw-ana a-che ko-n-ror-a / gose a-che ere bwe-ka**  
MZZ-IT NFS2U-SH-MZZ-ITKAN NFS3U-MZZ-MAT NGL1-IDU-MZZ **KUM** NFS3U-MZZ W NGL1-MZZ  
(Nenda umwambie atume mtoto aje kuniona au aje ye ye mwenyewe)

**(Muktadha: Darasani. Mwanafunzi anasimulia kuhusu maafa yanayoletwa na ukoma kama ilvyodhahirika katika hadithi moja)**

| Kikisii   | Kiswahili   |
|---|---|
| Oborwaire obu n'obobe pi. Bomochani<br>bokobwate igo bogokori bogokore pi. Buna<br>bono bokobwate gose nekiara nigo orarore<br>obororo obobe. Nabo kerasaboke pi keere <b>gose</b><br>kebutoke. Togani bokobwate gose bobwate onde<br>omino. Nobobe!! | Ugonjwa huo ni mbaya. Ukitushika utakumaliza<br>kabisa. Kama sasa ukitushika kidole utaona tabu<br>kubwa. Kinawenza kuchubuka kabisa <b>au</b><br>kikatike. Usitamani ukushike au ye yote wa<br>kwenu. Ni mbaya!! |

- b) Nabo kerasaboke pi keere /**gose kebutoke**.  
**Nabo ke-ra-sabok-e pi ke-ere /gose ke-butok-e**  
MZZ NGL-NJ-MZZ-MAT MZZ NGL-MZZ **KUM** NGL-MZZ-MAT  
(Kinawenza kuchubuka kabisa kiishe au kikatike)

Katika **MF5<sup>1</sup>** kumetumika **KUM** ‘**gose**’. Katika **MF5<sup>1a</sup>** **KUM** ‘**gose**’ kimetumika kuweka pamoja tungo mbili ambazo ni ‘*Gachi omotebi atome omwana ache kondora*’ (nenda umwambie atume mtoto aje kuniona) na ‘*Gachi omotebi ache ere bweka*’ (nenda umwambie aje ye ye mwenyewe). Katika sehemu hii, udondoshaji wa T ‘*gachi*’ (nenda) umefanywa. Katika **MF5<sup>1b</sup>** ‘**gose**’ imetumika katika kuunganisha tungo ‘*Nabo kerasaboke pi keere*’ (kinawenza kuchubuka kabisa kiishe) na ‘*Nabo kerabutoke*’

(kinaweza kukatika). Sehemu iliyodondoshwa hapa ni ‘*nabo*’ ambayo inachukua jukumu la KIM. Aidha, sehemu ‘*ra*’ iliyo na jukumu la NJ imedondoshwa katika sehemu ya pili ya tungo hii. Hivi ni kuashiria kuwa tungo hizi mbili zinashikamana kwa kuwa zinaashiria kirejelewa kimoja. Umbo **gose** huwa haliwekewi kiambishi chochote na hivyo huchukuliwa kuwa ni umbo asilia.

## **Na**

### **MF5<sup>2</sup>:**

**(Muktadha: Mazungumzo ya kijamii. Wasailiwa watatu wanajadiliana kuhusu amani)**

| Kikisii  | Kiswahili  |
|--|--|
| <p><b>Ondari:</b> Ninki mwanyabanto aranyare gokora bweka ase obogima obo?</p> <p><b>Mokua:</b> (Kicheko) Bosa! Bosa pi! Mwanyabanto takonyara kende gionsi, ngese ense eye ne ya Nyasae!</p> <p><b>Ondari:</b> Uuuu! Ee n’amaene tata. Naende tari nse yoka. Nonya nigoro. Ebuku nigo egoteba nga agwo omochakano Nyasae nigo atongete igoro na nse. <b>Na</b> ense tiyarenge na kieni kende. Ntu mwanyabanto gote nigo twachete aiga totabwati kende.</p> <p><b>Mauti:</b> (Akisafisha koo) eki mwanyabanto atakeire gosaba ase ense eye nomorembe. Nomanyete nga morembe obe toba oo mbosa. Meremo ende teiyo erakorekane! Onye omonto gotagete</p> | <p><b>Ondari:</b> Ni nini mwanadamu mwenyewe anaweza kufanya katika maisha haya?</p> <p><b>Mokua (Kicheko)</b> Bure! Bure Kabisa! Mwanadamu hawezi chochote, si hii dunia ni ya Mungu!</p> <p><b>Ondari:</b> Uuuu! Ni kweli bwana. Tena si dunia pekee. Hata juu. Bibilia inasema kuwa hapo mwanzo Mungu aliumba mbingu na nchi. <b>Na</b> dunia haikuwa na sura yoyote. Sisi binadamu si tulikuja hapa bila kuwa na kitu.</p> <p><b>Mauti:</b> (Akisafisha koo) anachotakiwa kuomba mwanadamu katika ulimwengu huu ni amani. Unajua kuwa bila ya amani ni bure. Hakuna kazi inayoweza kufanyika! Iwapo mtu unataka kusaidika omiba sana kuwa: amani iwe kwako na kwa nyumba yako.</p> |

|  |  |
|--|--|
| gokonyeka saba mono nga:<br>Omorembe obe ase ore na ase<br>enyomba yao |  |
|--|--|

- a) Agwo omochakano Nyasae nigo atongete igoro na nse./ *Na ense tiyarenge na kieni kende*

Agwo o-mo-chakano Nyasae nigo a-tong-ete igoro na nse. / *Na e-nse ti-ya-rengé na kieni ke-nde*

MZZ NGL-IDU-MZZ MZZ KIM NFS3U-MZZ-K MZZ U MZZ. **KUM** MZZ PING-NGL-MZZ U MZZ NGL-MZZ

(Hapo mwanzo Mungu aliumba mbingu na nchi. **Na** nchi haikuwa na sura)

- b) Omorembe obe ase ore /*na ase enyomba yao*

O-morembe o-b-e ase o-re / *na ase e-nyomba ya-o*

NGL-MZZ NGL-MZZ-MAT MZZ NFS2U **KUM** MZZ NGL-MZZ NGL-NFS2U

(Amani iwe kwako na kwa nyumba yako)

Katika **MF5<sup>2</sup>a** na **MF5<sup>2</sup>b** ‘na’ imetumika kama **KUM**. Matumizi ya ‘na’ katika mifano hii yanafanikisha mshikamano katika tungo husika. Katika **MF5<sup>2</sup>a**, kumejitokeza kurudiwa kwa kipashio ‘ense’ (nchi). Kipashio hiki kimetokeza mara tu kabla na mara tu baada ya ‘na’. Matumizi ya **KUM** ‘na’ katika tungo hii yanafanikisha kushikamana kwa tungo mbili: ‘*Agwo omochakano Nyasae nigo atongete igoro na nse*’ (hapo mwanzo Mungu aliumba mbingu na nchi) na ‘*Ense tiyarenge na kieni kende*’ (Nchi haikuwa na sura yoyote) ‘na’ hapa imetumika kwa madhumuni ya kuendeleza ujumbe ambao ulikuwa umetangulizwa katika tungo ya kwanza. **KUM** ‘na’ vilevile hakiwekewi viambishi vyovoyote na huchukuliwa kuwa ni cha asilia.

Katika **MF5<sup>2b</sup>**, kunajitokeza udondoshaji wa vipashio ‘*omorembe obe*’ (amani iwe) ni dhahiri kuwa udondoshaji huu umetokana na matumizi ya **KUM** ‘na’. **KUM** ‘na’ kinadhihirika kuwa asilia kwa kuwa hakijafungamanishwa viambishi vyovyyote.

## Aba

### **MF5<sup>3</sup>:**

(**Muktadha: Mazungumzo ya kijamii. Wazungumzaji wawili James na Mikuro wanazungumza juu ya mwenzao aliyenunua shamba**)

| Kikisii   | Kiswahili  |
|---|--|
| <p><b>Mikuro:</b> Tiga obongainereri (huku akicheka) momura ori takogora boremo pi.</p> <p><b>James:</b> Ninki bono ogokwana. Ngese ninche mmomanyete buya. Bono aye gose mbono gwacha komomanya. Omomura ori nagorete. (kwa msisitizo) Nagorete agaakana chiropi chionsi pi.</p> <p><b>Aba</b> tamenyeti aroro.</p> <p><b>Mikuro:</b> Mmmm. Igo mbuya. Onye ogorire mbuya; Tochaya monto tata.</p> | <p><b>Mikuro:</b> Acha uongo (Huku akicheka) huyo kijana hawezি kabisa kununua shamba.</p> <p><b>James:</b> Unasema nini sasa. mimi ndiye ninayemfahamu vizuri. Sasa si wewe ni juzi umeanza kumfahamu. Yule kijana alinunua. (kwa msisitizo) alinunua akalipa pesa zote. <b>Ingawa</b> haishi hapo.</p> <p><b>Mikuro:</b> Mmmm. Hivyo ni vizuri. Ikiwa amenunua ni vizuri; usidharau mtu bwana.</p> |

- a) Nagorete agaakana chiropi chionsi pi. /**Aba** tamenyeti aroro

Ni-a-gor-ete a-ga-akan-a chi-ropi chi-onsi pi. **Aba** ti-a-men-y-eti aroro

KIM-NFS3U-MZZ-K NFS3U-MZZ-IT NGL-MZZ MZZ **KUM** PING-NFS3U-MZZ-KTK MZZ

(Alinunua akalipa besa zote kabisa ingawa haishi huko)

**(Muktadha: Mazungumzo ya kijamii. Wazungumzaji wawili g na h wanazungumza kuhusu uhasama walio nao watu; wanaeleza jinsi paka alivyopewa sumu lakini haikumdhuru)**

| Kikisii  | Kiswahili  |
|--|--|
| <p><b>G:</b> Aye kira. Notaraikera abanto ababe.<br/>Ense eye n'enkongu</p> <p><b>H:</b> Nimanyete bo.</p> <p><b>G:</b> Nabo orabe komanyete otatiga tiga<br/>ngotebi abanto mbare orakage nga<br/>nabaya kwamanya gokumi<br/>amangana bakorire</p> <p><b>H:</b> Ninki gwatebera igo yaa</p> <p><b>G:</b> Noroche omongina ori basinyaine na<br/>Maritha?</p> <p><b>H:</b> Ee</p> <p><b>G:</b> Nomanyete nga omongina ori<br/>nomorogi omororo? Ori nomoiti pi.<br/>Nomanyete nga engaki nere<br/>angire nabanto pi? Nigo aimogete<br/>akagani goita omogaka oye. Agakemba<br/>akamobekera eriogo<br/>ase endagera.</p> <p><b>H:</b> Aa!</p> <p><b>G:</b> Ee! Ange omogaka oyu oye ari<br/>endagera eywo. Egesio ekiya, ekaba<br/>nga omwana nare konyora<br/>ororire. Omwana oyu nere ochiete<br/>gotebi omogaka ori. Nere akamanya<br/>koba omongaini. Akabwata akaa<br/>ekemoni endagera eri.<br/>Ekemoni ekyo gekari endagera eyu<br/>kegaku. (huku akimwashiria paka<br/>wake) Nomanyete nga nonya neke<br/>nkiariete esumo? Ekemoni eke nkiaetu<br/>esumo gekari <b>aba</b> manya nonya<br/>kiariete tigekweti</p> <p><b>H:</b> Amaene bono ogokwana nga</p> | <p><b>G:</b> Wewe Nyamaza. Ni kwa sababu hujafikia<br/>watu wabaya. Hii dunia ni ngumu.</p> <p><b>H:</b> Ninajua hivyo</p> <p><b>G:</b> Unaweza kuwa unajua lakini acha<br/>nikwambie kuna watu unaweza kufikiria<br/>kuwa ni wema kisha unashangazwa na<br/>mambo wamefanya</p> <p><b>H:</b> Mbona umesema hivyo <i>yaa?</i></p> <p><b>G:</b> Unaona yule mama jirani ya Marith?</p> <p><b>H:</b> Ee</p> <p><b>G:</b> Unajua yule mama ni mchawi mkubwa?<br/>Yule ni mwuaji kabisa. Unajua kuwa kuna<br/>wakati alikuwa amekataliwa na watu kabisa?<br/>Alitaka kumwua bwanake. Akamwekea dawa<br/>kwa chakula.</p> <p><b>H:</b> Aa!</p> <p><b>G:</b> Ee! Karibu mumewe ale hicho chakula . kwa<br/>bahati nzuri kulikuwa na mtoto aliye kuuwa<br/>ameona. Mtoto huyo ndiye alienda<br/>kumwambia bwana yule. Naye akawa<br/>mwerevu. Akampa oaka kile chakula. Huyo<br/>paka akala kile chakula akafa. (huku<br/>akimwashiria paka wake) unajua kuwa hata<br/>huyu wangu alikula sumu? Paka huyo<br/>alipewa sumu akala <b>ingawa</b> fahamu hata<br/>ingawa alikula hakufa</p> <p><b>H:</b> Ni ukweli unasema kuwa mama huyo<br/>alimwekea mumewe sumu!</p> |

|   |  |
|---|--|
| omongina oyu akabekera omogaka oye esumo! |  |
|---|--|

- b) Ekemoni eke nkiaetu esumo gekari */aba manya nonya kiariete tigekweti*  
 E-ke-moni e-ke n-ki-a-etu e-sumo ge-ka-ri **aba** manya nonya ki-a-ri-ete ti-ge-ku-eti.  
 NGL-NGL:IDU-MZZ NGL-NGL:IDU KIM-NGL-NJ-K NGL-MZZ **KUM** MZZ MZZ NGL-NJ-MZZ-K PING-NGL-MZZ-KTK  
 (Paka huyu alipewa sumu ingawa jua hata ingawa alikula hakufa)

Umbo ‘aba’ nalo ni umbo la **KUM** linalojitokeza kuwa asilia. Umbo hili halijawekewa viambishi vyovyote. Katika **MF5<sup>3a</sup>**, na **MF5<sup>3b</sup>** **KUM** ‘aba’ kimetumika ili kuleta mshikamano baina ya tungo mbili husika. Ni dhahiri vilevile kuwa umbo hili halijazuliwa kutoka kwa aina nydingine yoyote ya maneno kama vile nomino, vitenzi na kadhalika.

### Ani

#### **MF5<sup>4</sup>**

(Muktadha: Mazungumzo ya kijamii. *Wazungumzaji wawili James na Mikuro wanazungumza juu ya mwenzao aliyenunua shamba*)

| Kikisii   | Kiswahili   |
|---|---|
| <p><b>James:</b> Ori nomonto bwechogete</p> <p><b>Mikuro:</b> Aba nonya nigo nomokora are</p> <p><b>James:</b> Ee nomokora! Ndire ang'ainete bobe</p> <p><b>Mikuro:</b> (Kwa mshangao) Naki akongainete?</p> <p><b>James:</b> Igo ang'ainete nga abana baye noo bamenyete ase oboremo obu bwaye. Nkegena bo omogambi. Nkaba engaki entabe totanyakoumerana. Engaki eyemo enachiete nkanyora nga</p> | <p><b>James:</b> Yule ni mtu amejipanga</p> <p><b>Mikuro:</b> Ingawa hata hivyo ni mkora</p> <p><b>James:</b> Ndiyo ni mkora! Kuna wakati alinidanganya vibaya</p> <p><b>Mikuro:</b> (Kwa mshangao) alikudanganyaje?</p> <p><b>James:</b> Alinidanganya kuwa watoto wake wanaishi katika hilo shamba lake. Nikaamini hivyo mzee. Ikawa muda mrefu bila ya kukutana naye. Siku moja nilienda nikapata kuwa ni uongo kabisa; nilienda nikapata kumbe watoto hao wake hawaishi hapo.</p> |

|   |   |
|---|---|
| <p>noborimo pi; Enachiete nkanyora<br/>ani abana abu baye tibamenyeti oo</p> <p><b>Mikuro:</b> Oranyore natatagete omanye ase bamenyeti.</p> <p><b>James:</b> Ninki bono narenge kobakorera nimmanya ase bamenyeti.</p> | <p><b>Mikuro:</b> Unawe kupata hakutaka ujue mahali wanaishi</p> <p><b>James:</b> Sasa ningewafanyia nini hata ningejua wanakoishi.</p> |
|---|---|

a) Enachiete nkanyora /*ani abana abu baye tibamenyeti oo*

E-ni-a-chi-ete Ni-ka-nyor-a /*ani a-b-an a-bu ba-ye ti-ba-men-eti oo*

KIM-NFS1U-NJ-MAT KIM-SM-MZZ-IT **KUM** NGL-IDW-MZZ NGL-MZZ NGL:ID-MZZ KAN-IDW-MZZ-MAT MZZ  
(Nilienda nikapata kumbe watoto hao wake hawaishi huko)

**MF5<sup>4</sup>** ni mfano unaodhihirisha matumizi ya ‘**ani**’ kama **KUM**. **KUM** hiki vilevile kinajitokeza kuwa asilia kwa kuwa hakijawekewa viambishi vyovyote. **KUM** hiki kimetumika ili kufanikisha mshikamano baina ya tungo mbili husika. Katika **MF5<sup>4</sup> KUM** kimetumika katika kufanikisha mshikamano baina ya ‘Enachiete nkanyora’ (Nilienda nikapata) na ‘Abana abu baye tibamenyeti oo’ (Watoto hao wake hawaishi huko).

### Korende

**MF5<sup>5</sup>:**

(Muktadha: Mazungumzo ya kijamii. Wazungumzaji wawili G na H wanazungumza juu ya mwanamke fulani aliyeolewa na mwanamme ambaye si wa kabilia lake)

| Kikisii  | Kiswahili  |
|--|--|
| <p><b>G:</b> Aberi nigo abwatete akanywoma omokungu ekabira</p> <p><b>H:</b> Aa! Mokungu ori oye tari mogusii?</p> <p><b>G:</b> Yaya tari mogusii!</p> | <p><b>G:</b> Aberi alioa mwanamke wa kabilia linguine</p> <p><b>H:</b> Aa! Yule mkewe si mkisii?</p> <p><b>G:</b> Hapana si mkisii!</p> <p><b>H:</b> Hivyo ni wa kabilia linguine?</p> |

|   |  |
|---|--|
| <p><b>H:</b> Igo n'ekabira?</p> <p><b>G:</b> Nigo are omomaragori <b>korende</b><br/>akwane ekegusii tokomanya nga tari<br/>mogusii. Nigo arakwane<br/>nonya n'amangana amakongu<br/>y'ekegusii. Nonya n'echimbachero<br/>chionsi nachimanyete.</p> | <p><b>G:</b> Ni mmapragoli <b>lakini</b> akisema kikisii<br/>huwezi kujua kuwa si mkisii. Anaweza<br/>kusema hata maneno magumu ya kikisii.<br/>Hata methali yote anaifahamu</p> |
|---|--|

Nigo are omomaragori / **korende akwane ekegusii tokomanya nga tari mogusii**  
 Nigo a-r-e o-mo-maragori / **korende a-kwan-e e-kegusii ti-o-ko-many-a nga ti-a-r-i mo-gusii**  
 KIM NFS3U-MZZ-K KAT-IDU-MZZ **KUM** NFS3U-MZZ-K NGL-MZZ KAN-NFS2U-Kat-MZZ-IT KIM KAN-NJ-MZZ-IT IDU-MZZ  
 (Ni mmapragoli lakini akisema kikisii huwezi kujua kuwa si mkisii)

Katika **MF5<sup>5</sup>** kumetumika **KUM** ambacho ni ‘**korende**’. **KUM** hiki ni asilia na hakiambishiwi viambishi vyovyote. **KUM** hiki kimetumika katika kuweka pamoja vishazi viwili: ‘*nigo are omomaragori*’ (ye ye ni mmapragoli) na ‘*akwane ekegusii tokomanya gose tari mogusii*’ (akisema Kikisii huwezi kujua kuwa si mkisii). Ingawa katika sehemu hii **KUM ‘korende’** kimebainishwa kuwa **KUM** cha neno moja, **KUM** hiki kinabainika kuwa na maana sawa na **KUM ‘ko’** ambacho kimejadiliwa hapo awali katika 3.1.1. Hivyo ‘**ko**’ pamoja na ‘**korende**’ vinaweza kuchukuliwa kuwa ni alomofu za mofimu moja yenye maana ya ila au lakini.

### 3.1.2.2 VUM vinavyotokana na vitenzi

Utafiti huu ulibaini kuwa kuna VUM vinavyotokana na vitenzi. VUM hivi vilibainika kuwa na misingi iliyotokana na vitenzi. Aghalabu mizizi ya vitenzi huwa imewekewa viambishi ili kuunda VUM hivi. Baadhi ya mizizi ya vitenzi iliyowekewa viambishi ili kuunda VUM ni kama vile: ‘-many-’ (jua), ‘-bu-’ (shinda), ‘-ger-’ (sababisha), ‘-b-’ (kuwa), ‘-ik-’ (fika), ‘-nyor-’ (pata) na ‘-tig-’ (acha).

#### 3.1.2.2.1 VUM vinavyotokana na MZZ ya ‘–many-’ (jua)

##### Omanyete

###### MF6<sup>1</sup>:

(Muktadha: Mazungumzo ya kijamii. *g na h wanashiriki mazungumzo kuhusu uchawi*)

| Kikisii  | Kiswahili   |
|--|---|
| <p><b>G:</b> Ebinto ebyo nche nimbioboete</p> <p><b>H:</b> Nomanyste ng'a omotienyo o'ikomi na kabere bwo'mwaka ori babo Naomi mbachete koru abu Nyorobi. Omwana akagenda ekanisa agasiareru ebibiriri. <b>Omanyete</b> togasinyu naki tokomokora.</p> | <p><b>G:</b> Hivyo vitu mimi ninaviogopa</p> <p><b>H:</b> Unajua kuwa mwezi wa kumi na mbili mwaka jana akina Naomi walikuja kutoka Nairobi. Mtoto akaenda kanisani akamwagiwa uchawi wa macho. <b>Unajua</b> tukashindwa tutamfanyaje.</p> |

Omwana akagenda ekanisa agasiareru ebibiriri. / *Omanyete togasinyu naki tokomokora.*

O-mw-ana a-ka-gend-a e-kanisa a-ga-siar-er-u e-bibiriri. / *O-many-ete to-ga-siny-u naki to-ko-mo-kor-a.*

KAT-IDU-MZZ NFS3U-SM-MZZ-IT KAT-MZZ NFS3U-SM-MZZ-K-IT KAT-MZZ. **KUM**(NFS2U-MZZ-MAT) NFS1W-SM-K MZZ NFS1W-Kat-SH-MZZ-IT

(Mtoto akaenda kanisani akarushiwa uchawi wa macho unajua tukashindwa tutamfanyaje)

**MF6<sup>1</sup>** unadhihirisha mfano ambapo kumetumika **KUM** ambacho kimeundwa kutokana na mzizi *-many-* (jua). **KUM** hiki kimeambishiwa viambishi awali ‘**o-**’ na kiambishi tamati ‘**-ete**’. ‘**o-**’ kimetumika kudhihirisha NFS2U ilihali kiambishi ‘**-ete**’ kinadhihirisha matilaba. ‘*-many-*’ ni mzizi wa kitenzi ‘manya’ chenye maana ya ‘jua’ au ‘fahamu’. Matumizi ya **KUM** hiki kinachotokana na kitenzi yanafanikisha mshikamano katika tungo kilimotumika: ‘*Omwana akagenda ekanisa agasiareru ebibiriri*’ (Mtoto akaenda kanisani akarushiwa uchawi wa macho). Kishazi hiki kinashikamanishwa na kishazi ‘*togasinyu naki tokomokora*’ (Tukashindwa tutamfanyaje) kutokana na matumizi ya **KUM** ‘**omanyete**’ ambacho kimeundwa kutokana na mzizi wa kitenzi (-many-)

### 3.1.2.2.2 VUM vinavyotokana na MZZ ya **-bu-** (shinda)

#### Kobua

‘**Kobua**’ ni **KUM** ambacho kinatokana na mzizi wa kitenzi. Mzizi uliozua **KUM** hiki ni **-bu-** (shinda). Kiambishi awali tangulizi ‘**ko-**’ kimeambatishiwa mzizi **-bu-** na hivyo kuunda **KUM** chenye muundo wa kitenzi jina. Kutokana na mzizi **‘-bu-’**, **KUM** kinachojitokeza kinaashiria ulinganishi wa namna fulani:

#### **MF6<sup>2</sup>:**

(Muktadha: Mazungumzo ya kijamii. *Mzungumzaji J anawaeleza H na mtafiti kuhusu jinsi wazungu wanavyothamini watoto*)

| Kikisii  | Kiswahili  |
|--|--|
| <b>J:</b> Omosongo, gento tikeiyo akorenda buna omwana. Abaoroki ba abana babo igo bagoakanu chibesa chinyinge <b>kobua</b> bari bagosomi chisukuru chinene. | <b>J:</b> Mzungu, hakuna kitu analinda kama mtoto. Walimu wa watoto wao wanalipwa pesa nyingi <b>kuliko</b> wale wanaofundisha katika shule za juu |

Abaoroki ba abana babo igo bagoakanu chibesa chinyinge / **kobua bari bagosomi chisukuru chinene.**

A-ba-oroki ba a-b-ana ba-bo igo ba-go-akan-u chi-besa chi-nyinge / **ko-bua ba-ri ba-go-som-i chi-sukuru chi-nene.**

KAN-NGL-MZZ H NGL-IDW- MZZ NGL-MZZ KIM NGL:IDW-Kat-MZZ-K:IT IDW-MZZ IDW- MZZ NGL-MZZ  
**KUM(Kat-MZZ) IDW-MZZ IDW-Kat-MZZ-K:NJ NGL-MZZ NGL-MZZ**

(Walimu wa watoto wao wanalipwa pesa nyingi kuliko wale wanaofundisha katika shule za juu)

Katika **MF6<sup>2</sup>** **KUM** ‘**kobua**’ ambacho kimedhihirika kuwa na mofu mbili: **ko + bua**.

Dhana ya ulinganishi ambayo inadhirika katika tungo hii imetokana na dhana ya ‘**bua**’ (shinda) ambayo imejengeka katika **KUM** ‘**kobua**’. Ulinganishi unafanywa kati ya malipo wanayopewa walimu wa watoto na malipo wanayopewa wale wanaofundisha katika shule za juu; walimu wanaofundisha watoto wanalipwa pesa nyingi ikilinganishwa na wale wanaofundisha katika shule za juu.

### **3.1.2.2.3 VUM vinavyotokana na MZZ ya –ger- (sababisha)**

#### **Ekiagera**

Katika **MF6<sup>3</sup>** **KUM** ‘**ekiagera**’ kimetumika kufanikisha mshikamano katika tungo husika. **KUM** hiki kimeundwa kutokana na uambishwaji wa mofu katika mzizi **-ger-** unaotokana na kitenzi ‘**gera**’ (sababisha).

**MF6<sup>3</sup>:**

**(Muktadha: Darasani. *Mmoja wa wanafunzi anasimulia kisa cha kulaaniwa kwa nyoka*)**

| Kikisii  | Kiswahili  |
|--|--|
| Erio Omonene Nyasae akabea bobe mono<br>akaragereria engiti akanyetebia: Engiti eye aye, | Hivyo Mwenyezi Mungu akakasirika sana<br>akalaani nyoka akamwambia: Wewe nyoka |

|  |   |
|--|---|
| kwaragererigu. <b>Ekiagera</b> gwakorire aya, aye kwaragererigu kobua chingiti chionsi chigotugwa n'echingiti chionsi chiorosana | umelaaniwa. <b>Kwa kuwa</b> umefanya haya, wewe umelaaniwa kuliko wanyama wote wanaofugwa na wanyama wote wa mwituni. |
|--|---|

- a) *Ekiagera gwakorire aya / aye kwaragererigu kobua chingiti chionsi chigotugwa ne chingiti chionsi chiorosana*

**E-ki-a-ger-a gu-a-kor-ire a-ya / aye ku-a-ragereri-gu ko-bua chi-ngiti chi-onsi chi-go-tug-wa na e-chi-ngiti chi-onsi chi-o-rosana**

KUM(KIM-NGL-NJ-MZZ-IT) Kat:NFS2U-NJ-MZZ-K NGL-MZZ, W Kat:NFS2U-NJ-MZZ-K Kat-MZZ NGL-MZZ NGL-MZZ NGL-Kat-MZZ-K U KAT-NGL-MZZ NGL-MZZ NGL-KAT-MZZ

(Kwa kuwa umetenda haya, wewe umelaaniwa kuliko wanyama wote wanaofungwa na wa nyama wote wa mwituni)

**(Muktadha: Mazungumzo ya kijamii. F anamweleza G kuhusu ubaya wa sukari)**

| Kikisii   | Kiswahili  |
|---|--|
| <p><b>G:</b> Nga bono obo n'oburwaire bw'esukari?</p> <p><b>F:</b> Ee. Nabo bore igo</p> <p><b>G:</b> Aaa! N'obobe. Tibbwati riogo</p> <p><b>F:</b> Igo n'ogoteba nga totige konyu esukari?</p> <p><b>G:</b> Ee baba. Sukari teri ngiya <b>ekiagera</b> nigo eroseiri ebinto ebibe.</p> | <p><b>G:</b> Eti sasa huu ni ugonjwa wa sukari?</p> <p><b>F:</b> Ee. Uko hivyo</p> <p><b>G:</b> Aaa! Ni mbaya. Hauna dawa.</p> <p><b>F:</b> Hivyo ni kusema kuwa tuache kunywa sukari?</p> <p><b>G:</b> Ee <i>baba</i>. Sukari si nzuri <b>kwa kuwa</b> imetengenezewa vitu vibaya</p> |

- b) Sukari teri ngiya /*ekiagera nigo eroseiri ebinto ebibe*.

Sukari ti-er-i ng-iya **e-ki-a-ger-a** nigo e-ros-eiri e-bi-nto e-bi-be.

N KAN-MZZ-IT KAN NGL-MZZ **KUM**(KIM-NGL-NJ-MZZ-IT) KIM NGL-MZZ-K KAT-NGL-MZZ KAT-NGL-MZZ  
(Sukari sio nzuri kwa kuwa imetengenezewa vitu vibaya)

‘**ekiagera**’ kama ilivyotumika katika **MF6<sup>3</sup>a** na **MF6<sup>3</sup>b** ni **KUM** ambacho kimedhihirika kuwa na umbo la KIM-NGL-NJ-MZZ-IT. MZZ ‘-ger-’ kama ulivyotumika katika mifano hii ndio unaofanikisha kujengeka kwa dhana ya sababu kama inavyojitokeza katika tungo hii na hivyo kufanikisha mshikamano katika tungo hii.

### 3.1.2.2.4 VUM vinavyotokana na MZZ ya -b- (kuwa)

#### Okoba

KUM kingine ambacho kinadhihirika kuumbika kutokana na MZZ wa kitenzi ni ‘**okoba**’.

**MZZ** huo ni ‘-b-’ wenye maana ya kuwa:

**MF6<sup>4</sup>:**

(Muktadha: Mazungumzo ya kijamii. *G anamweleza H kuhusu ubaya wa sukari*)

| Kikisii  | Kiswahili   |
|--|---|
| <p><b>G:</b> Tinyigueti buya buna botambe. Igo naigu bobo okoba esukari yagenda igoro. Ngocha ere yambeka nse nonya nomokubi omogima.</p> <p><b>H:</b> Nakoir engora ekiababa. Tiga Nyasae agokonye.</p> | <p><b>G:</b> Sihisi vizuri kama kawaida. Nimehisi vibaya kwa kuwa sukari imeenda juu. Huwa inaniweka chini hata juma zima.</p> <p><b>H:</b> Nimekupa pole. Acha Mungu akusaidie</p> |

Igo naigu bobo /*okoba esukari yagenda igoro*.

Igo ni-a-igu bobo /*o-ko-ba e-sukari yi-a-gend-a igoro*.

KIM NFS1U-NJ-MZZ E **KUM** (KAT-Kat-MZZ) KAT-MZZ NGL-NJ-MZZ-IT E

(Nimehisi vibaya kwa kuwa sukari imeenda juu)

Katika **MF6<sup>4</sup>** Mzizi **-b-** wa kitenzi ‘**ba**’ (kuwa) umewekewa viambishi **o-** na **ko-** ili kutengeneza **KUM** ‘**okoba**’ ambayo inatekeleza jukumu la kuleta mshikamano katika tungo husika. Kama inavyodhihirika katika uchanganuzi wa **MF6<sup>4</sup>**, umbo la **KUM** ‘**okoba**’ linabainika kuwa lililoundwa kwa KAT-Kat-MZZ.

## **Neba**

Sawa na **KUM** *okoba* ambacho kimechananuliwa hapo juu katika **MF6<sup>4</sup>**, KUM ‘neba’ pia huwa na umbo lililotokana na MZZ. MZZ unaozua **KUM** hiki ni –b- na una maana ya kuwa:

### **MF6<sup>5</sup>:**

(Muktadha: *Mazungumzo ya kijamii. Wazungumzaji wawili James na Mikuro wanazungumza juu ya mwenzao aliyenunua shamba*)

| Kikisii   | Kiswahili   |
|---|---|
| <p><b>Mikuro:</b> Bono nabo abatebeti nga ogorire<br/>ase ari?</p> <p><b>James:</b> Ee! Igo nga tibwegeneti?</p> <p><b>Mikurio:</b> Aa! Tinyegeneti?</p> <p><b>James:</b> Nabo atotebeti boigo. <b>Neba</b><br/>taakaneti chionsi tari bobe.</p> <p><b>Mikuro:</b> E – e mbuya.</p> | <p><b>Mikuro:</b> Sasa aliwaambia kuwa<br/>amenunua mahali pale?</p> <p><b>James:</b> Ee! Hivyo hukuamini?</p> <p><b>Mikurio:</b> Aa! Tinyegeneti.</p> <p><b>James:</b> Ni hivyo alituambia hivyo. hata<br/>ikiwa hakulipa zote sio vibaya</p> <p><b>Mikuro:</b> E – e ni vizuri.</p> |

Nabo atotebeti boigo. / *Neba taakaneti chionsi tari bobe.*

Ni-a-bo a-to-teb-eti boigo. **Na-e-b-a** ti-a-akan-eti chi-onsi ti-a-ri bobe

KIM:NJ-MZZ NFS3U-NFS1W-MZZ-K E. **KUM(U-NGL-MZZ)** KAN-NF3U-MZZ-K NGL-MZZ KAN-NFS3U-MZZ E  
(Ni hivyo alituambia hivyo. hata ikiwa hakulipa zote sio vibaya)

Katika **MF6<sup>5</sup>** ‘neba’ imejitokeza kama **KUM**. Katika mfano huu inadhihirika kuwa **KUM ‘neba’** kimeundwa kwa kuambisha mofu ya uunganishaji **na-** pamoja na kiambishi awali –e- na kiambishi tamati –a kwenye mzizi –b- ambao ni mzizi wa kitensi *ba* chenye maana ya kuwa. KUM hiki kinadhihirika kuwa na muundo wa U-NGL-MZZ.

### 3.1.2.2.5 VUM vinavyotokana na MZZ ya -ik- (fika)

#### Goika

**KUM** ‘goika’ nacho kilidhihirika kuwa na umbo maalum. Ilibainika kuwa **KUM** hiki pia kilikuwa na MZZ uliotokana na kitenzi. Tazama **MF6<sup>6</sup>**.

#### **MF6<sup>6</sup>:**

(Muktadha: Mazungumzo ya kijamii. Wahusika wanajadiliana kuhusu nukuu fulani ya biblia)

| Kikisii   | Kiswahili  |
|---|--|
| <p><b>L:</b> Teba bono kemanyi. Ntu bande mmbosa.</p> <p><b>K:</b> Yaya getabu ekyo tikeri goteba igo ekenyamangana eke. Nigo kegoteba nga: Tinkonyu naende okwama kw'omosabibu <b>goika</b> engaki eria ndachiche naende</p> | <p><b>L:</b> Sema basi wewe mjuzi. Sisi wengine ni bure</p> <p><b>K:</b> Hapana hicho kitabu hakisemi hivyo. Kinasema kuwa: sitakunywa tena zao la mzabibu <b>hadi</b> wakati ule nitakuja tena.</p> |

Tinkonyu naende okwama kw'omosabibu / **goika engaki eria ndachiche naende**  
 Ti-n-ko-ny-u naende o-kw-ama kwa o-mo-sabibu/**go-ik-a** e-ngaki e-ria n-ra-chiche naende  
 KAN-NFS1U-Kat-MZZ-IT E KAT-Kat-MZZ H KAT-IDU-MZZ **KUM**(Kat-MZZ-IT) KAT-MZZ NGL-MZZ NFS1U-NJ-MZZ E  
 (Sitakunywa tena uzao wa mzabibu hadi wakati ule nitakuja tena)

Katika **MF6<sup>6</sup>** kumetumika **KUM** ‘goika’ ili kufanikisha mshikamano baina ya ‘Tinkonyu naende okwama kw'omosabibu (Sitakunywa tena uzao wa mzabibu) pamoja na ‘engaki eria ndachiche naende’ (wakati ule nitakuja tena). **KUM** hiki kimeundwa kutokana na MZZ ‘-ik-’ unaounda kitenzi *ika* chenye maana ya fika – kinaashiria wakati maalum. **KUM** hiki kimeundwa kwa kuambisha kiambishi awali **go-** ambacho ni Kat pamoja na kiambishi tamati **a** ambacho ni IT katika MZZ ‘-ik-’.

### 3.1.2.2.6 VUM vinavyotokana na MZZ ya -nyor- (pata)

#### Oranvore

MZZ -nyor- (pata) pia unaweza kuambishiwa kiambishi ili kuunda **KUM** kama inavyodhihirika hapa chini katika **MF6<sup>6</sup>**:

#### **MF6<sup>7</sup>:**

(Muktadha: **Mazungumzo ya kijamii. J na K wanashiriki mazungumzo huku wakiwa wanamngoja mwenzao ambaye amekawia. k anahoji kuwa huenda wanayemsubiri asije kwa kuwa amekawia**)

| Kikisii  | Kiswahili  |
|--|--|
| <p><b>J:</b> Chinsa echu chiachire mono. Gochi nkoira bogochi. Ntochetokore emeremo eye bori?</p> <p><b>K:</b> Tindochi tokonyekora</p> <p><b>J:</b> Igo tokogenda gose toramoganya ake?</p> <p><b>K:</b> Mokua onyoriru mono <b>oranyore</b> tari gocha. Omanyete nabo ankorete iga rinde nkamoganya nkaganyora naende nomokora omororo. Tari monto morachikane nga ngokora more gento nere aikerani.</p> | <p><b>J:</b> Hizi saa zimekwisha sana. Hata kunaelekea kuwa usiku. Tutafanya hii kazi kweli?</p> <p><b>K:</b> Sioni tukiifanya</p> <p><b>J:</b> Twende au tumsubiri kidogo?</p> <p><b>K:</b> Mokua amechelewa mno <b>huenda</b> haji. Unajua alinifanya hivi wakati fulani nikamsubiri nikachoka, tena ni mkora ajabu. Sio mtu mnaweza kuahidiana naye kuwa mnafanya kitu naye aafikie</p> |

- a) Mokua onyoriru mono /**oranyore** tari gocha

Mokua o-nyor-iru mono **o-ra-nyor-e** ti-a-r-i go-ch-a

N NFS3U-MZZ-K E **KUM**(KIM:NFS2U-NJ-MZZ-K) KAN-NFS3U-MZZ-ITKAN Kat-MZZ-IT

(Mokua amechelewa mno huenda haji)

‘oranyore’ ambayo imetumika kama **KUM** katika **MF6<sup>7</sup>** imeundwa kwa kuambisha viambishi awali ‘o-’ na ‘-ra-’ pamoja na kiambishi tamati ‘-e’ kwenye mzizi **-nyor-** amba ni mzizi wa kitenzi *nyora* chenye maana ya pata. **KUM oranyore** kinabainisha muundo wa KIM:NFS2U-NJ-MZZ-K.

### 3.1.2.2.7 VUM vinavyotokana na MZZ ya -tig- (acha)

#### Otatiga

‘Otatiga’ pia ni **KUM** ambacho kinadhihirika kutokana MZZ wa kitenzi. Mfano uliotolewa hapa chini katika **MF6<sup>7</sup>** unadhihirisha hali hii.

#### **MF6<sup>7</sup>:**

(Muktadha: *Mazungumzo ya kijamii. Wazungumzaji wawili L na M wanazungumza kuhusu mwenzao ambaye wanadai alienda kutafuta pesa lakini hakuzipata*)

| Kikisii  | Kiswahili   |
|--|---|
| <p><b>L:</b> Mbora ekeene nkeri nga momura ori tanyakogenda korigi besa chyaye?</p> <p><b>M:</b> Nachete agachi korigi chibesa <b>otatiga</b> besa echio tachinyoreti.</p> <p><b>L:</b> Mosuko nanyore. Gincha taku moyo</p> | <p><b>L:</b> Si ukweli ni kuwa kijana yule hajawahi kwenda kutafuta pesa zake?</p> <p><b>M:</b> Alienda kutafuta pesa lakini pesa hizo hakuzipata.</p> <p><b>L:</b> Siku moja atapata mradi tu asife moyo</p> |

- a) Nachete agachi korigi chibesa /**otatiga besa echio tachinyoreti**.

Ni-a-ch-ete a-ga-ch-i ko-rigi chi-besa **o-ti-a-tiga** besa e-chio ti-a-chi-nyor-eti.

KIM-NFS3U-MZZ-MAT NFS3U-SM-MZZ-IT Kat-MZZ NGL-MZZ **KUM**(KIM-KAN-NJ-MZZ-IT) N KAT-MZZ KAN-NFS3U-NGL-MZZ-K

(Alienda kutafuta pesa lakini pesa hizo hakuzipata)

**KUM ‘otatiga’** ambacho kimetumika katika **MF6<sup>7</sup>** kufanikisha mshikamano katika tungo husika: ‘*Nachete agachi korigi chibesa*’ (Alienda kutafuta pesa) na ‘*Besa echo tachinyoreti*’ (Pesa hizo hakuzipata). **KUM ‘otatiga’** kinabainika kuwa kilichoundwa kutokana na kuambisha viambishi awali **o-, -ti-** na **a** pamoja na kiambishi tamati **-a** kwenye mzizi **-tig-** amba ni mzizi wa kitenzi ‘*tiga*’ chenye maana ya acha. **KUM** hiki kina muundo wa KIM-KAN-NJ-MZZ-IT.

### 3.1.2.3 Vinavyotokana na kielezi

Utafiti huu uligundua kwamba kuna VUM ambavyo vinatokana na vielezi. VUM hivi vilidhihirika kuwa vilivyoundwa kutokana na mizizi ya vielezi. VUM vinavyotokana na vielezi vilibainika kuwa vya aina mbili kuu. Kuna vile vinavyoambishiwa viambishi na kuna vile ambavyo haviambishiwi viambishi vyovyyote.

#### 3.1.2.3.1 VUM vinavyotokana na vielezi na ambavyo vimewekewa viambishi

Katika matini semwa za Kikisii kulijitokeza VUM vinavyotokana na vielezi na ambavyo vimewekewa. Mifano ya VUM hivi ni pamoja na:

#### Obobe

**MF7<sup>1</sup>:**

(**Muktadha: Mazungumzo ya kijamii. Wazungumzaji wawili J na K wanazungumza kuhusu mtoto fulani ambaye anasumbuliwa na ugonjwa**)

| Kikisii   | Kiswahili  |
|---|--|
| <b>J:</b> Omwana ori bw'omasire bono naki akorokwa? | <b>J:</b> Yule mtoto wa Omasire huwa anaitwa nani?<br><b>K:</b> Sijui jina lake la Kikisii. La Kizungu ni Jhn. |

|   |  |
|---|--|
| <p><b>K:</b> Timanyeti rieta ryaye ry'ekegusii.<br/>Eriegesongo nigo akorokwa John</p> <p><b>L:</b> Omwana ori tata nabwate omoki ase amasomo!</p> <p><b>K:</b> John ngokora are omokia ase esukuru.<br/>Obobe, nigo akonya korwara</p> <p><b>L:</b> Nabo nkoiwu nga ngochara orwara...</p> | <p><b>L:</b> Yule mtoto bwana ana bidii katika masomo</p> <p><b>K:</b> John anafanya bidii shulenii ubaya anakuwakuwa mgonjwa</p> <p><b>L:</b> Huwa nasikia kuwa huwa anakuwa mgonjwa...</p> |
|---|--|

John ngokora are omokia ase esukuru. */Obobe, nigo akonya korwara*

John ni-go-kor-a a-re o-mokia ase e-sukuru. **Obobe**, nigo a-ko-nya ko-rwar-a

N KIM-Kat-MZZ-IT NFS3U-MZZ KAT-MZZ H KAT-MZZ. **KUM**(KAT-MZZ) KIM NFS3U-Kat-MZZ Kat-MZZ-IT

(John anafanya bidii shulenii ubaya anakuwakuwa mgonjwa)

**MF7<sup>1</sup>** unadhihirisha **KUM** ambacho inadhihirika kimejengeka kutokana na MZZ wa kielezi ‘bobe’ (vibaya). MZZ huu umeongezewa kiambishi awali tangulizi **o-** ili kuunda nomino ‘obobe’ (ubaya). Kutoakana na MZZ wa kielezi ‘bobe’, kumeundwa KUM ambacho kinawezesha mshikamano katika tungo husika. KUM hiki kina muundo wa KAT-MZZ.

### **VUM vya mzizi -many-**

MZZ ‘-many-’ pia umeweza kwa **KUM** kinachodhihirika kuwa kilichotokana na kielezi. ‘-many-’ hapa ni MZZ unaodhihirika kuwa na maana ya kisha/halafu. Maumbo ya **VUM** yanayojengeka kutokana na MZZ huu ni pamoja na ‘omanye’, ‘tomanye’, ‘omanya’. Dhana ‘kisha/ndipo’ ambayo inadhihirishwa kutokana na MZZ ‘-many-’ inaashiria kule kutokea kwa tendo baada ya lingine. Mifano **MF7<sup>2</sup>**, **MF7<sup>3</sup>** na **MF7<sup>4</sup>** inadhihirisha jinsi MZZ huu (‘-many-’) ulivyonumika kuunda VUM na kufanikisha mshikamano katika matini semwa za Kikisii.

## **Omanye**

**MF7<sup>2</sup>**

(Muktadha: Mazungumzo ya kijamii. *G na H wanashiriki mazungumzo kuhusu uchawi*)

| Kikisii  | Kiswahili  |
|--|--|
| <p><b>H:</b> Abanto bari n'ababe mono</p> <p><b>G:</b> Ase ki?</p> <p><b>H:</b> Ebagoziara ebibiriri</p> <p><b>G:</b> Ebibiriri! Gose nkoigu nga ngocha bire biarusigu?</p> <p><b>H:</b> Arari aa? Ngenchoki eye?</p> <p><b>G:</b> Ngocha bire biarusigu aye. Naende tari gosori! Igo ogotiga oborogi pi omanye gocha korusigu ebibiriri.</p> <p><b>H:</b> Waaaah! Tiga Nyasae akonye abanto baye!</p> | <p>H: Wale watu ni wabaya sana</p> <p>G: Kwa nini?</p> <p>H: Wanarusha uchawi wa macho</p> <p>G: Uchawi wa macho! Si ninasikia huwa unatolewa?</p> <p>H: Wapi? Vipi?</p> <p>G: Huwa unatolewa wewe. Tena si mchezo! Utaacha urogi kabisa ndipo uje kutolewa uchawi wa macho.</p> <p>H: Waaaah! Acha Mungu asaidie watu wake!</p> |

Igo ogotiga oborogi pi / *omanye gocha korusigu ebibiriri*.

Igo o-go-tig-a o-bo-rogi pi / *o-many-e go-ch-a ko-rusi-gu e-bibiriri*.

KIM NFS2U-Kat-MZZ-IT KAT-NGL-MZZ E **KUM**(NFS2U-MZZ-K) KAT-MZZ-IT KAT-MZZ-K NGL-MZZ

(Utaacha urogi kabisa ndipo uje kutolewa uchawi wa macho)

Katika **MF7<sup>2</sup>** kumetumika **KUM** ‘**omanye**’ ambacho kimetokana na kuambishwa kwa viambishi katika MZZ ‘-many-’. Umbo ‘**omanye**’ limetokana na kuambishwa kwa mofu ‘**o-**’ na ‘**-e**’ mwanzoni na mwishoni mwa mzizi ‘-many-’ katika usanjari huo. Mofu ‘-e’ imetumika katika **KUM** hiki ili kudhihirisha njeo ya wakati ujao katika hali simulizi. Matumizi ya **KUM** hiki yanafanikisha mshikamano katika tungo kilimotumika. Aidha matumizi yake yanaashiria hali kuwa kutendeka kwa kitendo kimoja kunategemea kutendeka au kutokea kwa kingine. Kwa mfano, katika **MF7<sup>2</sup>**, ili mhusika atolewe uchawi wa macho, ni lazima kwanza aache uchawi. Kama inavyodhahirika katika **MF7<sup>2</sup>**

**KUM ‘omanyé’** kinapotokea katika tungo, kinafuatwa na kitenzi *gocha* (kuja). Yamkini hili linafanyika ili kuweka wazi ile dhana ya uendelezwaji. Kwamba tukio husika litatendeka baada ya lingine la awali kukamilika. Muundo wa **KUM** hapa ni NFS2U-MZZ-K.

### **Omanyá**

KUM ‘omanya’ kama kilivytumika katika **MF7<sup>3</sup>** pia inabainika kimetokana na MZZ ‘-many-’

#### **MF7<sup>3</sup>:**

(**Muktadha: Mazungumzo ya kijamii. G na H wanashiriki mazungumzo kuhusu uchawi**)

| Kikisii  | Kiswahili  |
|--|--|
| <p><b>G:</b> Igo nga mongina oyu tarenge goika mwana ange?</p> <p><b>H:</b> (Huku akicheka) Otagotiga aye, gose igo arenge gokora amakumi. Igo nakamororire natebi omokungu agende abise omwana nyomba. Ekeru aikire egento kye ritangani akombori n’omwana. Omorigi nyomba <b>omanya</b> gontebi siari siari siari.</p> | <p><b>G:</b> Hivyo mama huyo hakuwa akimfika mtoto karibu?</p> <p><b>H:</b> (Huku akicheka) Acha wewe, si alikuwa akifanya maajabu. Nilikuwa nikimwona namwambia mwanamke aende akamfiche mtoto ndani ya nyumba. Wakati amefika kitu cha kwanza alikuwa ananiuliza ni mtoto. Anamtafuta ndani ya nyumba <b>kisha</b> ananiambia <i>siari siari siari</i></p> |

Omorigi nyomba /**omanya** gontebi siari siari siari.

O-mo-rig-i nyomba /**o-many-a** go-n-teb-i siari siari siari.

NGL-SH-MZZ-IT E **KUM**(NGL:NFS3U-MZZ-IT) Kat-NFS1U-MZZ-T E

(Anamtafuta ndani ya nyumba kisha ananiambia *siari siari siari*)

Katika **MF7<sup>3</sup>** **KUM** ‘omanya’ kimetumika ili kufanikisha mshikamano katika tungo husika. **KUM** hiki kimeundwa kutokana na mzizi ‘-many-‘ ambacho kinadhihirisha dhima ya kisha/ndipo. KUM hiki kimeambishiwa mofu ‘o-’ (awali) na ‘-a’ (tamati). Mofu ‘o-’ imetumika kuashiria NGL pamoja na NFS3U. Mofu tamati ‘-a’ imetumika ili kuzua njeo ya wakati ulipo hali endelesi. Aghalabu **KUM** hiki kinapotumika huwa kinafuatwa na Kat ambacho huweza kuwa ama ‘go-’ au ‘ko-’. Muundo wa KUM unaodhihirika hapa ni ule wa NGL:NFS3U-MZZ-IT.

### **Tomanye**

Mzizi ‘-many-‘ unaweza kuambishiwa kiambishi awali cha wingi ‘to-’ ikiwa kiima kinarejelea watendaji zaidi ya mmoja. Aidha, kiambishi tamati ‘e-’ huweza kuambishwa katika mzizi huu iwapo njeo ashiriwa ni ya wakati ujao katika hali simulizi. Hali hii inabainika katika **MF7<sup>4</sup>**.

### **MF7<sup>4</sup>:**

**(Muktadha: Mazungumzo ya kijamii. Wanakikundi cha maendeleo wanajadiliana kuhusu shughuli zao za kikundi mzungumzaji Janawashauri wenzake kuwa wamsubiri mwalimu wao wa kikukndi na kumuuliza ni kwa nini wao wasipewe ng’ombe)**

| Kikisii   | Kiswahili   |
|---|---|
| <p><b>J:</b>(Kwa hasira) nche narosire n’amangana<br/>ayu mokonya kombori. Omwarimu<br/>nere ogocha gocha tomanye komobori<br/>nga ebinto ebi gwatochorera igo tori<br/>gotoa ngombe? (kwa hasira) Intu igo<br/>torabwatane totebe nga intu neng’ombe<br/>toraegu</p> | <p><b>J:</b> (kwa hasira) mimi nimechoshwa na<br/>hayo maneno mnaniulizauliza.<br/>Mwalimu ndiye atakuja ndipo<br/>tumuulize kwamba vitu hivi<br/>umetuchagulia hutupi ngombe? (kwa<br/>hasira) sisi tutashikana tuseme kuwa<br/>sisi ni ng’ombe tuapewa.</p> |

Omwarimu nere ogocha gocha /**tomanye komobori nga ebinto ebi gwatochorera igo tori gotoa ngombe?**

O-mw-arimu ni-ere o-go-ch-a go-ch-a **to-many-e** ko-mo-bori nga e-bi-nto e-bi gu-a-to-chor-er-a igo ti-o-r-i go-to-a ngombe?

KAT-IDU-MZZ KIM-MZZ NGL-Kat-MZZ-IT Kat-MZZ-IT **KUM(NFS1W-MZZ-IT:K)** Kat-SH-MZZ E KAT-MZZ NFS2U-NJ-NFS1W-MZZ-K-IT KAN-NFS2U-MZZ-ITKAN KIM Kat-NFSU-IT N

(Mwalimu ndiye atakuja ndipo tumuulize kwamba vitu hivi umetuchagulia hutupi ngombe?)

**KUM ‘tomanye’** kilichotumika katika **MF7<sup>4</sup>** kimeundwa kutokana na kuambishwa kwa kiambishi awali **to-** na kiambishi tamati **e-** katika mzizi **–many-** . muundo wa KUM hapa ni NFS1W-MZZ-IT:K.

### **3.1.2.3.2 VUM vinavyotokana na vielezi na ambavyo havijawekewa viambishi**

Katika matini semwa za Kikisii kulidhihirika **VUM** ambavyo vimetokana na vielezi lakini havijaambishwa mofu zozote. VUM hivi vinaweza kuchukuliwa kuwa ni VUM asilia vinavyotokana na vielezi. VUM vyta aina hii vilivyojitokeza katika matini semwa za Kikisii ni kama vile *mono* (zaidi), *naende* (tena), *ekero* (wakati), *bono* (sasa), *erio* (wakati huo), *erinde* (ili) *na egere* (ili).

#### **Mono**

**MF8<sup>1</sup>:**

**(Muktadha: Mazungumzo ya kijamii. Wazungumzaji wawili J na K wanashiriki mazungumzo. Baadaye mtoto mdogo anaanza kulia karibu na walipo. j anakaripia kuwa mtoto huyo anapenda kulia bila sababu)**

| Kikisii   | Kiswahili   |
|---|---|
| <p><b>J:</b> Ee nabo nsinyire nga ninki Atari<br/>koimokerera igoro nere akore emeremo<br/>buna abanto bande!</p> <p><b>K:</b> Otagotiga aye! twachire komoira ngora<br/>(<i>mtoto anatokeza kutoka njiani akiwa analia</i>) Omwana<br/>oyu nigo anarete bobe. <b>Mono</b> nigo<br/>anchete korera bosa (<i>kwa sauti ya ukali</i>)<br/>Kira kiri agasiaka!</p> | <p>J: Ee ndiyo nashindwa mbona naye asisimame<br/>afanye kazi kama watu wengine</p> <p>K: Isipokuwa wewe! Tumejaribu kumpeleka<br/>polepole (<i>mtoto anatokeza kutoka njiani akiwa analia</i>) mtoto huyo amezoea vibaya.<br/>Zaidi anapenda kulia bure (<i>kwa sauti ya ukali</i>) Nyamaza kimya wewe kavulana.</p> |

Omwana oyu nigo anarete bobe. / **Mono** nigo anchete korera bosa

O-mw-ana o-yu nigo a-nar-ete bobe. **Mono** nigo a-nch-ete ko-rer-a bosa

KAT-IDU-MZZ NGL-MZZ KIM NFS3U-MZZ-MAT E. **KUM** KIM NFS3U-MZZ-MAT Kat-MZZ-IT E

(Mtoto huyo amezoea vibaya. Zaidi anapenda kulia bure)

Katika **MF8<sup>1</sup>** kumetumika **KUM ‘mono’** ili kuleta mshikamano. **KUM** hiki kinabainika kuwa kilichoundwa kutokana na kielezi ‘mono’ ambacho kinawakilisha dhana ya zaidi. **KUM** hiki hakijaambishiwa viambishi vyovoyote. **KUM** hiki kinabainika kuwa kinachowezesha mshikamano. Katika **MF8<sup>1</sup>** habari zaidi zimetolewa kuhusu tungo ya kwanza ambayo ni ‘*Omwana oyu nigo anarete bobe*’ (Mtoto huyo amezoea vibaya). Habari za ziada zilizotolewa ni kuwa mtoto anayerejelewa katika mfano huu anapenda kulia.

### **Naende**

**KUM** hiki ambacho kinatokana na kielezi pia ni asilia kwa kuwa hakiwekewi viambishi. Matumizi ya **KUM** hiki yalidhihirika katika matini semwa za Kikisii kama inavyojitokeza hapa chini katika **MF8<sup>2</sup>**.

## MF8<sup>2</sup>:

(Muktadha: Mazungumzo ya kijamii. Wazungumzaji wawili L na M wanashiriki mazungumzo. Anaingia mama fulani (P) ambaye anamundai L fedha kwa ukali mama huyo anamfokea L na kudai kuwa hatarudi tena kuomba fedha hizo)

| Kikisii   | Kiswahili   |
|---|---|
| <p><b>L:</b> Naki bono omosubati? Karibu!</p> <p><b>P:</b> Nche tinganeti mangana mange n'ebesa yane nacha!</p> <p><b>L:</b> Gaki baba bono iga timbwati, naende nibwate abageni. Tikwarenge gwancha oche mambi?</p> <p><b>P:</b> Aye tegerera. Nagosabire chibesa chiane ange omwaka omogima. (<i>kwa ghadhabu</i>) Natigire gocha igaa. <b>Naende</b> tingokora imocha ryogotoma mwana one igaa</p> | <p><b>L:</b> Jambo dada? Karibu!</p> <p><b>P:</b> Mimi sitaki mambo mengi nimekuja kwa pesa zangu!</p> <p><b>L:</b> Haki dada saa hizi sina, tena nina wageni. Si ungependa uje kesho?</p> <p><b>P:</b> We sikiza. Nimekuomba pesa zangu karibia mwaka mzima. (<i>kwa ghadhabu</i>) Nimeacha kuja hapa. Tena, sitafanya kosa la kutuma mtoto wangu hapa</p> |

Natigire gocha igaa. /**Naende** tingokora imocha ryogotoma mwana one igaa  
 N-a-tig-ire go-ch-a igaa. **Naende** ti-n-go-kor-a i-mocha ria o-go-tom-a mw-ana o-ne igaa  
 NFS1U-NJ-MZZ-K Kat-MZZ-IT E. **KUM** KAN-NFS1U-Kat-MZZ-IT IDU-MZZ H KAT-Kat-MZZ-IT IDU-MZZ NGL-MZZ E  
 (Nimeacha kuja hapa. Tena, sitafanya kosa la kutuma mtoto wangu hapa)

**KUM ‘naende’** kama kilivytumika katka **MF8<sup>2</sup>** kimetumika kufanikisha mshikamano baina ya ‘*Natigire gocha igaa*’ (Nimeacha kuja hapa) na ‘*Tingokora imocha ryogotoma mwana one igaa*’ (Sitafanya kosa la kutuma mtoto wangu hapa). Inaelekea kuwa tungo ya pili ni maelezo zaidi yanayoshereheshea tungo ya kwanza kuwa kando na hali kuwa mse maji ameacha kwenda kwa msikilizaji, pia hatafanya kosa la kumtuma mtoto wake huko. Ni dhahiri kuwa **KUM ‘naende’** ni kielezi asilia kwa kuwa hakijaambishiwa kiambishi chochote.

## **Ekero**

Katika **MF8<sup>3</sup>** kumejitokeza matumizi ya KUM ‘ekero’. KUM hiki kinajitokeza kuwa asilia kwa kuwa hakijafungamanishwa kiambishi chochote.

### **MF8<sup>3</sup>:**

(Muktadha: Mazungumzo ya kijamii. *G na H wanashiriki mazungumzo kuhusu uchawi*)

| Kikisii   | Kiswahili  |
|---|--|
| <p><b>G:</b> Amangana ayu ogokwana nayekeene bono?</p> <p><b>H:</b> Aye kaga nga negosori. Gose nigo baeberereti omwana oyu. Bakamongaina nere agancha.</p> <p><b>G:</b> Agancha kogenda nabu?</p> <p><b>H:</b> Omwana oyu agancha agende na abanto abu. <b>Ekero</b> agenda, bagaika nchera bakamokorera bobe mono</p> | <p><b>G:</b> Hayo maneno unasema ni ya kweli?</p> <p><b>H:</b> Wewe fikiri ni mchezo. Si walibembeleza huyo mtoto. Wakamdaganya naye akakubali.</p> <p><b>G:</b> Akakubali kwenda nao?</p> <p><b>H:</b> Mtoto huyo akakubali aende na watu hao. <b>Wakati</b> alienda, wakafika njiani wakamtendea vibaya sana</p> |

Omwana oyu agancha agende na abanto abu. / *Ekero agenda, bagaika nchera bakamokorera bobe mono*

O-mw-ana o-yu a-ga-nch-a a-gend-e na a-ba-nto a-bu. **Ekero** a-gend-a, ba-ga-ik-a nchera ba-ka-mo-kor-er-a bobe mono

KAT-IDU-MZZ NGL-MZZ NFS3U-SM-MZZ-IT NFS3U-MZZ-K U NGL-IDW-MZZ NGL-MZZ. **KUM** NFS3U-MZZ-IT, IDW-SM-MZZ-IT E IDW-SM-SH-MZZ-K-IT E E

(Mtoto huyo akakubali aende na watu hao. Wakati alienda, wakafika njiani wakamtendea vibaya sana)

KUM ekero kama kilivyotumika katika **MF8<sup>3</sup>** kinafanikisha mshikamano baina ya vishazi viwili: *Omwana oyu agancha agende na abanto abu* (Mtoto huyo akakubali aende na watu hao) na *bagaika nchera bakamokorera bobe mono* (wakafika njiani wakamtendea vibaya sana). Ingawa KUM ‘ekero’ kimetumika katika **MF8<sup>3</sup>** kufanikisha mshikamano, KUM hiki ni lazima kiambatanishwe na KT. Katika **MF8<sup>3</sup>** kimeambatishwa KT ‘agenda’ (alienda).

## **Bono**

### **MF8<sup>4</sup>:**

**(Muktadha: Darasani. *Mwanafunzi mmoja anasimulia hadithi*)**

| Kikisii   | Kiswahili   |
|---|---|
| Omosomba oyu omwegenu akamanya gosuka gochi ange n'omogambi. Akaringa egoti yaye. <b>Bono</b> akamanya gotebia omogambi nga otarendeti nkouru ore obogambi bwao. Renda mono ekiagera batianire..... | Mtumwa huyo mwaminifu akasogelea karibu na mtawala. Akakunja koti yake. <b>Sasa</b> akamwambia mtawala kwamba usipochunga utanyanganywa mamlaka yako. Chunga sana kwa kuwa wameapa..... |

Akaringa egoti yaye. */Bono akamanya gotebia omogambi nga otarendeti nkouru ore obogambi bwao*

A-ka-ring-a e-goti y-aye. **Bono** a-ka-many-a go-teb-i-a o-mo-gambi nga o-ti-a-rend-eti ni-ko-ur-u o-re o-bo-gambi bw-ao

NFS3U-SM-MZZ-IT KAT-MZZ NGL-NFS3U:E. **KUM** NFS3U-SM-MZZ-IT Kat-MZZ-K-IT KAT-IDU-MZZ U NFS2U-KAN-NFS3U-MZZ-K KIM-Kat-MZZ-IT NGL-MZZ KAT-NGL-MZZ NGL-MZZ

(Akakunja koti yake. Sasa akamwambia mtawala kwamba usipochunga utanyanganywa mamlaka yako)

Katika **MF8<sup>4</sup>** **KUM** ‘bono’ kimetumika katika kuwezesha mshikamano katika tungo husika. **KUM** hiki kimsingi hutekeleza jukumu la kielezi. Hata hivyo katika **MF8<sup>4</sup>** kimetumika kama **KUM**. Katika mfano huu, KUM hiki ni cha asilia kwa kuwa hakijaambishiwa viambishi vyovoyote.

## Erio

### **MF8<sup>5</sup>:**

(Muktadha: Darasani. *Mwanafunzi mmoja anasimulia hadithi kuhusu mtoto fulani ambaye mjomba wake alikataa kumlipia karo*)

| Kikisii  | Kiswahili  |
|--|--|
| ‘...omwana ori akagenda ase isemoke komosaba amokonye ebesa achiere esukuru. Nomanyete isemoke oyu akanga pi komokonya! Akamokani nga tabwati besa aramoakanere sukuru. <b>Erio</b> manya nigo abwate chibesa akoa abanto babande bosa.’ | ‘.....Mtoto yule akaenda kwa mjomba wake kumwomba fedha aendee shule. Unajua mjomba wake huyo alikataa kabisa kumsaidia! Akamkataza kuwa hana pesa anazoweza kumlipia shulen. <b>Hivyo</b> jua ana pesa anazowapa watu wa wenyewe bure.’ |

Akamokani nga tabwati besa aramoakanere sukuru. */Erio manya nigo abwate chibesa akoa abanto babande bosa.*

A-ka-mo-kan-i nga ti-a-bwa-ti besa a-ra-mo-akan-ere sukuru. **Erio** many-a nigo a-bwa-te chi-besa a-ko a-ba-nto ba-band bosa.

NFS3U-SM-SH-MZZ-IT U KAN-NFS3U-MZZ-KTK N NFS3U-NJ-SH-MZZ-K N. **KUM** MZZ-IT KIM NFS3U-MZZ-MAT NGL-MZZ NFS3U-MZZ NFS3U-IDW-MZZ H-MZZ E

(Akamkataza kwamba hana pesa anazoweza kumlipia shulen. Hivyo jua ana pesa anazowapa watu wa wenyewe bure)

Katika MF8<sup>5</sup> **KUM** ‘erio’ kimetumika. **KUM** hiki kiasilia huwa ni kielezi lakini katika mfano huu ‘erio’ imetumika kama **KUM. KUM** hiki huwa hakiwekewi viambishi.

## Erinde

### **MF8<sup>6</sup>:**

(Muktadha: Mazungumzo ya kijamii. *wasailiwa L na M wanajadiliana kuhusu tabia za wanafunzi wa Yesu*)

| Kikisii                            | Kiswahili                                       |
|------------------------------------|---|
| <b>M:</b> Bono aye orache mbarenge | <b>M:</b> Sasa wewe unaona walikuwa na imani ya |

|   |  |
|---|--|
| nobwegenu boisaine?<br><b>L:</b> Arariaa! Noinyorete bagotebi Yeso<br>nga: Kae abanto aba ribaga, erinde<br>bagende emechie na ebichie aria na<br>aaria, begorere endagera? Igo<br>mbwegenu ki babwate .... | kutosha?<br><b>L:</b> Wapi! Unakumbuka wakimwambia Yesu<br>kuwa: wape watu hawa nafasi ili waende<br>kwenye miji na vijiji huko na kule,<br>wajinunulie chakula? Hivyo ni imani gani<br>waliyokuwa nayo..... |
|---|--|

Kae abanto aba ribaga, */erinde bagende emechie na ebichie aria na aaria, begorere endagera*

Kae a-ba-nto a-ba ri-baga, **erinde** ba-gend-e e-me-chie na e-bi-chie aria na aaria, ba-e-gor-ere e-ndagera

T NGL-IDW-MZZ NGL-IDW NGL-MZZ **KUM** IDW-MZZ-K KAT-IDW-MZZ U KAT-IDW-MZZ U W, IDW-NFS3W-MZZ-K KAT-MZZ

(Wape watu hawa nafasi ili waende kwenye miji na vijiji huko na kule, wajinunulie chakula)

Sawa na kilivyo **KUM** ‘*erio*’ katika **MF8<sup>5</sup>**, katika **MF8<sup>6</sup>** ‘*erinde*’ imetumika kama **KUM**. **KUM** hiki kiasilia ni kielezi. Aidha, **KUM** hiki hakijawekewa viambishi vyovoyote na hivyo kinaweza kuchukuliwa kuwa ni **KUM** asilia kinachotokana na kielezi.

## Egere

**MF8<sup>7</sup>:**

**(Muktadha: Mazungumzo ya kijamii. F anamweleza G kuhusu ubaya wa sukari))**

| Kikisii   | Kiswahili  |
|---|--|
| <b>F:</b> Gwateba nga esukari nembe?  | <b>F:</b> Umesema kuwa sukari ni mbaya?                                  |
| <b>G:</b> Teri mbe yaya   | <b>G:</b> Hapana si mbaya  |
| <b>F:</b> Igo ngaki rende!  | <b>F:</b> Vipi hivyo sasa!   |
| <b>G:</b> Nigo otakeire okeie esukari koru<br>omobere <b>egere</b> toigu bobe | <b>G:</b> Unatakiwa upunguze sukari kutoka mwilini<br>ili usihisi vibaya |
| <b>F:</b> Igo omonto nabo akonyu otatiga<br>taetani ekerengo.                 | <b>F:</b> Hivyo mtu anaweza kunywa ila asipitishe<br>kipimo              |
| <b>G:</b> Eee.  | <b>G:</b> Eee  |

Nigo otakeire okeie esukari koru omobere /**egere** toigu bobe

Nigo o-tak-eire o-keie e-sukari koru o-mo-bere **egere** ti-o-igu bobe

KIM NFS2U-MZZ-K NFS2U-MZZ KAT-MZZ H KAT-IDU-MZZ **KUM** KAN-NFS2U-MZZ E

(Unatakiwa upunguze sukari kutoka kwa mwili ili usihisi vibaya)

**MF8<sup>7</sup>** unadhihirisha matumizi ya **KUM** ‘**egere**’ ili kufanikisha mshikamano katika matin semwa za Kikisii. **KUM** hiki kiasilia ni kielezi. Katika **MF8<sup>7</sup>** kimebainika kuwa **KUM** asilia kinachotokana na kielezi. Hii inatoakana na sababu kuwa hakijawekewa viambishi awali wala tamati.

### Igo

**MF8<sup>8</sup>:**

(Muktadha: Mazungumzo ya kijamii. *Wanakikundi cha maendeleo wanashiriki mazungumzo.*

*Mmoja wao anamweleza mwenyekiti kuwa mwenzao haji kwa kuwa hakupata pesa)*

| Kikisii   | Kiswahili  |
|---|--|
| <b>Mwanachama:</b> Nche nabo nabakani amangana<br>ay a y'okobetereri abanto koru<br>chiropi. Momanyi tanyoreti<br>besa igo tari gocha. Naende<br>motarendeti eke n'egento kerabe<br>kegokorekana kera engaki.<br>Abanto mbabe bakwanga gocha<br>emesangererekano. | <b>Mwanachama:</b> Mimi niliwakataza haya<br>maneno ya kulazimisha watu<br>kutoa pesa. Momanyi hakupata<br>pesa hivyo haji. Tena<br>msipochunga hiki ni kitu<br>kitakuwa kikitokea kila wakati.<br>Watu watakuwa wakikataa kuja<br>kwa mikutano. |

Momanyi tanyoreti besa /**igo** tari gocha

Momanyi ti-a-nyor-eti besa **igo** ti-a-ri go-ch-a

N KAN-NFSU-MZZ-K N **KUM** KAN-NFS3U-MZZ Kat-MZZ-IT

(Momanyi hakupata pesa hivyo haji)

‘**Igo**’ katika **MF8<sup>8</sup>** imetumika kama **KUM**. Kimetumika katika **MF8<sup>8</sup>** ili kufanikisha mshikamano baina ya ‘*Momanyi tanyoreti besa*’ (Momanyi hakupata pesa) na ‘*Tari gocha*’

(haji). Kiasilia, **KUM ‘igo’** huwa ni kielezi. **KUM** hiki hakijaambishwa viambishi vyovoyote na kwa sababu hiyo kinachukuliwa kuwa ni **KUM** kinachotokana na kielezi na ambacho hakiwekewi viambishi.

Kinachodhihirika ni kuwa VUM vinavyotokana na vielezi *mono, naende, ekero, bono, erio, erinde na egere* aghalabu hujitokeza katika tungo ambazo ni za kimasimulizi; zinasimulia au kuelezea kisa au tukio fulani.

### **3.1.3 VUM vilivyo na muundo wa Kirai**

Utafiti huu ulibaini kuwa VUM katika matini semwa za Kikisii huweza kujitokeza vikiwa na muundo wa virai. Mathalani KH, KE au hata KT

#### **3.1.3.1 VUM vinavyotokana na Kundi Husishi**

VUM vilivyo na kundi husishi (KH) huwa na muundo wa H+KN. Mifano ya VUM hivi iliyojitokeza katika matini semwa za Kikisii ni pamoja na:

#### **Ase engencho**

##### **MF9<sup>1</sup>:**

**(Muktadha: Mazungumzo ya kijamii. G na H wanashiriki mazungumzo kuhusu mama fulani jirani wao ambaye alienda safari na akaacha watoto wachanga peke yao.)**

| Kikisii  | Kiswahili  |
|--|--|
| <p><b>H:</b> Nche nasinyiru n'amanga aye.<br/>Atakanegeka!</p> <p><b>G:</b> Nomanyete ekero airanete nigo<br/>namoteberereti gosori etaiyo.<br/>Nkamotebi: Aye saba Nyasae<br/>mono as'engencho konyora momura</p> | <p><b>H:</b> Mimi nimeshindwa na maneno yake.<br/>Hakataziki!</p> <p><b>G:</b> Unajua wakati alirudi nilimsomea bila<br/>mchezo. Nikamwambia: Wewe shukuru<br/>Mungu sana kwa sababu ndugu yangu<br/>alikuwa anataka kwenda kukushtaki ushikwe</p> |

|   |  |
|---|--|
| <p>ominto oimokire achi kogosoera obwatu osibu. Baba, akaondoka koru erio nabo ndoche nga orairire magoro make.</p> | <p>ufungwe. Dada, aliogopa tangu wakati huo naona amepoa kidogo.</p> |
|---|--|

Aye saba Nyasae mono **/as'engencho konyora momura ominto oimokire achi kogosoera obwatu osibu.**

Aye saba Nyasae mono **ase e-ngencho** ko-nyor-a mo-mura o-minto o-imok-ire a-chi ko-go-soer-a o-bwat-u o-sibu.

N T N E **KUM(H-KN(N(GL-MZZ)** Kat-MZZ-IT IDU-MZZ NGL-MZZ NGL-MZZ-K NFS3U-MZZ Kat-NFS2U-MZZ-IT NFS2U-MZZ-IT NFS2U-MZZ

(Wewe shukuru Mungu sana kwa sababu ndugu yangu alikuwa anataka kwenda kukushtaki ushikwe ufungwe)

Katika **MF9<sup>1</sup>**, ‘ase engecho’ imetumika kama **KUM. KUM** hiki kimeundwa kutokana na vipashio viwili ambavyo ni ‘ase’ ambacho ni kihuishi na ‘eng’enko’ ambacho ni nomino. **KUM** hiki kimetuika kufanikisha mshikamano katika tungo husika. Muundo wa KUM unaojitokeza hapa ni H-KN(N(GL-MZZ).

### **Ribaga ria**

**MF9<sup>2</sup>:**

(Muktadha: Mazungumzo ya kijamii. *L anamkashifu M kwa kwenda kumsema kwa watu wengine*)

| Kikisii   | Kiswahili  |
|---|--|
| <p><b>M:</b> Igo igo ogoteba nga mbobe nagokererete? Pole!</p> <p><b>L:</b> Ee! mbobe gwankorerete. Onye kwarorire nakorire bobe togontebi? Mbuya oche ontobi nche bweka ribaga ria kogenda gotebi abanto batagokonye. Bono ekero</p> | <p><b>M:</b> Hivyo huko ni kusema kuwa nilikufanya vibaya? Pole!</p> <p><b>L:</b> Ee! Ulinifanya vibaya. Ikiwaumeona nimefanya vibaya mbona usiniambie? Ni vizuri uje uniambie mimi peke yangu badala ya kwenda kuambia watu ambao hawatakusaidia. Sasa wakati umewakimbizia</p> |

|   |  |
|---|--|
| <p>kwabaminyokeri amangana ninki<br/>bagokonya?<br/><b>M:</b> Naigure bono. Tiga aywo aerere abu.</p> | <p>maneno wamekusaidia nini?<br/><b>M:</b> Nimesikia basi. Acha hayo yaishie hapo.</p> |
|---|--|

Mbuya oche ontebi nche bweka */ribaga ria kogenda gotebi abanto batagokonye.*

M-buya o-ch-e o-n-teb-i nche bw-eka **ri-baga ri-a** ko-gend-a go-teb-i a-ba-nto ba-ti-a-go-kony-e.

KIM-MZZ NFS2U-MZZ-K NFS2U-SH-MZZ-K W IDU-MZZ **KUM**(NGL-MZZ NGL-H) Kat-MZZ-IT Kat-MZZ-IT NGL-IDW-MZZ IDW-KAN-NJ-Kat-MZZ-K

(Ni vizuri uje uniambie mimi peke yangu badala ya kwenda kuambia watu ambao hawatakusaidia)

Katika **MF9<sup>2</sup>**, **KUM ‘ribaga ria’** kimetumika kufanikisha mshikamano. Mshikamano unaodhihirika hapa ni baina ya vishazi: *Mbuya oche ontebi nche bweka* (Ni vizuri uje uniambie mimi peke yangu) na *kogenda gotebi abanto batagokonye* (kwenda kuambia watu ambao hawatakusaidia). **KUM** hiki kiasilia ni kihuishi chenye maana ya ‘badala ya’.

### Ase obwenge

**MF9<sup>3</sup>:**

**(Muktadha: Mazungumzo ya kijamii. Wanakindi cha maendeleo wanahimizana kuhusu yale wanayotakiwa kufanya ili kikundi chao kipate ufanisi)**

| Kikisii   | Kiswahili  |
|---|--|
| <p><b>Mwanakikundi:</b> Ninki moroche omonto omonene aranya gotochandera. Chingaki chionsi nga nere torengerereti. Morora buya ekeombe keri giatu tikegu. Timonya gotokorera ebinto bitari na ngencho. Ase obwenge, tiga obochai. Gaki ancha motige egosori pi.</p> | <p><b>Mwanakikundi:</b> Ni nini mnaona mtu mkubwa anaweza kututesea. Nyakati zote eti ni yeye tunafikiria. Chungeni kile chama chetu kisisambaratike. Msive mkitufanyia vitu visivyo na maana. Kwa ufupi acha madharau. Tafadhali acheni mchezo kabisa</p> |

Timonya gotokorera ebinto bitari na ngencho. */Ase obwenge, tiga obochai*  
 Ti-mo-nya go-to-kor-era e-bi-nto bi-ti-a-r-i na e-ngencho. **Ase obwenge**, tig-a o-bo-chai  
 KAN-IDW-NJ KAT-IDW-MZZ-K KAT-IDW-MZZ IDW-KAN-NJ-MZZ-K U KAT-MZZ. **KUM(H-N) MZZ-IT KAT-NGL-MZZ**  
 (Msiwe mkitufanyia vitu visivyo na maana. Kwa ufupi acha madharau)

‘**Ase obwenge**’ ambayo imetumika kama **KUM** katika **MF9<sup>3</sup>** inabainika kuwa iliyoundwa kutokana na H ‘ase’ chenye maana ya kwa pamoja na N ‘obwenge’ yenyе maana ya ufupi. Matumizi ya KUM katika **MF9<sup>3</sup>** yanafanikisha mshikamano baina ya vishazi viwili ambavyo ni: *Timonya gotokorera ebinto bitari na ngencho* (Msiwe mkitufanyia vitu visivyo na maana) na *Tiga obochai* (Acha madharau).

### **Ase igo**

#### **MF9<sup>4</sup>:**

(**Muktadha: Mazungumzo ya kijamii. Mtafiti anashiriki mazungumzo na rafiki zake kuhusu mavazi. Mzungumzaji mmoja anaeleza kuwa aina za mavazi hubadilikabadilka kulinagana na mazingira anamojikuta mtu**)

| Kikisii  | Kiswahili  |
|--|--|
| <p><b>P:</b> Onye intu toigwete obokendu iga ngaki gose abanto banyete ngumbu bamenyete!</p> <p><b>Q:</b> Ninki! Okagete igo omonto orasinyu komenza ande onsi? Chinse chiri chya ngumbu igo chibwate obokendu obonge. Ase igo chianga nchireo abanto bakobeka egere chibatange embeo.</p> | <p><b>P:</b> Ikiwa sisi tunahisi baridi hivi je watu ambao wanaishi ngambo wanaishi vipi!</p> <p><b>Q:</b> Ni nini! Unafikiri mtu utashindwa kuishi popote? Nchi zile za ngambo zina baridi nyingi. Kwa hivyo nguo zipo watu hucaa ili ziwazuie baridi</p> |

Chinse chiri chya ngumbu igo chibwate obokendu obonge. /*Ase igo chianga nchireo abanto bakobeka egere chibatange embeo.*

Chi-nse chi-ri chi-a ngumbu igo chi-bwat-e o-bokendu o-bonge. **Ase igo** chi-anga n-chi-re-o a-ba-nto ba-ko-beka egere chi-ba-tang-e embeo.

NGL-MZZ NGL-MZZ NGL-MZZ N KIM NGL-MZZ-K KAT-MZZ NGL-MZZ. **KUM(H-W)** NGL-MZZ-KAN-NGL-MZZ-W NGL-IDW-MZZ IDW-Kat-MZZ U NGL-IDW-MZZ-K N

(Nchi zile za ngambo zina baridi nyingi. Kwa hivyo nguo zipo watu huva ili ziwazuie baridi)

Katika **MF9<sup>4</sup>**, ‘ase igo’ imetumika kama **KUM**. **KUM** hiki kimeundwa kutokana kuweka pamoja kihuishi ‘ase’ chenye maana ya kwa, pamoja na kiwakilishi ‘igo’ chenye maana ya hivyo. Muundo wa KUM unaodhihirika ni ule wa H+KN.

### **Magega yayu**

**MF9<sup>5</sup>:**

(Muktadha: *Mazungumzo ya kijamii. wazungumzaji G na H wanazungumza kuhusu mama fulani ambaye alikuwa mlevi wa kupindukia*)

| Kikisii  | Kiswahili   |
|--|---|
| <p><b>G:</b> N’amaene bono ogokwana? Omongina ori tarikororekana gose nabwate mangana.</p> <p><b>H:</b> Omongina ori nigo atoreka. Magega yayu nigo arenge konyu amaru amange mono. Tiga arakanyeka konyora oetaniri ekerengo.</p> | <p><b>G:</b> Unasema ukweli? Mama yule haonekani kuwa na maneno.</p> <p><b>H:</b> Mama Yule aliokoka. Kabla ya hapo alikuwa anakunywa pombe nyingi mno. Acha apoe alikuwa amezidi</p> |

Omongina ori nigo atoreka. /*Magega yayu nigo arenge konyu amaru amange mono.*

O-mo-ngina o-ri nigo a-torek-a. **Magega yayu** nigo a-renge ko-nyu amaru a-mange mono.

KAT-IDU-MZZ NGL-MZZ KIM NFS3U:NJ-MZZ-IT. **KUM(H-W)** KIM NFS3U-MZZ Kat-MZZ N NGL-MZZ V

(Mama Yule aliokoka. Kabla ya hapo alikuwa anakunywa pombe nyingi mno)

Katika **MF9<sup>5</sup>** kumetumika **KUM** ‘magega yayu’. KUM hiki kimeundwa kutokana na kuunganishwa kwa kihuishi ‘magega’ chenye maana ya kabla pamoja na kiwakilishi ‘yayu’ chenye maana ya hayo.

### **Ase ekeene**

#### **MF9<sup>6</sup>:**

**(Muktadha: Mazungumzo ya kijamii. Wasailiwa wanazungumza kuhusu mwalimu fulani ambaye wanadai hakuwa akiwfundisha walipokuwa shulen)**

| Kikisii  | Kiswahili  |
|--|--|
| <p><b>K:</b> Tiga kongainereri tata! Mwarimu oyu tatosometi. Ase ekeene, igo asoete ekerasi gatato rioka. Bono oyu n’omonto oratebe nga natosometi. Omonto ori n’omworo bobe.</p> <p><b>J:</b> Ebe nasoete rimo gose gatato buna ogoteba igo nga tatosometi?</p> | <p><b>K:</b> Acha kudanganya bwana! Huyo mwalimu hakutufundisha Kwa hakika aliingia darasani mara tatu tu. Sasa huyo ni mtu utasema kuwa alitufundisha. Yule mtu ni mzembe vibaya.</p> <p><b>J:</b> Iwe aliingia mara moja au maratati kama unavyosema hivyo hakutufundisha?</p> |

Mwarimu oyu tatosometi. /Ase ekeene, igo asoete ekerasi gatato rioka.

Mw-arimu o-yu ti-a-nya-go-to-som-i. **Ase e-ke-ene** igo a-so-ete e-ke-rasi ga-tato ri-oka.

IDU-MZZ NGL-MZZ KAN-NJ-NFS3U-KAT-SH-MZZ-IT. **KUM(H-KAT-NGL-MZZ)** KIM NFS3U-MZZ-MAT KAT-IDU-MZZ NGL-MZZ NGL-MZZ

(Mwalimu huyo hakutufunza. Kwa hakika aliingia darasani mara tatu tu.)

Katika **MF9<sup>6</sup>**, ‘ase ekeene’ imetumika kama **KUM**. **KUM** hiki kimeundwa kwa kuunganisha kihuishi ‘ase’ chenye maana ya kwa, pamoja na nomino ‘ekeene’ (ukweli).

**KUM** hiki kina maana ya ‘kwa ukweli’.

## Ase enchera ende

### **MF9<sup>7</sup>:**

(Muktadha: Mazungumzo ya kijamii. *Mtafiti anashiriki mazungumzo na rafiki yake ambaye ametoka shambani. Rafiki huyo anamweleza kuwa amechoka mno*)

| Kikisii  | Kiswahili  |
|--|--|
| <p><b>W:</b> Aye tata! Mmogondo okare koru bono?</p> <p><b>Y:</b> Aye oroce nobisi nkoru? Mmogondo nkoru. Nagoyire. Ase enchera ende nigo ngoteba nga narosire pi. Igo nyigwete nanga naikire nka ntimoke.</p> | <p><b>W:</b> Wewe bwana! Unatoka shambani?</p> <p><b>Y:</b> Wewe unaona natoka afisini? Natoka shambani. Nimechoka. Kwa njia nyingine ninasema kuwa nimechoka kabisa. Nahisi ningekuwa nimefika nipumzike.</p> |

Nagoyire. /Ase enchera ende nigo ngoteba nga narosire pi  
 N-a-goy-ire. **Ase e-nchera e-nde** nigo n-go-teb-a nga ni-a-ros-ire pi  
 NFS1U-NJ-MZZ-K. **KUM(H-KAT-MZZ IDU-MZZ)** KIM NFS1U-Kat-MZZ-IT U NFS1U-NJ-NJ-MZZ-K E  
 (Nimechoka. Kwa njia nyingine ninasema kuwa nimechoka kabisa)

**KUM ‘ase enchera ende’** kimetumika katika **MF9<sup>7</sup>** ili kufanikisha mshikamano katika tungo kilimotumika. **KUM** hiki kimeundwa kutokana na kuweka pamoja kihuishi ‘ase’ (kwa) pamoja na nomino ‘enchera’ (njia) ‘ende’ (nyingine). Kinadhihirisha muundo wa H+KN(N+V).

## Ase bono

### **MF9<sup>8</sup>:**

(Muktadha: Mazungumzo ya kijamii. *Wazungumzaji G na H wanashiriki mazungumzo. H anamwomba g ampe usaidizi fulani lakini g anakataa kwa madai kuwa amechelewa*)

| Kikisii   | Kiswahili  |
|---|--|
| <p><b>G:</b> Nche tiga ngende. Tikonyara goetani ns'echi.</p> | <p><b>G:</b> Acha mimi niende siwezi kuzidisha saa hizi.</p> <p><b>H:</b> Si ukubali unisaidie kidogo kisha twende</p> |

|  |  |
|--|--|
| <p><b>H:</b> Otagwancha rende orambwatisi akeigo<br/>tomyete kogenderani gochi abwo</p> <p><b>G:</b> Nanyoriru mono <b>ase bono</b> tinkonyara<br/>kogokonya. Ninki otaganterbeiri koru<br/>gese. Gose n'enchera okorigi egere<br/>onyoreri igaa. Tiga aye nche<br/>nkobwatesi mambia.</p> | <p>pamoja</p> <p><b>G:</b> Nimechelewa sana <b>kwa sasa</b> sitaweza<br/>kukusaidia. Mbona hukunambia mapema.<br/>Au ni njia unatafuta unicheleweshe hapa.<br/>Acha wewe nitakusaidia kesho.</p> |
|--|--|

Nanyoriru mono /**ase bono** *tinkonyara kogokonya*  
**Ni-a-nyor-iru** mono **ase bono** ti-n-ko-nyar-a ko-go-kony-a  
 NFS1U-NJ-MZZ-K E **KUM(H-W)** KAN-NFS1U-Kat-MZZ-IT KAT-SH-MZZ-IT  
 (Nimechelewa sana kwa sasa sitaweza kukusaidia)

Katika **MF9<sup>8</sup>** kumetumika **KUM** ili kufanikisha mshikamano katika tungo husika. Tungo  
 hizo ni ‘*Nanyoriru mono*’ (Nimechelewa sana) na ‘*Tinkonyara kogokonya*’ (Sitaweza  
 kukusaidia). **KUM** ‘**ase bono**’ kimeundwa kwa kuweka pamoja kihuishi ‘ase’ (kwa)  
 pamoja na kiwakilishi ‘bono’ (sasa). Kina muundo wa H+KN.

### Ase ogokorera ekeene

**MF9<sup>9</sup>:**

(Muktadha: Mazungumzo ya kijamii. *Mtafiti anashiriki mazungumzo na rafiki yake ambaye ametoka shambani. Rafiki huyo anamweleza kuwa amechoka mno*)

| Kikisii   | Kiswahili   |
|---|---|
| <p><b>Mtafiti:</b> Ninki ogoyerete igo?</p> <p><b>Oriku:</b> Nakorire emeremo emenge rero. <b>Ase ogokorera ekeene</b> narosire. Igo<br/>okagete nga emeremo ngokora<br/>neyegosori....</p> | <p><b>Mtafiti:</b> Mbona umechoka hivyo?</p> <p><b>Oriku:</b> Nimefanya kazi nyingi leo. <b>Kwa kweli</b><br/>nimechoka. Unafikiri kuwa kazi ninafanya<br/>ni mchezo.....</p> |

Nakorire emeremo emenge rero. /*Ase ogokorera ekeene narosire.*

N-a-kor-ire e-me-remo e-menge rero. **Ase o-go-kor-era ekeene ni-a-ros-ire**

NFS1U-NJ-MZZ-K NGL-IDU-MZZ E **KUM(H – (KN) KAT-Kat-MZZ-K N)** NFS1U-NJ-MZZ-K

(Nimefanya kazi nyingi leo. Kwa kweli nimechoka)

Katika **MF9<sup>9</sup>** kumetumika KUM kina muundo wa KH. KUM hiki kina muundo wa H – (KN) KAT-Kat-MZZ-K N. Kimefanikisha mshikamano baina ya tungo mbili: *Nakorire emeremo emenge rero* (Nimefanya kazi nyingi leo) na *narosire* (nimechoka).

### **Ase bono iga**

**MF9<sup>10</sup>:**

**(Muktadha: Mazungumzo ya kijamii. Mzungumzaji F anamweleza G ni kwa nini hataki kumwadhibu mtoto wake ambaye ni mtukutu)**

| Kikisii   | Kiswahili   |
|---|---|
| <p><b>G:</b> Otarochi buya omwana oyo nkogosinyare pi. Igo agocha kogera orere amariga.</p> <p><b>H:</b> Ntebingo ninki ngokora? Natemire komokanya tari koigu. Goikera abu, timbwati ekio ndatebe. Ense nero erache komogambera. Abagusii ebagoteba gambera omuya .....</p> <p><b>G:</b> Igo nabo otagete agendere koba igo buna are?</p> <p><b>H:</b> Nche namokwaneire tatagetii koigu. Ase bono iga, nesabire amagoko ane. Tiga ere akore buna atagete.....</p> | <p><b>G:</b> Usipochunga huyu mtoto atakushinda kabisa. atakufanya ulie machozi</p> <p><b>H:</b> Niambie nifanye nini? Nimejaribu kumkanya hasikii. Kufikia hapo, sina cha kusema. Ulimwengu ndio utamrudi. Wakisii wanasesma mrekebishe mwema.....</p> <p><b>G:</b> Hivyo unataka kuwa hivyo alivyo?</p> <p><b>H:</b> Mimi nimenzungumzia hataki kusikia. Kwa sasa hivi, nimenawa mikono yangu. Acha yeeye afanya anavyotaka .....</p> |

Nche namokwaneire tatageti koigu. /**Ase bono iga**, nesabire amagoko ane.

Nche ni-a-mo-kwane-ire ti-a-taget-i ko-igu. **Ase bono iga**, ni-a-esab-ire a-ma-goko a-ne.

W NFS1U-NJ-SH-MZZ-K KAN-NJ-MZZ-IT Kat-MZZ **KUM(H-N-V)** NFS1U-NJ-MZZ-K NGL-IDW-MZZ NGL-MZZ  
(Mimi nimemzungumzia hataki kusikia. Kwa sasa hivi, nimenawa mikono yangu.)

Katika **MF9<sup>10</sup>** kumetumika KUM ‘ase bono iga’ (kwa sasa hivi). KUM hiki kimeundwa kutokana na KH na kinafanikisha mshikamano baina ya vishazi viwili: Nche namokwaneire tatageti koigu (Mimi nimemzungumzia hataki kusikia). na nesabire amagoko ane (nimenawa mikono yangu).

### **Ase chingaki echo**

**MF9<sup>11</sup>:**

**(Muktadha: Mazungumzo ya kijamii. Mtafiti anashiriki mazungumzo na wazee fulani ambapo mmoja wao anaeleza jinsi maisha yalivyoyeuka na kuwa magumu.)**

| Kikisii  | Kiswahili   |
|--|---|
| <p><b>Mtafiti:</b> Abagaka aba inu chingaki chiano nechingiya chiarenge.</p> <p><b>Ondimu:</b> Ninki gose gwatebera igo?</p> <p><b>Mtafiti:</b> Torochi buna mwariete amaremo</p> <p><b>Ondimu:</b> (Kicheko) Tari nga twariete. Amaremo nigo arenge koonigu inse ake. Ase chingaki echo tikwarenge konyora boremo bokoonigu ribu ngima.</p> | <p><b>Mtafiti:</b> Ninyi wazee ninyi siku zenu zilikuwa nzuri</p> <p><b>Ondimu:</b> Mbona umesema hivyo?</p> <p><b>Mtafiti:</b> Si unaona namna mlinyakua mashamba</p> <p><b>Ondimu:</b> (Kicheko) Sio eti tulinyakua. Mashamba yalikuwa yanauzwa chini kidogo. Kwa wakati huo hungepata shamba linalouzwa elfu nzima</p> |

Amaremo nigo arenge koonigu inse ake./ **Ase chingaki echo tikwarenge konyora boremo bokoonigu ribu ngima.**

A-ma-remo nigo a-renge ko-oni-gu inse ake. **Ase chi-*ngaki e-cho*** ti-kw-a-renge ko-nyor-a bo-remo bo-ko-oni-gu ribu ngima.

NGL-IDW-MZZ KIM NGL-MZZ Kat-MZZ-K E E. **KUM(H NG-MZZ NGL-MZZ)** KAN-NFS2U-NJ-MZZ Kat-MZZ-IT IDU-MZZ IDU-Kat-MZZ-K E E.

(Mashamba yalikuwa yanauzwa chini kidogo. Kwa wakati huo hungepata shamba linalouzwa elfu nzima)

Katika **MF9<sup>11</sup>** kumetumika **KUM** ambayo ni kirai kizima katika kuleta mshikamano katika tungo husika. KUM ‘ase chingaki echo’ kinadhihirika kujengwa kutoka kwa kihusishi.

### **3.1.3.2 VUM vinavyotokana na Kundu Tenzi**

VUM vinavyodhihirika katika sehemu hii ni VUM vyenye muundo wa virai na ambavyo mizizi yake inatokana na vitenzi.

#### **Kobua mono**

**MF10<sup>1</sup>:**

(Muktadha: Mazungumzo ya kijamii. *James anamweleza Mikuro matarajio yake ya baadaye*)

| Kikisii   | Kiswahili  |
|---|--|
| <p><b>James:</b> Nche tingokorera banto nchera eywo. Ninganeti gokonya ababoraka. Kobua mono nindabe ginkobakonya abangina amo na abataka.....</p> <p><b>Mikuro:</b> Igo mbuya. Nche igo nkogosabera. Nyasae aigu amasabo ao.</p> | <p><b>James:</b> Mimi siwezi kufanya watu hivyo. Ninataka kusaidia wajane. Zaidi sana nitakuwa nikiwasaidia akina mama pamoa na masikini....</p> <p><b>Mikuro:</b> Hivyo ni vizuri. Mimi ninakuombea. MUngu asikie maombi yako</p> |

Ninganeti gokonya ababoraka. /**Kobua mono** nindabe ginkobakonya abangina amo na abataka.

Ni-n-gan-eti go-kony-a a-ba-boraka. **Ko-bua mono** ni-n-rabe gi-n-ko-ba-kony-a a-ba-ningina amo na a-ba-taka.

KIM-NFS1U-MZZ-K Kat-MZZ-IT NGL-IDW-MZZ. **KUM**(Kat-MZZ E) KIM-NFS1U-MZZ NJ-NFS1U-Kat-IDW-MZZ-IT NGL-IDW-MZZ U NGL-IDW-MZZ

(Ninataka kusaidia wajane. Zaidi sana nitakuwa nikiwasaidia akina mama pamoja na masikini)

Katika **MF10<sup>1</sup>**, kumetumika **KUM ‘kobua mono’** **KUM** hiki kimeundwa kutokana na kitenzi ‘bua’ (shinda). MZZ huu wa kitenzi umewekewa kiambishi ko- ili kuunda nomino ya kitenzi jina ‘kobua’. Kielezi ‘mono’(zaidi) kimeongezewa ili kuunda **KUM**.

### **Komenta nayu**

**MF10<sup>2</sup>:**

*(Muktadha: Mazungumzo ya kijamii. Mtafiti anashiriki mazungumzo na rafiki zake kuhusu watoto wa mitaani. Mmoja wa rafiki zake anaeleza jinsi ambavyo watoto hao huweza kula au kunywa chochote bila ya kuathirika.)*

| Kikisii   | Kiswahili   |
|---|---|
| <p><b>Mtafiti:</b> Abana bari nNyasae obarendete<br/> <b>J:</b> (Akimkatiza) Naende Nyasae igo abanchete mono<br/> <b>K:</b> Abana aba ba chokora nigo bakori kende gionsi. <b>Komenta nayu</b> igo bakonyu mache ande onsi aba tibari korwara. Aye omochani ori endagera bakori igo ogokorera nyagetari.<br/> <b>J:</b> Amaene pi!....</p> | <p><b>Mtafiti:</b> Watoto wale ni Mungu anawalinda<br/> <b>J:</b> (Akimkatiza) Tena Mungu anawapenda sana<br/> <b>K:</b> Watoto hawa wa mitaani wanakula chochote. <b>Pamoja na hayo</b> wanakunywa maji yoyote ingawa hawawi wagonjwa. Wewe ukijaribu ule chakula wanachokula utaishia hospitali.<br/> <b>J:</b> Kweli kabisa! .....</p> |

Abana aba ba chokora nigo bakori kende gionsi. */Komenta nayu igo bakonyu mache ande onsi aba tibari korwara*

A-ba-na a-ba ba chokora nigo ba-ko-ri kende gi-onsi. **Ko-ment-a na-yu** igo ba-ko-nyu mache a-nde o-nsi aba ti-ba-ri ko-rwara

NGL-IDW-MZZ NGL-MZZ H N KIM IDW-Kat-MZZ V NGL-MZZ. **KUM**(Kat-MZZ-IT H-W) KIM IDW-Kat-MZZ N NGL-MZZ NGL-MZZ U KAN-IDW-MZZ Kat-MZZ

(Watoto hawa wa mitaani wanakula chochote. Pamoja na hayo wanakunywa maji yoyote ingawa hawawi wagonjwa)

**KUM ‘komenta nayu’** ambacho kimetumika katika **MF10<sup>2</sup>**, kinafanikisha mshikamano katika tungo kilimotumika. **KUM** hiki kimeundwa kwa kuweka pamoja nommo yakitenzi jina ‘komenta’ na kiwakilishi ‘nayu’. ‘komenta’ imeundwa kwa kuambisha Kat (ko) katika MZZ ‘-ment-‘ wenye maana ya ongeza. Katika **MF10<sup>2</sup>** KUM hiki kimefanikisha mshikamano.

### **Naki gekogera**

**MF10<sup>3</sup>:**

**(Muktadha: Mazungumzo ya kijamii. Wasailiwa wanajadiliana kuhusu madhara yanayowapata wakristo bandia)**

| Kikisii  | Kiswahili   |
|--|---|
| <p><b>J:</b> Gose igo okonyora omonto egasete rituko ryesabato. Omonto agotara orakage nga nigoro arure</p> <p><b>K:</b> (Akimkatiza) okonyora ebinto bagokora amatuko aya ande nebyogokumi.</p> <p><b>J:</b> Naende manya bakori nonya nepasaka</p> <p><b>K:</b> Otagotiga aye. Nomanyete nga nkonyora bare amaaku amanene?</p> <p><b>J:</b> Ee! Abange barire omogati na konywa egekombe batarengereti, naki gekogera abange babeire abarwaike na abareu. Nyasae tari gokoreru gosori naende tokomongaina. Mmwanyabanto oranya kongaina.</p> | <p><b>J:</b> Si unapata mtu amejikaza siku ya sabato. Mtu anatembea utafikiri ametoka juu</p> <p><b>K:</b> (Akimkatiza) utapata vitu wanafanya hizi siku nydingine ni vya ajabu</p> <p><b>J:</b> Tena fahamu wanashiriki hata pasaka</p> <p><b>K:</b> We acha. Unajua kuwa wanapata adhabu kubwa?</p> <p><b>J:</b> Ee! Wengi wamekula mkate na kunywa kikombe bila ya kujihoji. Ndicho kinachofanya wengi wamekuwa wagonjwa na wanyonge. Mungu hafanyiwi mchezo tena huwezi kumdangaya. Ni binadamu unaweza kuwa ukidanganya.</p> |

Abange barire omogati na konywa egekombe batarengereti, */naki gekogera abange babeire abarwaire na abareu*

A-ba-nge ba-ri-re o-mo-gati na ko-nywa e-ge-kombe ba-ti-a-renger-eti, **naki ge-ko-ger-a** a-ba-nge ba-b-eire a-ba-rwaire na a-ba-reu

NGL-IDW-MZZ IDW-MZZ-KIT:NJ KAT-IDU-MZZ U Kat-MZZ KAT-NGL-MZZ IDW-KAN:NJ NFS3W-KAN-NJ-MZZ-MAT, **KUM** (W NGL-Kat-MZZ-IT) NGL-NGL-MZZ IDW-MZZ-K:NJ NGL-IDW-MZZ U NGL-IDW-MZZ

(Wengi wamekula mkate na kunywa kikombe bila ya kujihoji. Ndicho kinachofanya wengi wamekuwa wagonjwa na wanyonge)

‘**Naki gekogera**’ ambacho ni **KUM** katika **MF10<sup>3</sup>** kimefanikisha mshikamano. **KUM** hiki kimeundwa kutokana na kitenzi ambacho MZZ wake ni ‘-ger-’ na ambao una maana ya sababisha.

### **Kobwati ayu**

**MF10<sup>4</sup>:**

(Muktadha: Darasani. *Mwanafunzi mmoja anasimulia kisa kuhusu mtoto fulani aliyekuwa mtundu*)

| Kikisii   | Kiswahili  |
|---|--|
| .....omwana oyu nigo arenge omochäge ekerage. Ebe nka ebe esukuru, Mokeira tarengé gokanegeka gose gotebererigu. Gochi nka tarengé mobe mono asengecho ise arenge omotindi. Engaki eyemo nakorete amakumi esukuru. Mokeira igo arenge konya goaka eriogi. Kobwati ayu ekero omwarimu amorangeria gochi abisi igo aagete omwarimu. | .... Mtoto huyo alikuwa mchokozi sana. Iwe nyumbani iwe shulen, Mokeira alikuwa hakataziki. Hata nyumbani hakuwa mbaya sana kwakuwa baba yake alikuwa mkali. Siku moja alifanya maajabu shulen. Mokeria alikuwa akipigapiga kelele. Kufuatia hayo, wakati mwalimu alimwita, alimpiga mwalimu |

Mokeira igo arenge konya goaka eriogi. */Kobwati ayu ekero omwarimu amorangeria gochi abisi igo aagete omwarimu.*

Mokeira igo a-re-nge ko-nya go-ak-a e-riogi. **Ko-bwat-i ayu** ekero o-mw-arimu a-mo-rangeri-a go-chi abisi igo a-ag-ete o-mw-arimu.

N KIM NFS3U-MZZ-K Kat-MZZ Kat-MZZ-IT NGL-MZZ.KUM(Kat-MZZ NGL-MZZ) N  
KAT- NGL-MZZ-IT Kat-MZZ KIM NFS3U- MZZ-MAT KAT-NGL-MZZ

(Mokeria alikuwa akipigapiga kelele. Kufuatia hayo, wakati mwalimua alimwita, alimpiga mwalimu)

Katika **MF10<sup>4</sup>**, **KUM ‘kobwati ayu’** kimetumika ili kuleta mshikamano katika tungo husika. **KUM** hiki kimeundwa kutokana na kitenzi ambacho MZZ wake ni ‘-bwat-’ wenye maana ya fuata. MZZ huu umeambishwa Kiambishi awali tangulizi (ko-) na baadaye kufuatizwa na kiwakilishi.

### **Goikera bono**

#### **MF10<sup>5</sup>:**

**(Muktadha: Mazungumzo ya kijamii. Wazungumzaji wawili L na M wanamwelezea mtafiti ni kwa nini hawapendi kujishughulisha na biashara)**

| Kikisii  | Kiswahili  |
|--|--|
| <p><b>L:</b> Buna nche mboonchoreri ki ntarakora?</p> <p><b>M:</b> Aa! Twatemire tata!</p> <p><b>L:</b> Twatemire kera egento goikera bono twatigire gwechanda. Omonto igo korora nga gincha onye gokonyara konyora endagera, ngecho teiyo oranya konya gwechandera.</p> | <p><b>L:</b> Kama mimi ni biashara gani sijafanya?</p> <p><b>M:</b> Aa! Tumejaribu bwana!</p> <p><b>L:</b> Tumejaribu kila kitu hadi sasa tumeacha kujisumbua. Mtu unaona kuwa ilmradi unaweza kupata chakula, hapana haja ya kujisumbuasumbua</p> |

Twatemire kera egento /**goikera bono twatigire gwechanda**

Tu-a-tem-ire kera e-gento **go-ik-era bono** tu-a-tig-ire go-e-chand-a

NFS1W-NJ-MZZ-K V N **KUM**(Kat-MZZ-K E) NFS1W-NJ-MZZ-K Kat-NJ-MZZ-IT

(Tumejaribu kila kitu hadi sasa tumeacha kujisumbua)

‘**Goikera bono**’ ambayo imetumika kama **KUM** katika **MF10<sup>5</sup>**. Hapa **KUM** imeundwa kutokana na kitenzi chenye MZZ ‘-ik-’ chenye maana ya fika. MZZ huu umeambishiwa Kat (go-) na baadaye kufuatizwa kielezi *bono* chenye maana ya sasa.

### Goikera abu

**MF10<sup>6</sup>:**

(Muktadha: Mazungumzo ya kijamii. *Mzungumzaji F anamweleza G ni kwa nini hataki kumwadhibu mtoto wake ambaye ni mtukutu*)

| Kikisii  | Kiswahili   |
|--|---|
| <p><b>G:</b> Otarochi buya omwana oyo<br/>nkogosinya are pi. Igo agocha kogera<br/>orere amariga.</p> <p><b>H:</b> Ntebingo ninki ngokora? Natemire<br/>komokanya tari koigu. Goikera abu,<br/>timbwati ekio ndatebe. Ense nero<br/>erache komogambera. Abagusii<br/>ebagoteba gambera omuya .....</p> | <p><b>G:</b> Usipochunga huyo mtoto atakushinda<br/>kabisa. Atakufanya ulie machozi.</p> <p><b>H:</b> Hebu niambie nifanye nini? Nimejaribu<br/>kumkanya hasikii. Kufikia hapo sina cha<br/>kusema. Ulimwengu utamrudi. Wakisii<br/>wanasema mkanye mwema .....<br/>tabia</p> |

Natemire komokanya tari koigu. /**Goikera abu, timbwati ekio ndatebe.**

Ni-a-tem-ire ko-mo-kany-a ti-a-r-i ko-igu **go-ik-era abu**, ti-m-bwat-i e-kio n-ra-teb-e.

NFS1U-NJ-MZZ-K Kat-SH-MZZ-IT KAN-NFS3U-MZZ-ITKAN Kat-MZZ **KUM**(Kat-MZZ-K E)

KAN-NFS1U-MZZ-IT NGL-MZZ NFS1U-NJ-MZZ-K

(Nimejaribu kumkataza hasikii kufikia hapo sina cha kusema)

Katika **MF10<sup>6</sup>**, ‘goikera abu’ kimetumika kama **KUM**. **KUM** hiki kimetumika katika kufanikisha mshikamno katika tungo kilimotumika. **KUM** hiki kimeundwa kwa kuambishiwa Kat (go-) na baadaye kuongezewa kielezi *abu* chenye maana ya hapo.

### **Otatiga bono**

#### **MF10<sup>7</sup>:**

(Muktadha: Mazungumzo ya kijamii. *Wazungumzaji wawili G na H wanajadiliana ni vipi ambavyo kaiyefa ni nzuri kwa kuweka ua*)

| Kikisii   | Kiswahili   |
|---|---|
| <p><b>G:</b> Onye ndiri omonto okonyara nanga igo okorigi enchera ere engiya yokogita. Sengenge teri ngiya ase okogita...</p> <p><b>H:</b> (Akimkatiza) Yaya sengenge teri ngiya! Ekaiyaba nigo ere engiya mono ase okogita. Otatiga bono okobwata kwaye naku ogokongu.</p> | <p><b>G:</b> Ingekuwa mtu unaweza ungetafuta njia nzuri ya kuweka ua. Sengenge sio nzuri kwa kuweka ua</p> <p><b>H:</b> (Akimkatiza) Hapana sengenge sio nzuri! <i>Kaiyefa ni nzuri sana kwa kuweka ua.</i> Isipokuwa sasa kushika kwake ndiko kugumu</p> |

Ekaiyaba nigo ere engiya mono ase okogita. */Otatiga bono okobwata kwaye naku ogokongu.*

E-kaiyaba nigo e-re e-ngiya mono ase o-ko-git-a. **Otatiga bono** o-ko-bwat-a ku-aye naku o-go-kongu

NGL-MZZ KIM NGL-MZZ NGL-MZZ E H KAT-Kat-MZZ-IT **KUM**. KAT-Kat-MZZ-IT NGL-MZZ V KAT-Kat-MZZ

(*Kaiyefa ni nzuri sana kwa kuweka ua. Isipokuwa sasa kushika kwake ndiko kugumu*)

‘**Otatiga bono**’ ambayo imetumika kama **KUM** katika **MF10<sup>7</sup>**. Imeundwa kutokana na MZZ wa kitenzi ‘-tig-’ chenye maana ya acha. **KUM** hiki huchukua nafasi ya katikati katika tungo na kama inavyojitokeza katika **MF10<sup>7</sup>** hutanguliza tungo ya pili ya matini husika.

## **Kobwatekani naywo**

**MF10<sup>8</sup>:**

(Muktadha: Darasani. *Mwanafunzi mmoja anawahimiza wenzake kusoma kwa bidii. Anawatolea kisa cha mvulana ambaye alikuwa akicheza na masomo*)

| Kikisii   | Kiswahili  |
|---|--|
| Timonya gokora egosori namasomo. Omogano oyu nabaa nabo oisane kobaoroki obobe bwogokora egosori ase amasomo. Omomura ori nigo akorete egosori ase amasomo. Kobwatekani naywo takoreti buya ase amatemu ..... | Msiwe mkifanya mchezo na masomo. Hadithi hiyo ambayo nimewapa unatosha kuwaonyesha ubaya wa kufanya mchezo masomoni. Mvulana yule alifanya mchezo katika masomo. Kufuatana na hayo hakufanya vizuri katika masomo yake |

Omomura ori nigo akorete egosori ase amasomo. /**Kobwatekani naywo takoreti buya ase amatemu**

O-mo-mura o-ri nigo a-kor-ete e-gosori ase a-masomo. **Ko-bwatekani na-aywo** ti-a-kor-eti buya ase a-ma-temu

KAT-IDU-MZZ NGL-MZZ KIM NFS3U-MZZ-MAT KAT-MZZ H NGL-MZZ. **KUM**(Kat-MZZ H-MZZ) KAN-NFS3U-MZZ-K E H NGL-IDW-MZZ

(Mvulana yule alifanya mchezo katika masomo. Kufuatana na hayo hakufanya vizuri katika masomo yake)

Katika **MF10<sup>8</sup>**, kumetumika **KUM. KUM** hiki kimeundwa kutokana na kuambishwa kwa Kat (ko-) katika MZZ wa kitenzi ‘bwatekani’ (fuatana). Kinafanikisha mshikamano katika tungo hii kwa kuashiria ule mfuatano wa matukio baina ya upande mmoja wa tungo na ule mwengine.

## **Nabo oranyore**

**MF10<sup>9</sup>:**

(Muktadha: Mazungumzo ya kijamii. *J na K wanashiriki mazungumzo huku wakiwa wanamongoja mwenzao ambaye amekawia. k anahoji kuwa huenda wanayemsubiri asije kwa kuwa amekawia*)

| Kikisii  | Kiswahili   |
|--|---|
| <p><b>J:</b> Chinsa echu chiachire mono. Gochi<br/>nkaira bogochi. Ntoche tokore<br/>memeremo eye bori?</p> <p><b>K:</b> Tindochi tokonyekora</p> <p><b>J:</b> Igo tokogenda gose toramoganya ake?</p> <p><b>K:</b> Mokua onyoriru mono oranyore tari<br/>gocha. Omanyete nabo ankorete iga<br/>rinde nkamoganya nkaganyora.<br/>Naende nomokora omororo. Tari<br/>monto morachikane nga ngokora<br/>more gento nere aikerani.</p> | <p><b>J:</b> Hizi saa zimekwisha sana. Hata kunaelekea<br/>kuwa usiku. Tutafanya hii kazi kweli?</p> <p><b>K:</b> Sioni tukiifanya</p> <p><b>J:</b> Twende au tumsubiri kidogo?</p> <p><b>K:</b> Mokua amechelewa mno huenda haji.<br/>Unajua alinifanya hivi wakati fulani<br/>nikamsubiri nikachoka, tena ni mkora ajabu.<br/>Sio mtu mnaweza kuahidiana naye kuwa<br/>mnafanya kitu naye aafikie</p> |

Mokua onyoriru mono. / *Nabo oranyore tari gocha*

Mokua o-nyor-iru mono. **Nabo o-ra-nyor-e** ti-a-r-i go-ch-a

N NFS2U-MZZ-K E. **KUM**(KIM NFS2U-K-MZZ-K) KAN-NFS3U-MZZ-IT Kat-MZZ-IT

(Mokua amechelewa sana. Unaweza kupata haji)

**MF10<sup>9</sup>** unadhihirisha **KUM** ambacho kimeundwa kwa KIM na mzizi wa kitenzi uliambishiwa viambishi. KUM katika **MF10<sup>9</sup>** kimejitokeza katikati ya matini hiyo na kimebainika kutanguliza tungo ya pili ya matini husika.

### 3.1.3.3 VUM vinavyotokana Kundi Elezi

VUM katika kundi hili hudhihirika kutokana na vielezi. Aghalabu VUM hivi hufanikisha mshikamano katika tungo husika kwa kutolea maelezo kuhusu tukio fulani lililotangulizwa katika sehemu ya kwanza ya tungo husika.

#### **Omoerio oye**

**MF11<sup>1</sup>:**

**(Muktadha: Mazungumzo ya kijamii. G na H wanajadiliana kuhusu msichana fulani ambaye G anadai kuwa ana bidii sana katika masomo)**

| Kikisii   | Kiswahili   |
|---|---|
| <p><b>G:</b> Omwano ori nigo are omwango.</p> <p><b>H:</b> Maria nigo abwate omoki ase amasomo aye. Omoerio oye goika akore buya mono. Chingaki chionsi igo okonyora kagokora emeremo yaye y'esukuru. Omanyete ndire nkwoboa nonya n'okomotoma?</p> | <p><b>G:</b> Yule mtoto ni mwepesi.</p> <p><b>H:</b> Maria ana bidii katika masomo yake mwishowe lazima atafanya vizuri mno. Nyakati zote utampata akifanya kazi yake ya shule. Unaju kuna wakati ninaogopa hata kumtuma?</p> |

Maria nigo abwate omoki ase amasomo aye. /Omoerio oye goika akore buya mono.

Maria nigo a-bwat-e omoki ase a-masomo a-ye. **Omoerio oye** go-ik-a a-kor-e buya mono.

N KIM NFS3U-MZZ-K N H NGL-MZZ NFS31-MZZ. **KUM(N-V) Kat-MZZ-IT NFS3U-MZZ-IT E E**

(Maria ana bidii katika masomo yake mwishowe lazima atafanya vizuri mno)

Katika MF11<sup>1</sup> **KUM ‘omoerio oye’** kimetumika. **KUM** hiki kimetumika ili kufanikisha mshikamnao katika tungo husika. **KUM** hiki kimeundwa kutokana na E ‘omoerio’ chenye maana ya mwisho.

## **Mambi yaye**

### **MF11<sup>2</sup>:**

(Muktadha: Mazungumzo ya kijamii. *Mzungumzaji J anamweleza K kuhusu maafa aliyokumbana nayo kwa kumkaribisha mgeni*)

| Kikisii   | Kiswahili  |
|---|--|
| <p><b>K:</b> Nche nnatiga obuya obonge. Igo ogokorera omonto amaya ere okobangera amabe oka.</p> <p>Nomanyete nga ndire nekorete omuya nkenyorera emechando? Omosani one nachete akarara bwone rimo. Mambi yaye nigo aimogete akagenda atachieti nantebi nga ochire....</p> <p><b>J:</b> (Akimkatiza) Oyu goika agakorete egento (kicheko).....</p> | <p><b>K:</b> Mimi niliacha uzuri mwingi. Unafanya mtu mazuri yeye anakupangia mabaya pekee.</p> <p>Unajua kuna wakati nilijifanya mzuri nikajipatia shida? Rafiki yangu alikuja akalala kwangu mara moja. Kesho yake alitoka akaenda bila hata kuniambia kuwa ameenda.....</p> <p><b>J:</b> (Akimkatiza) huyo lazima alifanya kitu (kicheko) .....</p> |

Omosani one nachete akarara bwone rimo. */Mambi yaye nigo aimogete akagenda atachieti nantebi nga ochire.*

O-mo-sani o-ne ni-a-ch-ete a-ka-rar-a bw-one ri-mo. **Mambi yaye** nigo a-imok-ete a-ka-gend-a a-ti-a-chi-eti ni-a-n-teb-i nga o-ch-ire.

KAT-IDU-MZZ NGL-MZZ KIM-NFS3U-MZZ-MAT NGL-MZZ NGL-MZZ. **KUM(N-V)** KIM NFS3U-MZZ-MAT NFS3U-SM-MZZ-IT NFS3U-KAN-NFS3U-MZZ-MAT KIM-NJ-NFS1U-MZZ-IT NGL-MZZ-K

(Rafiki yangu alikuja akalala kwangu mara moja. Kesho yake alitoka akaenda bila hata kuniambia kuwa ameenda)

Katika **MF11<sup>2</sup>**, **KUM ‘mambi yaye’** kimetumika. **KUM** hiki kimeundwa kutokana na E ‘mambi’ (kesho) pamoja na ‘yaye’ (yake). Viwili hivi vimetumika pamoja kama kielezi chenye maana ya kesho yake.

## Ekero ekio gionsi

### **MF11<sup>3:</sup>**

(Muktadha: Mazungumzo ya kijamii. *Mtafiti anashiriki mazungumzo na rafiki yake ambaye hajaonana naye kwa muda. Rafiki huyo anamweleza kuwa kwa muda mrefu amekuwa akiishi na jamaa yake*)

| Kikisii   | Kiswahili  |
|---|--|
| <b>Mtafiti:</b> Amatuko aywo onsi. Igo nga<br>ninka kwebisete<br><b>P:</b> Tinamenyete nka. Ekero ekio gionsi<br>nigo namenyete nomoiri. Onye ninka<br>aa nanga tikwarenge kondora. | <b>Mtafiti:</b> Siku hizo zote. Hivyo ulikuwa<br>umejificha nyumbani<br><b>P:</b> Sikuwa naishi nyumbani. Wakati huo wote<br>nilikuwa naishi na jamaa yangu. Ingekuwa<br>ni hapa nyumbani si ungekuwa unaniona |

Tinamenyete nka. */Ekero ekio gionsi nigo namenyete nomoiri*

Ti-ni-a-men-y-ete nka. **E-kero e-kio gi-onsi** nigo ni-a-men-y-ete na-o-mo-iri

KAN-NFS1U-NJ-MZZ-MAT N. **KUM**(NGL-MZZ NGL-MZZ NGL-MZZ) KIM NFS1U-NJ-MZZ-MAT H-KAT-IDU-MZZ  
(Sikuwa naishi nyumbani. Wakati huo wote nilikuwa naishi na jamaa yangu)

**KUM** kilichotumika katika **MF11<sup>3</sup>** kimeundwa kina muundo wa N+KV(V+E). Muundo huu kwa pamoja umeunda kielezi ambacho kimefanya kazi kama **KUM** ambacho kinawezesha mshikamano baina ya vishazi vinavyodhihirika katika tungo hii.

## Chinsa echo echo

### **MF11<sup>4:</sup>**

(Muktadha: Mazungumzo ya kijamii. *g na h ambao ni marafiki wanakutana na h anamfahamisha g kuhusu safari yake ilivyokuwa*)

| Kikisii  | Kiswahili   |
|--|---|
| <b>G:</b> Gwachire bwango! Endege kwarina<br>koru Getembe? | <b>G:</b> Umekuja upesi! Ni ndege umepanda kutoka<br>Getembe? |

|  |   |
|--|---|
| <p><b>J:</b> Nkoigu bono nga ebinto mbire bigosoa<br/>ase omobere ebio biagera omonto<br/>ochandeka engecho embe?</p> <p><b>K:</b> Bori? Gose nche igo nkagete nga<br/>noborwaire tu bogosoa?</p> <p><b>J:</b> Mbuya omanyе nga ebinto mbiroo.<br/>ebinyinyi ebio bikori ase omobere<br/>bwomonto</p> | <p><b>J:</b> Nasikia eti kuna vitu huwa vinaingia katika mwili<br/>na kufanya mtu asumbuke vibaya</p> <p><b>K:</b> Kweli? Si mimi ninadhani kwamba ni ugonjwa<br/>tu unaingia?</p> <p><b>J:</b> Ni vizuri ufahamu kuwa kuna vitu. Viini hivyo<br/>vinakula katika mwili wa mtu</p> |

- b) Mbuya omanyе nga **ebinto** mbiroo. **Ebinyinyi** ebio bikori ase omobere bwomonto  
M-buya o-many-e nga **e-bi-nto** m-bi-re oo. **E-bi-nyinyi** e-bio bi-ko-ri ase o-mo-bere  
bwa o-mo-nto  
KIM-MZZ IDU-MZZ-K KIM KAT-IDW-MZZ KIM-IDW-MZZ E. KAT-IDW-MZZ KAT-MZZ IDW-Kat-MZZ H  
KAT-IDU-MZZ H KAT-IDU-MZZ  
(Ni vizuri ufahamu kuwa kuna vitu. Viini hivyo vinakula katika mwili wa mtu)

Kisawe unganishi kinachukuliwa kuwa ni kipashio ambacho kinafanana na kipashio kingine kimaana na kando na kufanana huko, kinatekeleza jukumu la kuunganisha tungo au matini. Katika **MF17a**, neno *chiropi* limetumika kama kisawe cha *besa* (pesa). Aidha, katika **MF17b**, neno *ebinyinyi* (viini) limejitokeza kama kisawe cha *ebinto* (vitu). Usawe unaojitokeza katika **MF17a** ni wa kisemantiki ilhali unaojitokeza katika **MF17b** ni wa kimuktadha. Visawe hivi unganishi hasa vinavyojitokeza katika sehemu au tungo za pili kwenye matini husika mathalani: *chiropi* (pesa) na *ebinyinyi* (viini) vinaweza kuwa ni **VUM** kwa kuwa vinafanikisha mshikamano katika matini husika.

### **3.2.4 Jina la jumla**

Utafiti huu pia ulibainisha kuwa mshikamano katika tungo unaweza kufanikishwa na matumizi ya jina la jumla.

#### **MF18:**

**(Muktadha: Mazungumzo ya kijamii. Wazungumzaji wawili G na H wanajadiliana ni vipi ambavyo kaiyefa ni nzuri kwa kuweka ua)**

| Kikisii  | Kiswahili   |
|--|---|
| <p><b>G:</b> Onye ndiri omonto okonyara nanga igo okorigi enhera ere engiya yokogita. Sengenge teri ngiya ase okogita...</p> <p><b>H:</b> (Akimkatiza) Yaya sengenge teri ngiya! Ekaiyaba nigo ere engiya mono ase okogita. Otatiga bono okobwata kwaye naku ogokongu.</p> <p><b>G:</b> Ngwantebeti bono nga omomura ori omomanyi namanyete koringa ekaiyefa eyu buya?</p> <p><b>H:</b> Omochani omotebi nga <b>ndingere ekaiyeba</b>, nigo <b>arakogitere</b> oichane nga mmangana ki aya</p> <p><b>G:</b> Nachio bono ngocha gosimeka?</p> | <p><b>G:</b> Ingekuwa mtu unaweza ungetafuta njia nzuri ya kuweka ua. Sengenge sio nzuri kwa kuweka ua</p> <p><b>H:</b> (Akimkatiza) Hapana sengenge sio nzuri! <i>Kaiyefa ni nzuri sana kwa kuweka ua.</i> Isipokuwa sasa kushika kwake ndiko Kugumu</p> <p><b>G:</b> Si uliniambia kuwa yule kijana wa Momanyi anajua kukunja hiyo <i>kaiyefa vizuri?</i></p> <p><b>H:</b> Ukidhubutu umwambie <b>nikunjie kaiyefa</b> anaweza <b>kukuwekea ua</b> ushangae ni maneno gani haya</p> <p><b>G:</b> Ndizo sasa nitapanda</p> |

- a) Omochani omotebi nga **ndingere ekaiyeba**, nigo **arakogitere** oichane nga mmangana ki aya  
O-mochani o-mo-teb-i nga **n-ring-ere e-kaiyeba**, nigo **a-ra-ko-git-ere** o-ichan-e nga m-ma-ngana ki aya  
NFS2U-MZZ NFS2U-SH-MZZ-IT KIM NFS1U-MZZ-K NGL-MZZ, KIM NFS3U-NJ-NFS2U-MZZ-K NFS2U-MZZ-K KIM KIM-IDW-MZZ V W  
(Ukidhubutu umwambie akukunjie *kaiyefa* anaweza kukuwekea ua ushangae ni maneno gani haya)

**(Muktadha: Mazungumzo ya kijamii. Wanakikundi cha maendeleo wanajadiliana kuhusu shughuli zao za kikundi. Mzungumzaji J anawashauri wenzake kuwa ikiwa mtu anataka kujifunza kuhusu mradi fulani ni bora anwite mwalimu wao ili ampe mafunzo)**

| Kikisii   | Kiswahili  |
|---|--|
| <b>J:</b> Omwarimu oito nabo eruete ase emeremo yaye. Tindochi naseki omonto orachandeke gosoa gokora meremo otanyare. Igo atebete nga onyore gotagete gosoma nigo okomorangeri akworokereri nga naki ogokora | <b>J:</b> Mwalimu wetu amejitolea katika kazi yake. Sioni ni kwa nini mtu unaweza kusumbuka kwa kufanya kazi usiyoweza. Alisema kuwa ikiwa unataka kusoma unamwita akuonyeshe ni vipi unafanya |

- b) Igo atebete nga onyore gotagete **gosoma** nigo okomorangeri **akworokereri** nga naki ogokora  
 Igo a-teb-ete nga onyore go-tag-ete **go-som-a** nigo o-ko-mo-ranger-i **a-ku-orokereri** nga n-naki o-go-kor-a  
 KIM NFS3U-MZZ-MAT KIM U NFS2U-MZZ-MAT Kat-MZZ-IT KIM NFS2U-Kat-SH-MZZ-IT NFS3U-NFS2U-MZZ KIM KIM-E NFS2U-Kat-MZZ-IT  
 (Alisema kuwa ikiwa unataka kusoma unamwita akuonyeshe ni vipi unafanya)

Mshikamano katika matini pia unaweza kuwezesha na matumizi ya **VUM (LP)** ambavyo ni majina ya jumla. Katika **MF17a**, *okogita* (kuweka ua) kunachukuliwa kuwa ni jina la jumla linaloweza kuashiria *okoringa ekaiyeba* (kukunja *kaiyefa*). Aidha, katika **MF17b**, *okoorokereri* (kuonyesha) inachukuliwa kuwa ni jina la jumla la *ogosoma* (kusoma). Kwa kuwa majina haya ya jumla – *okogita* (kuweka ua) na *okoorokereri* (kuonyesha) yanawezesha mshikamano katika matini ambamo yametumika, basi inachukuliwa kuwa majina haya ya jumla ni **VUM (LP)**.

### 3.3. Hitimisho

Katika sura hii imebainika kuwa mshikamano katika matini semwa za Kikisii unaweza kufanikishwa kwa matumizi ya VUM (U). Aidha, ilibainika kuwa VUM (U) katika matini semwa za Kikisii huwa na maumbo na miundo maalum ambayo ni bainifu. Kutokana na uchanganuzi uliofanyika katika sura hii ilibainika kuwa VUM (U) vinaweza kuwa vyamofu moja, neno moja, kirai au hata kishazi tegemezi. Sura hii pia imechanganua aina mbalimbali za VUM (LP) zinazojitokeza katika matini semwa za Kikisii. Utafiti ulibainisha kuwa VUM (LP) katika matini za Kikisii huwa za aina mbalimbali na kuwa kutokana na matumizi hayo ya VUM (LP) mshikamano hupatikana katika matini. VUM (LP) vilivyojitokeza katika matini semwa za Kikisii ni zile zilizodhihirisha udondoshaji wa nomino, vitenzi, kishazi na nomino + kitenzi. Aidha, aina nyiningine ya VUM (LP) ni vile vilivyojitokeza kufanikisha mshikamano kutokana na uradidi. Aina hizi za VUM zilihusisha uradidi wa N, KN na W. Ilibainika pia kuwa matini semwa za Kikisii visawe unganishi pamoja na majina ya jumla pia huweza kutumika kama VUM (LP) na kuwa vinapotumika hufanikisha mshikamano katika tungo.

## SURA YA NNE

### **MWINGILIANO WA VIJENZI UNGANISHI VYA MSHIKAMANO**

#### **4.0 Utangulizi**

Sura hii inachanganua na kuweka wazi miingiliano baina ya VUM mbalimbali vinavyopatikana katika matini semwa za Kikisii. Inaonyesha ni jinsi gani VUM viwili au zaidi vinaweza kutokea katika tungo moja na vinaingiliana na kukamilishana vipi.

#### **4.1 Mwingiliano wa LP na U**

##### **MF4<sup>2</sup>:**

*(Muktadha: Darasani. Hadithi ambapo msimulizi anasimulia kisa kuhusu watoto fulani waliokuwa watundi)*

| Kikisii  | Kiswahili   |
|--|---|
| Egatoka nga tibakonyara gokora buna konyora batebigu n'abaibori babo. Tibachieti gokanyeka nore. Naki gekogera abange bare abareu <b>na</b> abarwaire. Naende tari boigo rioka, tibarikonyara nonya nokorengereri nga naki baranyare gwekonya ase obogima bwabo. | Ikawa kuwa hawangeweza kufanya kama walivyokuwa wameambiwa na wazazi wao. hawakupo hata kidogo. Ndiyo sababu wengi ni wanyonge <b>na</b> wagonjwa. Tena si hivyo tu, hawawezi hata kufikiria ni vipi wanaweza kujisaidia katika maisha ya sasa. |

Naki gekogera abange bare abareu **/na abarwaire**

Naki ge-ko-ger-a a-bange ba-r-e a-ba-reu **na** a- ba-rwaire

W NGL-Kat-MZZ-IT NGL-NGL IDW-MZZ-K NGL-IDW-MZZ **KUM** NGL-IDW-MZZ

(Ndicho kinafanya wengi wako wanyonge na wagonjwa)

Katika **MF4<sup>2</sup>**, kumejitokeza mwingiliano wa VUM. Kama inavyodhihirika katika mfano huu, kuna LP na vilevile kuna U. LP inajitokeza kutokana na udondoshaji kama inavyodhihirika katika matini hii. Kitendi 'bare' (wako) kimedondoshwa kutoka kwa

tungo ya pili. Aidha, ‘**na**’ imetumika kama kiunganishi kinachounganisha tungo mbili za matini hii: ‘*naki gekogera abange bare abareu* (ndicho kinafanya wengi wako wanyonge)’ na ‘*naki gekogera abange bare abarwaire* (ndicho kinafanya wengi kuwa wagonjwa)’

### **MF5<sup>1</sup>:**

**(Muktadha: Mazungumzo ya kijamii. Wazee wawili C na D wanashiriki mazungumzo, mara anatokeza mtoto fulani na d anaamua kumtuma kwa mjomba wake)**

| Kikisii  | Kiswahili   |
|--|---|
| <p><b>C:</b> Ense ya bono yakongire. Tenga buna riri kare.</p> <p><b>D:</b> Aaah! Ee nabo igo tata. Noroche buna endagera yoka yachi igoro. Gose omonto igo ogosinyu mmeremo ki oranyore egere oikere oboigima bwa bono. (anatokeza mtoto fulani). Aye baba mbuya ore?</p> <p><b>Mtoto:</b> Ee! Mbuya mono sokoro</p> <p><b>D:</b> Ningore nka?</p> <p><b>Mtoto:</b> Ntata.</p> <p><b>D:</b> Igo mbuya. Gachi omotebi atome omwana ache kondora <b>gose</b> motebi ache ere bweka. Narosire namanga akonya gonkori. Tiga amanye nga nche n'omonto omonene. Tindi mwana nche.</p> | <p><b>C:</b> Dunia ya sasa imekuwa ngumu. Sio kama zamani.</p> <p><b>D:</b> Aaah! Ee ni hivyo bwana. Unaona namna chakula pekee kimepanda. Si mtu unashindwa ni kazi utapata ili ufkie maisha ya sasa. (anatokeza mtoto fulani) we hujambo?</p> <p><b>Mtoto:</b> Ee! Sijambo babu</p> <p><b>D:</b> Nani yuko nyumbani?</p> <p><b>Mtoto:</b> Ni baba</p> <p><b>D:</b> Hivyo ni vizuri. Nenda umwambie atumie mtoto aje kuniona <b>au</b> mwambie aje ye ye mwenyewe. Nimechoshwa na mambo ambayo ananifanyisha. Acha ajue kuwa mimi ni mtu mzima. Mimi si mtoto.</p> |

Gachi omotebi atome omwana ache kondora /**gose** motebi ache ere bweka.

Gach-i o-mo-teb-i a-tom-e o-mw-ana a-che ko-n-ror-a **gose** a-che bwe-ka

MZZ-IT NFS2U-SH-MZZ-ITKAN NFS3U-MZZ-MAT NGL1-IDU-MZZ **KUM** NFS3U-MZZ NGL1-MZZ

(Nenda umwambie atume mtoto aje kuniona au aje mwenyewe)

Katika **MF5<sup>1</sup>** pia kumejitokeza mwingiliano wa VUM. Hapa kuna LP inayotokana na udondoshaji wa vipashio na kwa wakati uo huo kuna U. Katika tungo ya pili ya matini hii, kipashio ‘*gachi*’ (nenda) pamoja na kiambishi NFS2U ‘o’ vimedondoshwa. Aidha, katika matini hii kuna matumizi ya VUM (U) ambayo ni *gose* (au). Matumizi ya LP

pamoja na U katika matini hii yanadhihirisha kuwa VUM (LP) na U huweza kuingiliana na kukamilishana katika kufanikisha mshikamano katika matini semwa za Kikisii.

## MF5<sup>2</sup>:

**(Muktadha: Mazungumzo ya kijamii. *wasailiwa watatu wanajadiliana kuhusu amani*)**

| Kikisii  | Kiswahili   |
|--|---|
| <p><b>Ondari:</b> Ninki mwanyabanto aranyare gokora bweka ase obogima obo?</p> <p><b>Mokua:</b> (Kicheko) Bosa! Bosa pi! Mwanyabanto takonyara kende gionsi, ngese ense eye ne ya Nyasae</p> <p><b>Ondari:</b> Uuuu! Ee namaene tata. Naende tari nse yoka. Nonya nigoro. Ebuku nigo egoteba nga agwo omochakano Nyasae nigo atongete igoro na nse. Na ense tiyarenge na kieni kende. Ntu mwanyabanto gose nigo twachete aiga totabwati kende.</p> <p><b>Mauti:</b> (Akisafisha koo) eki mwanyabanto atakeire gosaba ase ense eye nomorembe. Nomanyete nga morembe obe toba oo mbosa meremo ende teiyo erakorekane! Onye omonto gotagete gokonyeka saba mono nga: Omorembe obe ase ore <b>na</b> ase enyomba yao</p> | <p><b>Ondari:</b> Ni nini mwanadamu mwenyewe anaweza kufanya katika maisha haya?</p> <p><b>Mokua</b> (Kicheko) Bure! Bure Kabisa! Mwanadamu hawezি chochote, si hii dunia ni ya Mungu!</p> <p><b>Ondari:</b> Uuuu! Ni kweli bwana. Tena si dunia pekee. Hata juu. Bibilia inasema kuwa hapo mwanzo Mungu aliumba mbingu na nchi. Na dunia haikuwa na sura yoyote. Sisi binadamu si tulikuja hapa bila kuwa na kitu.</p> <p><b>Mauti:</b> (Akisafisha koo) anachotakiwa kuomba mwanadamu katika ulimwengu huu ni amani. Unajua kuwa bila ya amani ni bure. Hakuna kazi inayoweza kufanyika! Iwapo mtu unataka kusaidika omba sana kuwa: amani iwe kwako <b>na</b> kwa nyumba yako.</p> |

Omorembe obe ase ore /**na** ase enyomba yao  
 O-morembe o-b-e ase o-re **na** ase e-nyomba ya-o  
 NGL-MZZ NGL-MZZ-MAT MZZ NFS2U **KUM** MZZ NGL-MZZ NGL-NFS2U  
 (Amani iwe kwako na kwa nyumba yako)

**MF5<sup>2</sup>** pia unadhihirisha mwingiliano wa VUM. Katika matini hii kuna LP ya udondoshaji na vilevile U. Katika tungo ya pili ya matini hii, nomino *omorembe* (amani) na T *obe* (iwe) vimedondoshwa. U ‘*na*’ katika matini hii inaunganisha tungo mbili husika: ‘*omorembe obe ase ore*’ (amani iwe kwako) na ‘*omorembe obe ase enyomba yao*’ (amani iwe katika nyumba yako).

### **MF6<sup>11</sup>:**

(Muktadha: Mazungumzo ya kijamii. *Wazungumzaji wawili L na M wanazungumza kuhusu mwenzao ambaye wanadai alienda kutafuta pesa lakini hakuzipata*)

| Kikisii  | Kiswahili   |
|--|---|
| <p><b>L:</b> Mbora ekeene nkeri nga momura ori tanyakogenda korigi besa chyaye?</p> <p><b>M:</b> Nachete agachi korigi chibesa <b>otatiga</b> besa echio tachinyoreti.</p> <p><b>L:</b> Mosuko nanyore. Gincha taku moyo</p> | <p><b>L:</b> Si ukweli ni kuwa kijana yule hajawahi kwenda kutafuta pesa zake?</p> <p><b>M:</b> Alienda kutafuta pesa lakini pesa hizo hakuzipata.</p> <p><b>L:</b> Siku moja atapata mradi tu asife moyo</p> |

Nachete agachi korigi chibesa /**otatiga** besa echio tachinyoreti.

Ni-a-ch-ete a-ga-ch-i ko-rigi chi-besa **o-ti-a-tiga** besa e-chio ti-a-chi-nyor-eti.

KIM-NFS3U-MZZ-MAT NFS3U-SM-MZZ-IT Kat-MZZ NGL-MZZ **KUM**(KIM-KAN-NJ) N KAT-MZZ KAN-NFS3U-NGL-MZZ-K

(Alienda kutafuta pesa lakini pesa hizo hakuzipata)

**MF6<sup>11</sup>** unadhihirisha mwingiliano wa VUM ambavyo ni LP pamoja na U. LP inajitokeza kutokana na urudiaji wa nomino *besa* (pesa). Nomino hii inajitokeza baada tu ya U ‘otatiga’ (isipokuwa). U ‘otatiga’ imetumika kuunganisha tungo mbili za matini hii: ‘nachete agachi korigi chibesa’ (alikuja akaenda kutafuta pesa) na ‘besa echo tachinyoreti’ (pesa hizo hakuzipata).

### **MF7<sup>1</sup>:**

**(Muktadha: Mazungumzo ya kijamii. Wazungumzaji wawili J na K wanazungumza kuhusu mtoto fulani ambaye anasumbuliwa na ugonjwa)**

| Kikisii   | Kiswahili  |
|---|--|
| <p><b>J:</b> Omwana ori bw’omasire bono naki akorokwa?</p> <p><b>K:</b> Timanyeti rieta ryaye ry’ekagusii. Eriegesongo nigo akorokwa John</p> <p><b>L:</b> Omwana ori tata nabwate omoki ase amasomo!</p> <p><b>K:</b> John ngokora are omokia ase esukuru. Obobe, nigo akonya korwara</p> <p><b>L:</b> Nabo nkoiugu nga ngochara orwara...</p> | <p><b>J:</b> Yule mtoto wa Omasire huwa anaitwa nani?</p> <p><b>K:</b> Sijui jina lake la Kikisii. La Kizungu ni Jhn.</p> <p><b>L:</b> Yule mtoto bwana ana bidii katika masomo</p> <p><b>K:</b> John anafanya bidii shulenii ubaya anakuwakuwa mgonjwa</p> <p><b>L:</b> Huwa nasikia kuwa huwa anakuwa mgonjwa...</p> |

John ngokora are omokia ase esukuru. / ***Obobe, nigo akonya korwara***

John ni-go-kor-a a-re o-mokia ase e-sukuru. ***Obobe, nigo a-ko-nya ko-rwar-a***

N KIM-Kat-MZZ-IT NFS3U-MZZ KAT-MZZ H KAT-MZZ. ***KUM KIM NFS3U-Kat-MZZ Kat-MZZ-IT***

(John anafanya bidii shulenii ubaya anakuwakuwa mgonjwa)

Katika **MF7<sup>1</sup>'a**, nomino ‘John’ imedondoshwa kutoka kwa tungo ya pili ya matini hii. Hali hii inadhihirisha kuwepo kwa mshikamano katika matini hii. kipashio ‘*obobe*’ (ubaya) kinajitokeza kuunganisha tungo mbili zinazojitokeza katika matini hii: ‘*John ngokora are omokia ase esukuru.*’ (John anafanya bidii shulen) na ‘*John nigo akonya korwara.*’ (John anakuwakuwa mgonjwa).

### **MF8<sup>1</sup>:**

(Muktadha: *Mazungumzo ya kijamii. Wazungumzaji wawili J na K wanashiriki mazungumzo. Baadaye mtoto mdogo anaanza kulia karibu na walipo. j anakaripia kuwa mtoto huyo anapenda kulia bila sababu*)

| Kikisii  | Kiswahili   |
|--|---|
| <p><b>J:</b> Ee nabo nsinyire nga ninki Atari<br/>koimokerera igoro nere akore emeremo<br/>buna abanto bande!</p> <p><b>K:</b> Otagotiga aye! twachire komoira ngora<br/>(<i>mtoto anatokeza kutoka njiani akiwa analia</i>) Omwana oyu nigo anarete<br/>bobe. Mono nigo<br/>anchete korera bosa (<i>kwa sauti ya ukali</i>) Kira kiri agaisi aka!</p> | <p>J: Ee ndiyo nashindwa mbona naye asisimame<br/>afanye kazi kama watu wengine</p> <p>K: Isipokuwa wewe! Tumejaribu kumpeleka<br/>polepole (<i>mtoto anatokeza kutoka njiani akiwa analia</i>) mtoto huyo amezoea vibaya.<br/>Zaidi anapenda kulia bure (<i>kwa sauti ya ukali</i>) Nyamaza kimya wewe kavulana.</p> |

- a) Omwana oyu nigo anarete bobe. / ***Mono nigo anchete korera bosa***  
**O-mw-ana o-yu nigo a-nar-ete bobe. *Mono nigo a-nch-ete ko-rer-a bosa***  
 KAT-IDU-MZZ NGL-MZZ KIM NFS3U-MZZ-MAT E. **KUM KIM NFS3U-MZZ-MAT Kat-MZZ-IT E**  
 (Mtoto huyo amezoea vibaya. Zaidi anapenda kulia bure)

Sawa na ilivyo katika **MF7<sup>1</sup>'a**, katika **MF8<sup>1</sup>'a**, kuna mwilingiano wa VUM. Mwingiliano huu unadhihirisha kuwepo kwa LP na vilevile U katika matini moja. Katika tungo ya pili ya **MF8<sup>1</sup>'a**, kumedondoshwa KN ‘omwana oyu’ (mtoto huyo). Kipashio ‘mono’ (sana)

kinachojitokeza katika matini hii kinatekeleza dhima ya uunganishaji wa tungo mbili husika katika matini hii. Hizo ni: ‘*Omwana oyu nigo anarete bobe*’ (mtoto huyo amezoea vibaya) na ‘omwana oyu nigo anchete korera bosa’. Kinachodhihirika hapa ni kuwa mwingiliano wa VUM hivi ndio unafanikisha mshikamano katika matini husika.

### **MF11<sup>8</sup>:**

**(Muktadha: Mazungumzo ya kijamii. J na K wanazungumza kuhusu jamaa fulani mwenye hasira)**

| Kikisii   | Kiswahili   |
|---|---|
| <p><b>J:</b> Omoisi ori nabo abwato obomwenu<br/>boisaine</p> <p><b>K:</b> Ori ekero okomokani egento nari bono<br/>okomotebi agekore. Gose moisonde<br/>naaka omonto obande bosabosa!</p> <p><b>J:</b> John igo amokaneti. <b>Bono ekero</b><br/>amotebi atige, akamanya koimoka<br/>nekerundo akamongwani<br/>oro. Mosuko naikere ayaye....</p> | <p><b>J:</b> Yule kijana una ujeuri mwangi</p> <p><b>K:</b> Yule unapomkataza kitu ndio unamwambia<br/>akifanye. Si juzi alipiga mtu wa wenyewe<br/>bure bure!</p> <p><b>J:</b> John alimkataza. <b>Sasa wakati</b> alimwambia<br/>aache, akatoka mbio akamzaba kofi. Siku<br/>moja atakumbana na yake.....</p> |

John igo amokaneti. / **Bono ekero** amotebi atige, akamanya koimoka nekerundo  
akamongwani oroe.

John igo a-mo-kan-eti. **Bono ekero** a-mo-teb-i a-tig-e, a-ka-many-a ko-imok-a na-e-ke-  
rundo a-ka-mo-ngwani o-roe.

N KIM NFS3U-SH-MZZ-MAT. **KUM(E E)** NFS3U-SH-MZZ-IT NFS3U-SM-MZZ-IT Kat-MZZ-IT H-KAT-NGL-MZZ  
NFS3U-SM-SH-MZZ KAT-MZZ

(John alimkataza. Sasa wakati alimwambia aache, akatoka mbio akamzaba kofi)

Katika **MF11<sup>8</sup>** kuna mwingiliano wa VUM. Katika mfano huu, LP pamoja na U vimeingiliana. Katika utungo wa kwanza wa matini hii kumetumika kitenzi ‘amokaneti’ (alimkataza). Katika utungo wa pili, kitenzi hicho kimerudiwa kwa kisawe ambacho ni ‘amotebeti atige’ (amwambie aache). Hii inadhihirisha kuwepo kwa LP. Katika utungo huo wa pili, kumejitokeza pia U ‘**bono**’ na U ‘**ekero**’ mwingiliano wa LP na U katika matini hii umefanikisha mshikamano katika matini hii na hivyo kuwezesha upatanifu.

### **MF9<sup>5</sup>:**

*(Muktadha: Mazungumzo ya kijamii. wazungumzaji G na H wanazungumza kuhusu mama fulani ambaye alikuwa mlevi wa kupindukia)*

| Kikisii   | Kiswahili  |
|---|--|
| <p><b>G:</b> N’amaene bono ogokwana? Omongina ori tarikororekana gose nabwate mangana.</p> <p><b>H:</b> Omongina ori nigo atoreka. <b>Magega yayu</b> nigo arenge konyu amaru amange mono. Tiga arakanyeka konyora oetaniri ekerengo.</p> | <p><b>G:</b> Unasema ukweli? Mama yule haonekani kuwa na maneno.</p> <p><b>H:</b> Mama Yule aliokoka. <b>Kabla ya hapo</b> alikuwa anakunywa pombe nyingi mno. Acha apoe alikuwa amezidi</p> |

Omongina ori nigo atoreka. **Magega yayu** nigo arenge konyu amaru amange mono.

O-mo-ngina o-ri nigo a-torek-a. **Magega yayu** nigo a-renge ko-nyu amaru a-mange mono.

KAT-IDU-MZZ NGL-MZZ KIM NFS3U:NJ-MZZ-IT. **KUM(H-W)** KIM NFS3U-MZZ Kat-MZZ N NGL-MZZ V

(Mama Yule aliokoka. Kabla ya hapo alikuwa anakunywa pombe nyingi mno)

**MF9<sup>5</sup>** unadhihirisha hali ambapo mshikamano katika matini unafanikishwa na kuwepo na VUM LP pamoja na U katika matini moja. LP imetokana na kudondoshwa kwa KN (omongina ori) kutoka kwa tungo ya pili katika matini hii. Aidha, kumejitokeza U ambacho ni ‘magega yayu’ kimetumika kuwezesha mshikamano baina ya tungo ‘omongina ori nigo atoreka’ (mama yule aliokoka) na ‘omongina ori nigo arenge konyu amaru amange mono’ (mama yule alikuwa anakunywa pombe nyingi mno).

**MF9<sup>6</sup>:**

**(Muktadha: Mazungumzo ya kijamii. Wasailiwa wanazungumza kuhusu mwalimu fulani ambaye wanadai hakuwa akiwafundisha walipokuwa shulen)**

| Kikisii   | Kiswahili  |
|---|--|
| <p><b>K:</b> Tiga kongainereri tata! Mwarimu oyu tatosometi. <b>Ase ekeene</b>, igo asoete ekerasi gatato rioka. Bono oyu n'omonto oratebe nga natosometi. Omonto ori n'omworo bobe.</p> <p><b>J:</b> Ebe nasoete rimo gose gatato buna ogoteba igo nga tatosometi?</p> | <p><b>K:</b> Acha kudanganya bwana! Huyo mwalimu hakutufundisha <b>Kwa hakika</b> aliingia darasani mara tatu tu. Sasa huyo ni mtu utasema kuwa alitufundisha. Yule mtu ni mzembe vibaya.</p> <p><b>J:</b> Iwe alilingia mara moja au maratati kama unavyosema hivyo hakutufundisha?</p> |

Mwarimu oyu tatosometi. /*Ase ekeene, igo asoete ekerasi gatato rioka.*

Mw-arimu o-yu ti-a-nya-go-to-som-i. **Ase e-ke-ene** igo a-so-ete e-ke-rasi ga-tato ri-oka.

IDU-MZZ NGL-MZZ KAN-NJ-NFS3U-KAT-SH-MZZ-IT. KUM(H-KAT-NGL-MZZ) KIM NFS3U-MZZ-MAT KAT-IDU-MZZ NGL-MZZ NGL-MZZ

(Mwalimu huyo hakutufunza. Kwa hakika aliingia darasani mara tatu tu.)

Mwingiliano wa VUM pia unadhihirika katika matini hii - **MF9<sup>6</sup>**. Katika matini hii, LP inajitokeza kutokana na kudondoshwa kwa KN (mwarimu oyu) kutoka kwa tungo ya pili ya matini hii. ‘*Ase ekeene*’ imetumika katika matini hii ili kuwezesha mshikamano baina ya tungo mbili za matini hii ambazo ni: ‘*Mwarimu oyu tatosometi*’ (mwalimu huyo hakutufunza) na ‘*igo asoete ekerasi gatato rioka*’ (aliingia darasani mara tatu tu).

**MF10<sup>2</sup>:**

(Muktadha: Mazungumzo ya kijamii. *Mtafiti anashiriki mazungumzo na rafiki zake kuhusu watoto wa mitaani. Mmoja wa rafiki zake anaeleza jinsi ambavyo watoto hao huweza kula au kunywa chochote bila ya kuathirika.*)

| Kikisii  | Kiswahili   |
|--|---|
| <p><b>Mtafiti:</b> Abana bari nNyasae obarendete</p> <p><b>J:</b> (Akimkatiza) Naende Nyasae igo abanchete mono</p> <p><b>K:</b> Abana aba ba chokora nigo bakori kende gionsi. Komenta nayu igo bakonyu mache ande onsi aba tibari korwara. Aye omochani ori endagera bakori igo ogokorera nyagetari.</p> <p><b>J:</b> Amaene pi!....</p> | <p><b>Mtafiti:</b> Watoto wale ni Mungu anawalinda</p> <p><b>J:</b> (Akimkatiza) Tena Mungu anawapenda sana</p> <p><b>K:</b> Watoto hawa wa chokora wanakula chochote. Pamoja na hayo wanakunywa maji yoyote ingawa hawaii wagonjwa. Wewe ukijaribu ule chakula wanachokula utaishia hospitali.</p> <p>J: Kweli kabisa! .....</p> |

Abana aba ba chokora nigo bakori kende gionsi. /**Komenta nayu igo bakonyu mache ande onsi aba tibari korwara**

A-ba-na a-ba ba chokora nigo ba-ko-ri kende gi-onsi. **Ko-ment-a na-yu** igo ba-ko-nyu mache a-nde o-nsi aba ti-ba-ri ko-rwara

NGL-IDW-MZZ NGL-MZZ H N KIM IDW-Kat-MZZ V NGL-MZZ. **KUM**(Kat-MZZ-IT H-W) KIM IDW-Kat-MZZ N NGL-MZZ NGL-MZZ U KAN-IDW-MZZ Kat-MZZ

(Watoto hawa wa chokora wanakula chochote. Pamoja na hayo wanakunywa maji yoyote ingawa hawaii wagonjwa)

Katika **MF10<sup>2</sup>** vilevile kunajitokeza mwilingiliano wa VUM. Katika matini hii LP imejitokeza kutokana na udondoshwaji wa KN ‘abana aba ba chokora’ (watoto hawa wa chokora). KN hili limedondoshwa kutoka kwa tungo ya pili ya matini hii. ‘Komenta nayu’ ambayo imedhihirika katika matini hii imetumika kama U. VUM hivi viwili vimeingiliana na kukamilishana katika matini hii na kwa njia hiyo kufanikisha mshikamano baina ya tungo mbili husika katika matini hii. Tungo hizi ni: ‘*Abana aba ba chokora nigo bakori kende gionsi*’ (Watoto hawa wa chokora wanakula chochote) na

*'Abana aba ba chokora igo bakonyu mache ande onsi aba tibari korwara'* (Watoto hawa wa chokora wanakunywa maji yoyote ingawa hawawi wagonjwa).

### MF10<sup>8</sup>:

(Muktadha: Darasani. *Mwanafunzi mmoja anawahimiza wenzake kusoma kwa bidii. Anawatolea kisa cha mvulana ambaye alikuwa akicheza na masomo*)

| Kikisii   | Kiswahili   |
|---|---|
| Timonya gokora egosori namasomo. Omogano oyu nabaa nabo oisane kobaoroki obobe bwogokora egosori ase amasomo. Omomura ori nigo akorete egosori ase amasomo.<br><b>Kobwatekani naywo</b> takoreti buya ase amatemu ..... | Msiwe mkifanya mchezo na masomo. Hadithi hiyo ambayo nimewapa unatosha kuwaonyesha ubaya wa kufanya mchezo masomoni. Mvulana yule alifanya mchezo katika masomo.<br><b>Kuambatana na hayo</b> hakufanya vizuri katika mitihani..... |

Omomura ori nigo akorete egosori ase amasomo. /**Kobwatekani naywo** takoreti buya ase amatemu

O-mo-mura o-ri nigo a-kor-ete e-gosori ase a-masomo. **Ko-bwatekani na-aywo** ti-a-kor-eti buya ase a-ma-temu

KAT-IDU-MZZ NGL-MZZ KIM NFS3U-MZZ-MAT KAT-MZZ H NGL-MZZ. **KUM**(Kat-MZZ H-MZZ) KAN-NFS3U-MZZ-K E H NGL-IDW-MZZ

(Mvulana yule alifanya mchezo katika masomo. Kuambatana na hayo hakufanya vizuri katika mitihani)

**MF10<sup>8</sup>**, ni mfano mwinine unaodhihirisha mwingiliano baina VUM. Katika **MF10<sup>8</sup>** kumedhihirika kuingiliana kwa LP na U. LP inayodhihirika katika matini hii ni ya udondoshaji wa KN '*omomura ori*' (mvulana yule) ambayo imedondoshwa kutoka kwa tungo ya pili ya matini hii. U '*kobwatekani naywo*' (kufuatana na hayo) kimetumika kuunganisha tungo mbili za matini hii: '*Omomura ori nigo akorete egosori ase*

*amasomo*' (Mvulana yule alifanya mchezo katika masomo) na '*Omomura ori takoreti buya ase amatemu*'. (Mvulana yule hakufanya vizuri katika mitihani).

### MF10<sup>9</sup>:

(**Muktadha:** *Mazungumzo ya kijamii. J na K wanashiriki mazungumzo huku wakiwa wanamangoja mwenzao ambaye amekawia. k anahoji kuwa huenda wanayemsubiri asije kwa kuwa amekawia*)

| Kikisii  | Kiswahili  |
|--|--|
| <p><b>J:</b> Chinsa echu chiachire mono. Gochi nkoira bogochi. Ntochetokore emeremo eye bori?</p> <p><b>K:</b> Tindochi tokonyekora</p> <p><b>J:</b> Igo tokogenda gose toramoganya ake?</p> <p><b>K:</b> Mokua onyoriru mono <b>oranyore</b> tari gocha. Omanyete nabo ankorete iga rinde nkamoganya nkaganyora naende nomokora omororo. Tari monto morachikane nga ngokora more gento nere aikerani.</p> | <p><b>J:</b> Hizi saa zimekwisha sana. Hata kunaelekea kuwa usiku. Tutafanya hii kazi kweli?</p> <p><b>K:</b> Sioni tukiifanya</p> <p><b>J:</b> Twende au tumsubiri kidogo?</p> <p><b>K:</b> Mokua amechelewa mno huenda haji. Unajua alinifanya hivi wakati fulani nikamsubiri nikachoka, tena ni mkora ajabu. Sio mtu mnawenza kuahidiana naye kuwa mnafanya kitu naye aafikie</p> |

Mokua onyoriru mono. /**Nabo oranyore tari gocha**

Mokua o-nyor-iru mono. **Nabo o-ra-nyor-e** ti-a-r-i go-ch-a

N NFS2U-MZZ-K E. **KUM**(KIM NFS2U-K-MZZ-K) KAN-NFS3U-MZZ-IT Kat-MZZ-IT

(Mokua amechelewa sana. Unaweza kupata haji)

Kama ilivyojitokeza katika **MF10<sup>8</sup>**, **MF10<sup>9</sup>** pia unadhihirisha hali ya mwingiliano wa VUM katika matini semwa za kiKisii. Katika **MF10<sup>9</sup>** kunabainika LP inayotokana na kudondoshwa kwa nomino Mokua kutoka kwa tungo ya pili ya matini husika. Aidha, U 'nabo oranyore' nacho kimetumika ili kuwezesha mshikamano baina ya '*Mokua onyoriru mono*' (Mokua amechelewa sana) na '*Mokua tari gocha*' (Mokua haji)

**MF15<sup>2</sup>:**

(Muktadha: Mazungumzo ya kijamii. *G na H wanashiriki mazungumzo kuhusu uchawi*)

| Kikisii   | Kiswahili  |
|---|--|
| <p><b>G:</b> Ekero kwairu, obibwate, nkomanyore nga kwabienanire?</p> <p><b>H:</b> Yaya! Naye oyo okoete tomanyeti gose nomonto omonene <b>gose</b> nomwana</p> <p><b>G:</b> (Akirejelea mada ya awali) bono omwana oyu nachete akaba buya?</p> <p><b>H:</b> Buya? Omwana akabwata akagireka. Ngakura gose ngakura. Onde achi kongebereri nkire, mmobori nga: ‘Torochi igo akwete chinsa isano; koru chinsa echo goika marogoba naende goika marogoba ende.’.....</p> | <p><b>G:</b> Wakati umepewa, unavyo, unajua kuwa umepewa?</p> <p><b>H:</b> Hapana! Nawe aliyekupa hujui ikiwa ni mtu mzima <b>au</b> ni mtoto</p> <p><b>G:</b> (Akirejelea mada ya awali) sasa huyo mtoto alikuja akawa vizuri?</p> <p><b>H:</b> Vizuri? Mtoto akazirai. Nikapiga nduru. Yeyote akinibembeleza ninyamaze, ninamuuliza: ‘Huoni alikufa saa tano; Tangu saa hizo hadi jioni tena hadi jioni nyingine...’</p> |

Naye oyo okoete tomanyeti gose nomonto omonene **gose** nomwana

Ni-aye oyo o-ko-e-ete ti-o-many-eti gose ni-o-mo-nto o-mo-nene **gose** ni-o-mw-ana

KIM-MZZ MZZ NGL-Kat-MZZ-MAT KAN-NFS2U-MZZ-MAT U KIM-KAT-IDU-MZZ KAT-IDU-MZZ U KIM-KAT-IDU-MZZ

(Nawe aliyekupa hujui ikiwa ni mtu mzima au ni mtoto)

**MF15<sup>2</sup>** unadhihirisha mwingiliano baina ya VUM ambapo LP imeingiliana na U. LP katika **MF15<sup>2</sup>** imetokana na kudondoshwa kwa kitenzi kutoka kwa tungo ya pili ya matini husika. Kitensi kilichodondoshwa ni ‘*okoete*’ (aliyekupa). Katika matini hii pia kunadhihirika U ‘*gose*’ (au). U hiki kimeingiliana na LP lili kufanikisha mshikamano katika matini hii.

**MF15<sup>3</sup>:**

**(Muktadha: Mazungumzo ya kijamii. P na Q wanajadiliana kuhusu mama fulani mzee aliye kuwa na sifa nzuri katika kijiji chao)**

| Kikisii  | Kiswahili  |
|--|--|
| <p><b>P:</b> Nigo anchete obochenu.</p> <p><b>Q:</b> Omongina oyu nigo arenge gwasibi oraba.<br/><b>neba nga</b> mmogondo agochi. Otagotiga<br/>aye ....</p> | <p><b>P:</b> Anapenda usafi</p> <p><b>Q:</b> Ajuba huyo alikuwa akioga anangara. <b>Hata ikiwa</b> ni shambani anaenda</p> |

- a) Omongina oyu nigo arenge gwasibi oraba. /**neba nga mmogondo agochi**.

O-mo-ningina oyu nigo a-renge go-esibi o-rab-a. **Na-e-b-a** nga m-mogondo a-go-ch-i.

KAT-IDU-MZZ MZZ KIM NFS3U-MZZ Kat-MZZ NFS2U-MZZ-IT. KIM-NGL-MZZ-IT KIM KIM-MZZ  
NFS3U- Kat-MZZ-IT

(Ajuba huyo alikuwa akioga anangara. Hata ikiwa ni shambani anaenda)

**(Muktadha: Mazungumzo ya kijamii. Wazungumzaji wawili James na Mikuro wanazungumza juu ya mwenzao aliyenunua shamba)**

| Kikisii  | Kiswahili  |
|--|--|
| <p><b>James:</b> Ori n'omonto bwebanete</p> <p><b>Mikuro:</b> Aba nonya nigo nomokora are</p> <p><b>James:</b> Ee nomokora! Ndire angainete bobo</p> <p><b>Mikuro:</b> (kwa mshangao) naki akongainete</p> <p><b>James:</b> Igo angainete nga abana baye noo bamenyete ase oboremo obu bwaye. Nkegena bo omogambi. Nkaba engaki entabe totanya koumerana. Engaki eyemo enachiete nkanyora nga n'oborimo pi; Enachiete nkanyora ani abana abu baye tibamenyeti oo</p> <p><b>Mikuro:</b> oranyore natatagete omanye ase bamenyete.</p> <p><b>James:</b> Ninki bono narenge kobakorera nimanya ase bamenyete.</p> | <p><b>James:</b> Yule ni mtu amejipanga</p> <p><b>Mikuro:</b> Ingawa hata hivyo ni mkora</p> <p><b>J:</b> Ee ni mkora! Kuna wakati alinidanganya vibaya</p> <p><b>Mikuro:</b> (Kwa mshangao) alikudanganyaje?</p> <p><b>James:</b> Alinidanganya kuwa watoto wake wanaishi katika hilo shamba lake. Nikaamini hivyo mzee. Ikawa muda mrefu bila ya kukutana naye. Siku moja nilienda nikapata kuwa ni uongo kabisa; nilienda nikapata kumbe watoto hao wake hawaishi hapo.</p> <p><b>Mikuro:</b> Unaweza kupata hakutaka ujue mahali</p> |

|  |  |
|--|--|
| <p><b>Mikuro:</b> Mmmm. Nere okonya<br/>gwechanda bosa.</p> <p><b>James:</b> Tari gotaka gotebi monto keene.</p> <p><b>Neba</b> ninche</p> | <p>wanaishi</p> <p><b>James:</b> Sasa ningewafanya nini hata ningejua<br/>wanakoishi.</p> <p><b>Mikuro:</b> Mmmm. Ni ye ye anajisumbua bure<br/>James: huwa hataki kuambia mtu<br/>ukweli. <b>Hata ikiwa ni mimi</b></p> |
|--|--|

- b) Tari gotaka gotebi monto keene. /**Neba** ninche

Ti-a-r-i go-tak-a go-teb-i mo-nto keene. Na-e-ba ni-nche  
KAN-NJ-MZZ-IT Kat-MZZ-IT Kat-MZZ-IT IDU-MZZ N. KIM-NGL-MZZ NFS1U-MZZ  
(Huwa hataki kuambia mtu ukweli. Hata ikiwa ni mimi)

Katika **MF15<sup>3'a</sup>** na **MF15<sup>3'b</sup>**, kuna mwingiliano wa VUM unaotokana na kuingiliana kwa LP na U. Katika **MF15<sup>3'a</sup>** **kishazi** ‘*Omongina oyu nigo arenge gwasibi oraba*’ (mama huyo alikuwa akioga anangara) kimedondoshwa kutoka kwa tungo ya pili ya matini hii. Katika **MF15<sup>3'b</sup>**, ‘*tari gotaka gontebi keene*’ (huwa hapendi kuniambia ukweli). Kama inavyobainika katika **MF15<sup>3'a</sup>** na **MF15<sup>3'b</sup>**, ‘*neba*’ (hata ikiwa) imetumika katika matini hizi mbili ili kufanikisha mshikamano katika tungo husika za matini hizi mbili.

## 4.2 Mwingiliano wa U na U

**MF6<sup>11</sup>:**

(Muktadha: *Mazungumzo ya kijamii. Mtafiti anashiriki mazungumzo na mzee fulani kuhusu umuhimu wa masomo. Mzee huyo anasimulia kuhusu mzee mwingine ambaye alikuwa mwanafunzi*)

| Kikisii  | Kiswahili   |
|--|---|
| <p><b>Mtafiti:</b> Amatuko aya nonya nabagaka ngosoma bare</p> <p><b>Momanyi:</b> Naboigo aye tata. Nnanyora omogaka gete omogotu mono ogosoma. Otatiga omanyete bagaka buna abu tibari gokora buya ase amasomo.</p> | <p><b>Mtafiti:</b> Siku hizi hata wazee wanasoma</p> <p><b>Momanyi:</b> Ni hivyo bwana. Nilipata mzee fulani aliyezeeka mno akisoma. Ila unajua wazee kama hao huwa hawafanyi vizuri katika masomo.</p> |

Nnanyora omogaka gete omogotu mono ogosoma. /*Otatiga omanyete bagaka buna abu tibari gokora buya ase amasomo.*

Ni-na-nyor-a o-mo-gaka gete o-mo-gotu mono o-go-som-a. **Otatiga** o-many-ete ba-gaka buna a-bu ti-ba-r-i go-kor-a buya ase a-ma-somo.

KIM-NFS1U-MZZ-IT KAT-IDU-MZZ V KAT-IDU-MZZ NGL-Kat-MZZ-IT. **KUM** NGL-MZZ-MAT IDW-MZZ E NGL-MZZ KAN-NGL-MZZ-ITKAN KAT-MZZ-IT H KAT-NGL-MZZ

(Nilipata mzee fulani aliyezeeka mno akisoma. Ila unajua wazee kama hao huwa hawafanyi vizuri katika masomo)

**MF6<sup>11</sup>** unadhihirisha mwingiliano hivi kwamba U mbili tofauti zinaingiliana. Katika matini hii, U ‘*otatiga*’ (ila) pamoja na U ‘*omanyete*’ (unajua) zimeingiliana na hivyo kukamilisha mshikamano baina ya tungo mbili husika katika matini hii. Tungo hizo ni: ‘*Nnanyora omogaka omogotu mono ogosoma*’ (Nilipata mzee fulani aliyezeeka mno akisoma) na ‘*omanyete bagaka buna abu tibari gokora buya ase amasomo*’ (Unajua wazee kama hao huwa hawafanyi vizuri katika masomo). Katika hali kama hii, inadhihirika kuwa U ‘*otatiga*’ (ila) ndicho kikuu na ‘*omanyete*’ (unajua) inajitokeza tu kama kipashio kilicho na dhima ya kukamilisha U kikuu ambacho ni ‘*otatiga*’. Hata

hivyo ni vyema ifahamike kuwa hali hii hutokea pale tu ambapo kunajitokeza viunganishi viwili katika msururu.

### **MF8<sup>5</sup>:**

**(Muktadha: Darasani. *Mwanafunzi mmoja anasimulia hadithi kuhusu mtoto fulani ambaye mjomba wake alikataa kumlipia karo*)**

| Kikisii   | Kiswahili   |
|---|---|
| ‘...omwana ori akagenda ase isemoke komosaba amokonye ebesa achiere esukuru. Nomanyete isemoke oyu akanga pi komokonya! Akamokani nga tabwati besa aramoakanere sukuru. Erio manya nigo abwate chibesa akoa abanto babande bosa.’ | ‘.....Mtoto yule akaenda kwa mjomba wake kumwomba fedha aendee shule. unajua mjomba wake huyo alikataa kabisa kumsaidia! Akamkataza kuwa hana pesa anazoweza kumlipia shulen. Hivyo jua ana pesa anazowapa watu wa wenyewe bure.’ |

Akamokani nga tabwati besa arangakanere sukuru. / **Erio** manya nigo abwate chibesa akoa abanto babande bosa.

A-ka-mo-kan-i nga ti-a-bwa-ti besa a-ra-ni-akan-ere sukuru. **Erio** many-a nigo a-bwa-te chi-besa a-ko a-ba-nto ba-band bosa.

NFS3U-SM-SH-MZZ-IT U KAN-NFS3U-MZZ-KTK N NFS3U-NJ-SH-MZZ-K N. **KUM** MZZ-IT KIM NFS3U-MZZ-MAT NGL-MZZ NFS3U-MZZ NFS3U-IDW-MZZ H-MZZ E

(Akamkataza kwamba hana pesa anazoweza kunilipia shulen. Hivyo jua ana pesa anazowapa watu wa wenyewe bure)

Vipashio ‘erio’ na ‘manya’ ambavyo vinafanya kazi kama viunganishi katika matini hii, vinaingiliana na kukamilishana katika matini hii ili kukamilisha mshikamano. Kama ilivyodhihirika katika **MF6<sup>11</sup>**, katika **MF8<sup>5</sup>** kunajitokeza kuwepo na U kikuu ambacho ni ‘erio’ pamoja na U kinachotekeleza kazi ya kukamilisha U kikuu ambacho ni manya. Viunganishi hivi viwili vimetumika kwa pamoja ili kukamilisha mshikamano katika matini husika.

#### **4.3 Hitimisho**

Katika sura hii imebainika kuwa VUM mbalimbali huweza kuingiliana na kukamilishana katika matini semwa mbalimbali za Kikisii. Kutokana na uchanganuzi uliofanywa katika sura hii, ilibainika kuwa kuna mwingiliano wa VUM mbalimbali katika matini semwa za Kikisii. Mwingiliano mkubwa uliojitokeza ni ule wa LP na U na vilevile U na U. Ilibainika kuwa mwingiliano baina ya VUM hivi katika matini semwa za Kikisii huwezesha mshikamano. Ni dhahiri kama ilivyojitokeza katika sura hii kwamba mwingiliano mkubwa wa VUM katika matini semwa za Kikisii hujitokeza baina ya VUM U na LP za udondoshaji. LP za uradidi huingiliana na VUM U kwa kiwango kidogo. Mwingiliano na kukamilishana kwa VUM katika matini semwa za Kikisii huchangai pakubwa katika kufanikisha mshikamano katika matini hizo.

## SURA YA TANO

### **AMALI ZINAZOTEKELEZWA NA VIJENZI UNGANISH VYA MSHIKAMANO**

#### **5.0 Utangulizi**

Katika sura hii kumefanywa uchambuzi wa amali mbalimbali ambazo zinatekelezwa na VUM katika matini semwa za Kikisii. Kando na kuonyesha jinsi VUM hufanikisha mshikamano katika matini za Kikisii, sura hii inachunguza na kuweka wazi amali nyingine ambazo zinatekelezwa na VUM.

#### **5.1. Mrejeo sawa**

Moja kati ya amali zinazotekelezwa na VUM kando na mshikamano ni ufanuzi. Utafiti huu ulibaini kuwa VUM huweza kutekeleza amali ya kutoa ufanuzi kuhusu suala ambalo linalengwa na msemaji. Ufanuzi unaweza kufanikishwa kwa njia mbili: matumizi ya mrejeo sawa na kwa utoaji mfano. Mrejeo sawa hujitokeza pale ambapo msemaji analazimika kutoa kauli nyingine ili kutoa ufanuzi wa kauli aliyokwisha kutoa awali na ambayo anahisi haikuelewaka vyema

##### **a) Maelezo**

###### **MF19:**

**(Muktadha: Mazungumzo ya kijamii. *Mzungumzaji F anamweleza G tabia za mtoto wake ambaye ni mtukutu*)**

| Kikisii  | Kiswahili   |
|--|---|
| <b>G:</b> Otarochi buya omwana oyo<br>nkogosinya are pi. Igo agocha kogera<br>orere amariga. | <b>G:</b> Usipochunga huyo mtoto atakushinda<br>kabisa. Atakufanya ulie machozi.<br><b>H:</b> Hebu niambie nifanye nini? Nimejaribu |

|  |  |
|--|--|
| <p><b>H:</b> Ntebingo ninki ngokora? Natemire komokanya tari koigu. Goikera abu, timbwati ekio ndatebe. Ense nero erache komogambera. Abagusii ebagoteba gambera omuya .....</p> <p><b>G:</b> Igo nabo otagete agendere koba igo buna are?</p> <p><b>H:</b> Nche namokwaneire tatageti koigu. Ase bono iga, nesabire amagoko ane. Tiga ere akore buna atagete.....</p> <p><b>G:</b> Tokomobuchri rende emeremo egere ekeani amanga aya abwate amange:</p> <p><b>H:</b> Mwana oyu tancheti gokora kende. Ase enchera ende oku nogoteba nga omwana oyu nomworo. Togwancha ningotebi nga ebyo bionsi natemire.....</p> <p><b>G:</b> (Akimkatiza) Bana tibatakeiri gotigeru ibaga. <b>Eki ngoteba nkeri nga</b> abana igo batakeire korendu tibabasi gosari ebikoru.....</p> | <p>kumkanya hasikii. Kufikia hapo sina cha kusema. Ulimwengu utamrudi. Wakisii wanasema mkanye mwema .....</p> <p><b>G:</b> Hivyo unataka aendelee kuwa jinsi alivyo?</p> <p><b>H:</b> Mimi nimemzungumzia hataki kusikia. Kwa sasa, nimenanwa mikono yanguu. Acha afanye anavyotaka</p> <p><b>G:</b> Si basi umpe kazi nydingi ili impunguzie haya maneno mengi aliyo nayo</p> <p><b>H:</b> Mtoto huyo hapendi kufanya chochote. Kwa njia nydingine, mtoto huyo ni mvivu. Hutakubali hata nikikwambia kuwa nimejaribu hivyo vyote</p> <p><b>G:</b> (Akimkatiza) Watoto hawatakiwi kuachiwa nafasi. <b>Ninachosema ni kuwa</b> watoto wanatakiwa kulindwa wasije wakaharibu tabia.....</p> |
|--|--|

- a) Bana tibatakeiri gotigeru ibaga. */Eki ngoteba nkeri nga abana igo batakeire korendu tibabasi gosari ebikoru biabo*  
 Ba-ana ti-ba-tak-eiri go-tig-eru i-baga. **Eki ngoteba nkeri nga** a-ba-ana igo ba-tak-eire ko-rend-u ti-ba-basi go-sari e-bi-koru bi-abo  
 IDW-MZZ KAN-IDW-MZZ-K Kat-MZZ-K IDU-MZZ **KUM** NGL-IDW-MZZ KIM IDW-MZZ-K Kat-K KAN-IDW-MZZ Kat-MZZ NGL-IDW-MZZ NGL-MZZ  
 (Watoto hawatakiwi kupewa nafasi ninachosemea hivyo ni kuwa watoto wanatakiwa kulindwa wasije kuharibu tabia zao)

**(Muktadha: Mazungumzo ya kijamii. F anamweleza G kuhusu ubaya wa sukari na namna mgonjwa wa sukari anatakiwa kujilinda)**

| Kikisii  | Kiswahili  |
|--|--|
| <p><b>G:</b> Nga bono obo noburwaire bwesukari?</p> <p><b>F:</b> Ee. Nabo bore igo</p> <p><b>G:</b> Aaa! Nobobe. Tibobwati riogo</p> <p><b>F:</b> Igo nogoteba nga totige konyu esukari?</p> <p><b>G:</b> Ee baba. Sukari teri ngiyaekiagera nigo eroseiri ebinto ebibe.</p> <p><b>F:</b> Ayeeee!! Igo agwetonga esindani ere omonyene?</p> <p><b>G:</b> Ee. Ekero kwarwarire igo okweegeria gwetonga</p> <p><b>F:</b> Nyasae one!!</p> <p><b>G:</b> Notakeire kweegeria gwetonga esindani. <b>Eki ngotebera bo nkeri nga</b> onde taiyo ogocha konya kogotonga sindani.</p> | <p><b>G:</b> Eti sasa huu ni ugonjwa wa sukari?</p> <p><b>F:</b> Ee. Uko hivyo</p> <p><b>G:</b> Aaa! Ni mbaya. Hauna dawa.</p> <p><b>F:</b> Hivyo ni kusema kuwa tuache kunywa sukari?</p> <p><b>G:</b> Ee <i>baba</i>. Sukari si nzuri kwa kuwa imetengenezewa vitu vibaya</p> <p><b>F:</b> Ayeeee!! Anajidunga sindano yeye mwenyewe?</p> <p><b>G:</b> Ee. Wakati umekuwa mgonjwa unajifunza kujidunga</p> <p><b>F:</b> Mungu wangu!!</p> <p><b>G:</b> Unatakiwa kujifunza kujidunga sindano. <b>Kinachonifanya niseme hivyo ni kuwa hakuna mtu ambaye atakuwa akikudungadunga sindano</b></p> |

- b) Notakeire kweegeria gwetonga esindani. **/Eki ngotebera bo nkeri nga onde taiyo ogocha konya kogotonga sindani.**  
 Ni-o-tak-eire ko-e-egeria go-e-tong-a e-sindani. **Eki ngotebera bo nkeri nga** o-nde ti-ai-  
 iyo o-go-ch-a ko-nya ko-go-tong-a sindani.  
 KIM-NFS2U-MZZ-K Kat-Kj-MZZ Kat-Kj-MZZ-IT IDU-MZZ **KUM** NGL-MZZ KAN-NJ-MZZ NGL-Kat-MZZ-IT Kat-  
 NFS2U-MZZ-IT N  
 (Unatakiwa kujifunza kujidunga sindano. Kinachonifanya kusema hivyo ni kuwa hakuna  
 mtu atakuwa akikudungadunga sindano)

Katika **MF19a** pamoja na **MF19b** kumetumika KUM '**Eki ngotebera bo nkeri nga**'.

KUM hiki kando na kufanikisha mshikamano katika matini ambamo kimetumika,  
 kinatimiza amali ya kutoa maelezo. Habari zinazotokeza baada ya KUM hiki zinabainika  
 kuwa zinazotoa habari zaidi kuhusu tungo zilizotangulia katika matini hizo husika.

Msemaji katika matini hii anatoa maelezo kuhusu ni nini kilichomfanya kutoa tungo tangulizi katika matini hizi. Katika **MF19b** kwa mfano, anaeleza kuwa sababu iliyomfanya kumwambia msikilizaji kuwa anatakiwa kujifunza kujidunga sindano ni kuwa hakuna mtu atakuwa akimdunga sindano.

### b) Utoaji mfano

#### MF20:

**(Muktadha: Mazungumzo ya kijamii. Wasailiwa R na S wanapeana ushauri.)**

| Kikisii  | Kiswahili   |
|--|---|
| <p><b>S:</b> Ase bono monto tokonyara koganyerera gento kemo gioka</p> <p><b>R:</b> Yaya! Mbuya abaremi basimeke ebimeri aoao <b>buna bono</b> ebituma amo na amatunda. Ekemo getracho koba nabo okonyora ekende kiabeire.....</p> | <p><b>S:</b> Kwa sasa mtu huwezi kungoja kiyu kimoja pekee</p> <p><b>R:</b> Hapana! Ni vizuri wakulima wapande mimea mbalimbali kama vile mahindi pamoja na matunda</p> |

- a) Mbuya abaremi basimeke ebimeri aoao. /**Buna bono** ebituma amo na amatunda M-buya a-ba-remi ba-simek-e e-bi-meri aoao. **Buna bono** e-bi-tuma amo na a-ma-tunda KIM-MZZ NGL-IDW-MZZ IDW-MZZ-K NGL-IDW-MZZ V **KUM(E-E)** NGL-IDW-MZZ U NGL-IDW-MZZ (Ni vizuri wakulima wapande mimea mbalimbali kama vile mahindi pamoja na matunda)

**(Muktadha: Mazungumzo ya kijamii. Mtafiti anashiriki mazungumzo na wazee fulani ambapo mmoja wao anaeleza jinsi maisha yalivyogeuka na kuwa magumu.)**

| Kikisii   | Kiswahili  |
|---|--|
| <p><b>S:</b> Ebinto biakongire oyonka. Iroka chiombe!</p> <p><b>R:</b> Chiombe chiakongire amagori. Buna bono tokonyora ngombe na ribu isano. Timanyeti nga ngai ense eye erochi.....</p> | <p><b>S:</b> Vitu vimekuwa ghali wa kwetu. Hasa ng'ombe</p> <p><b>R:</b> Ng'ombe wamepanda bei. Kama sasa huwezi kupata ng'ombe kwa elfu tano. Sijui hii dunia inaelekea wapi.....</p> |

- b) Chiombe chiakongire amagori. **Buna bono** tokonyora ngombe na ribu isano  
 Chi-ombe chi-a-kong-ire a-ma-gori. **Buna bono** ti-o-ko-nyor-a ngombe na ribu isano  
 NGL-MZZ NGL-NJ-MZZ-K NGL-IDW-MZZ. **KUM** (E-E) KAN-NFS2U-Kat-MZZ-IT N U N V  
 (Ngombe wamekuwa ghali. Kama sasa huwezi kupata ngombe kwa elfu tano)

VUM ambavyo vimetumika katika **MF20** vinatoa fafanuzi ambazo ni za kutoa mifano. Katika **MF20a** **KUM ‘buna bono’** kimetumika katika kutoa mifano ya aina mbalimbali za ‘ebimeri (mimea) ambayo inazungumziwa katika utungo wa kwanza wa matini hii. Aidha, **KUM ‘buna bono’** ambacho kimetumika katika **MF20b** kimetumika ili kutoa maelezo kwa kutoa mifano. Kinatoa mfano kuwa mtu hawezi kupata ng’ombe kwa shilingi elfu tano. Tungo hii inafafanua zaidi tungo tangulizi ya matini hii inayoeleza kuwa bei ya ng’ombe imekuwa ghali.

## 5.2 Ufafanuzi

Utafiti huu ulibainisha kuwa katika matini semwa za Kikisii ufanuzi unaweza kuwa wa aina mbalimbali: rekebishi, katizi, dhihirishi, hitimishi, bainishi na hata rejelezi.

### a) Rekebishi

#### **MF 21:**

(Muktadha: **Mazungumzo ya kijamii. Wazungumzaji wawili G na H wanazungumza juu ya mwanamke fulani aliyeolewa na mwanamme ambaye si wa kabila lake**)

| Kikisii  | Kiswahili   |
|--|---|
| <b>G:</b> Aberi nigo abwatete akanywoma<br>omokungu ekabira<br><b>H:</b> Aa! Mokungu ori oye tari mogusii?<br><b>G:</b> Yaya tari mogusii! | <b>G:</b> Aberi alioa mwanamke wa kabila linguine<br><b>H:</b> Aa! Yule mkewe si mkisii?<br><b>G:</b> Hapana si mkisii!<br><b>H:</b> Hivyo ni wa kabila linguine? |

|   |  |
|---|--|
| <p><b>H:</b> Igo n'ekabira?</p> <p><b>G:</b> Nigo are omomaragori <b>korende</b><br/>akwane ekegusii tokomanya nga tari<br/>mogusii. Nigo arakwane nonya<br/>n'amangana amakongu<br/>y'ekegusii. Nonya n'echimbachero<br/>chionsi nachimanyete.</p> | <p><b>G:</b> Ni mmapragoli <b>lakini</b> akisema kikisii<br/>huwezi kujua kuwa si mkisii. Anaweza<br/>kusema hata maneno magumu ya kikisii.<br/>Hata methali yote anaifahamu</p> |
|---|--|

Nigo are omomaragori / **korende akwane ekegusii tokomanya nga tari mogusii**  
 Nigo a-r-e o-mo-maragori / **korende a-kwan-e e-kegusii ti-o-ko-many-a nga ti-a-r-i mo-gusii**  
 KIM NFS3U-MZZ-K KAT-IDU-MZZ **KUM** NFS3U-MZZ-K NGL-MZZ KAN-NFS2U-Kat-MZZ-IT KIM KAN-NJ-MZZ-IT IDU-MZZ  
 (Ni mmapragoli lakini akisema kikisii huwezi kujua kuwa si mkisii)

KUM ‘**korende**’ kimetumika katika **MF21** kwa madhumuni ya kurekebisha matarajio fulani. Katika **MF21**, inatarajiwa kuwa kwa kuwa mzungumziwa ni mmapragoli, Kikisii chake kingekuwa duni. Kinyume na hayo, inabainika kuwa Kikisii chake ni sanifu.

### b) Vikatizi

#### MF 22:

(Muktadha: **Mazungumzo ya kijamii. Wazungumzaji wawili James na Mikuro wanazungumza juu ya mwenzao aliyenunua shamba**)

| Kikisii   | Kiswahili   |
|---|---|
